ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed		-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	- Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	- Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Kumi – Tarehe 30 Juni, 2011

Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 213

Maandalizi ya Uchaguzi wa Mwaka 2015

Mhe. Asha Bakari Makame (Kny: Mhe. Kazija Khamis Kona) - Aliuliza:-

Katika Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar uliopita wananchi wengi walikosa haki yao ya msingi ya kuwachagua Viongozi wanaowataka baada ya kukosa Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, ambacho kilikuwa ni kati ya kielelezo muhimu kinachomuwezesha mwananchi kupata Kadi ya Uchaguzi.

Je, Mhe. Waziri, Serikali ya Awamu ya Saba imejipanga vipi kukabiliana na changamoto hiyo kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 213 naomba kutoa maelezo yafuatayo :

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ni kati ya kielelezo muhimu kinachomuwezesha mwananchi wa Zanzibar kupata kadi ya

uchaguzi na hatimaye kushiriki katika uchaguzi wa kumchagua kiongozi anayemtaka

Mhe. Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa watu waliojiandikisha kupiga kura katika uchaguzi uliofanyika Oktoba, 2010 ni 407,669 wakati idadi ya watu waliokuwa na vitambulisho vya ukaazi hadi kufikia Oktoba, 2010 ni 560,722. Hii ni dhahiri kuwa wapo wananchi wengi ambao tayari walikuwa na vitambulisho lakini wao wenyewe waliamua kutoshiriki katika uchaguzi huo.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Usajili wa kadi za vitambulisho wa Mzanzibar Mkaazi ni Taasisi ya Kudumu ambayo inaendelea kutoa huduma hiyo kwa wananchi wanajitokeza kubadilisha vitambulisho vyao pamoja na kusajili wananchi wanaotimiza masharti.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi wote ambao bado hawajachukua vitambulisho vyao Ofisi ya Usajili waende kuvichukua na wale waliotimiza masharti ya kupata vitambulisho hivyo waende kuomba kupatiwa vitambulisho ili kuepusha usumbufu wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, napenda nilihakikishie Baraza lako tukufu na wananchi wote wa Zanzibar kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Tume ya Uchaguzi tunaandaa mazingira mazuri kuondoa kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika chaguzi zilizopita, na kuhamasisha mazingira ya maelewano na kuzidisha kutoa elimu kwa umma ili wananchi wajitokeze kwa wingi katika uchaguzi mkuu ujao kwa kupata haki yao ya msingi ya kuchagua viongozi wanaowapenda.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa miongoni mwa mambo yaliyowafanya watu wasipate vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni matatizo yaliyojitokeza katika vyeti vyao vya kuzaliwa, wengine walikuwa navyo lakini vilikuwa vimebadilika ama herufi moja au imekaa sipo na wengine hawakuwa navyo kabisa, lakini wanatimia umri kwa mfano hata bibi yangu alikwenda lakini alikuwa hana cheti kwa hivyo hakupata.

Je, Mhe. Waziri unawaahidi nini wananchi kuhusu matatizo kama haya ambayo yamewanyima haki yao muhimu sana, lengo sio kupiga kura tu lakini kuna mahitaji mengine sana kwa kitambulisho hiki. Je, unawaahidi ni matatizo haya yatasawazishwa vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema nia ya serikali ni kuondosha usumbufu wa aina yoyote katika uchaguzi unaokuja, na Mhe. Mwakilishi hapa ameeleza mang'uniko yake kutokana na tatizo la kupatikana kwa vyeti vya kuzaliwa ama kwa wale wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa kupata hati ya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika jambo hili tutalichukua tukae na wahusika ili tuone namna gani tutarahisisha wananchi wetu waweze kupata hati za Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na kuwa Mhe. Waziri ameeleza kuwa hili tatizo atalichukua, lakini hiki kitambulisho cha kuzaliwa hata wale wenye vyeti vile vidogo hawana vyeti vya *register* kwani Sheha huwa anakataa kutoa fomu. Je, Baraza litaarifiwa lini kuhusu vyeti vile ambavyo sio vya *register* vya kuzaliwa ambavyo vijana wetu wanavyo na wanastahili kupata vitambulisho hivi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema awali kwamba serikali kwa kushirikiana na taasisi zake husika itachukua kila hatua kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata hayo yao ya msingi ya kupata kadi zao za Mzanzibari Mkaazi. Kwa hivyo, hizi kasoro ndogo ndogo ambazo waheshimiwa wanazieleza napenda tena kulihakikishia Baraza lako tukufu tutazichukua kuzifanyia kazi ili tatizo hilo liondoke na Wazanzibari wote kadi zao za Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake alikiri kwamba nia ya serikali ni kuwaondoshea usumbufu wananchi wake, na kwa kuwa tuna vijana wengi ambapo sasa hivi wamo katika maskuli yetu ya serikali na yale ya binafsi wanasoma na wanastahiki sasa kupatiwa vitambulisho kutokana na umri wao. Kwa kuwa idara hii iliwahi kufanya utaratibu pale mwanzo wa kuweka vituo vya kufanya ule uwandikishaji wa vitambulisho Mhe. Waziri haoni kwamba kuna haja ya serikali sasa hivi kwenda kuwafuata skuli ili kuwarahisishia wao kupata elimu na vile vile kuwapatia vitambulisho vyao kama raia waliokuwa wamekamilika hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ushauri wake ni mzuri tutaufanyia kazi tuone uwezekano kama idara yetu hiyo inaweza kuchukua jukumu hilo na kuweza kukamilisha kazi hiyo kwa ufanisi. Lakini kwa sasa Mhe. Naibu Spika, vituo vyetu viko katika Wilaya vinafanya kazi nzuri na nimeweza kuandikisha wananchi wengi sana, na ndio maana

mpaka hivi sasa kuna kadi za Mzanzibari Mkaazi 42,000 hazijachukuliwa katika vituo husika vya kadi za Mzanzibari Mkaazi.

Nam. 161

Mchango wa SMZ Katika Kuviwezesha Vyama vya Siasa

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Kny: Mhe. Omar Ali Shehe) - Aliuliza:-

Utaratibu unaotumika nchini mwetu wa kupata viongozi (Rais, Wawakilishi, Wabunge na Madiwani) ni kwa chaguzi kupitia vyama vya siasa vilivyopata usajili Kisheria.

Kwa kuwa Viongozi hao wa Zanzibar wanatokana na vyama vya siasa.

Je, Serikali ya SMZ kwa upande wake ina mpango gani wa kuviwezesha kifedha vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mkuu hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilshi swali lake Nam. 161 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli utaratibu unaotumika wa kuwapata viongozi wa Serikali ni kwa Uchaguzi Mkuu kwa kupitia vyama vya siasa vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 1992 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kifungu Nam. 13 (1) (d) cha sheria hiyo kinaelezea kuwa vyama vya siasa vitapata ruzuku kutoka Serikalini. Vile vile, kifungu Nam. 16 (1) kinaelezea kuwa Serikali itatoa asilimia isiyozidi mbili (2%) ya matumizi yake ya kawaida ya mwaka baada ya kuondoa malipo ya deni la taifa kama ni ruzuku kwa vyama vya siasa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, vyama vya siasa ni suala la Muungano na sheria Nam. 5 ya mwaka 1992 ya vyama vya siasa imetoa nafasi ya kupatiwa ruzuku vyama vya siasa.

Mhe. Naibu hata hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia sheria Nam. 6 ya 1997 nayo imeweka ruzuku kwa vyama vya siasa, ruzuku hiyo isipungue asilimia moja (1%) ya bajeti ya kawaida ya mwaka. Hata hivyo, nia ya Serikali ni nzuri lakini kutokana na uwezo mdogo tumeshindwa kuvipatia vyama vya siasa ruzuku.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu yake Mhe. Waziri amekiri wajibu wa serikali kwa kuchangia hivi vyama vya siasa. Mimi napenda nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Inapofika muda ule wa kuchangia serikali je, serikali inachukua jukumu la kuwaandikia vyama vya siasa na kuwaarifu upungufu wake wa kifedha na wajibu wake wa kuchangia.

b) Je, hilo lihesabiwe kwamba ni deni katika vyama vya siasa au wamewaandikia vyama wawasamehe kutokana na ukosefu wa fedha hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba sheria ya Zanzibar kifungu Nam. 4(1) kiko wazi kinampa nguvu Waziri wa Fedha hali ya uchumi itakapokuwa nzuri aweze kuvisaidia vyama vya siasa. Kimsingi na ni imani yangu kwamba kama hawajapata fedha hizo katika mwaka nina amini Makatibu Wakuu wa vyama watachukua kwamba jibu ni kifungu Nam. 4(1) cha sheria hiyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kutunga sheria ambayo haiwezi kutekelezeka katika nchi yetu kwa sababu napenda kukiri kama kweli serikali yetu ni nyonge, haina uwezo kwani uwezo wake ni mdogo lakini kutunga sheria ambayo haiwezi kutekelezeka katika nchi yetu. Je, hamuoni kama ni kuipaka matope serikali hiyo na kama hivyo ndivyo je atakubaliana na mimi kama wakati wa uchaguzi mkuu vyama vinakuwa na gharama nyingi za uchaguzi, kwa hiyo kuna haja ya kuwasaidia japo kidogo cha asilimia kinachotakikana ili kuviwezesha vyama viweze kufanya kazi zake.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nikubaliane nae Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wa uchaguzi vyama vyetu vya siasa kwa sababu ya uchanga wake vinakuwa na gharama kubwa sana, na kwa kweli kuna haja kubwa sana kwa serikali kuvisaidia vyama vyetu vya siasa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nataka nitoe taarifa tu kwa Waheshimiwa Wajumbe kwamba mapungufu ya sheria yoyote ile unayajua baada ya kuitekeleza ile sheria, mimi binafsi nimeipitia sheria hii na nimeona kwamba muda muafaka sasa umefika wa kuifanyia marekebisho sheria hii. Kwanza kima ambacho kimewekwa kwa mujibu wa muono wangu ni kikubwa mno, lakini vile vile kima kilichowekwa kinasema kisipungue asilimia 2 tofauti na ile ya Muungano ambayo inasema isizidi asilimia 1. Kwa hivyo, kama kisipungue asilimia 2 halafu kinajumuisha madeni ya serikali kwa hivyo kima ni kikubwa na mimi ninashawishika wizara inayohusika tulete marekebisho ya sheria hii ili tuweze kuitekeleza kama ilivyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa huu ni mwaka wa 13 tangu tuingie katika mfumo wa vyama vingi vya siasa na kwa kuwa tangu kuanzishwe serikali bado haijapata uwezo na wala haina dalili ya kupata uwezo wa kuvisaidia vyama vya siasa. Je, kuendelea na kutowapa ruzuku vyama vya siasa si kudhalilisha hivi vyama kufanya shughuli zake na kama serikali inaendelea kuwa haina uwezo si bora tukarudi katika mfumo wa chama kimoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimshauri tukirudi katika chama kimoja basi iwe ni CCM. Mhe. Naibu Spika, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi nia ya serikali ni nzuri sana lakini kama nilivyoeleza kwamba kifungu hiki ukipiga mahesabu utaona ni fedha nyingi sana tunazotakiwa tutoe. Mimi nataka nitoe ushauri tu tukifanyie marekebisho kifungu hiki tukiweke wazi kwamba isizidi asilimia 1 na tutoe mikopo kwa sababu bajeti ya kawaida inajumuisha mikopo na ukisema kisipungue asilimia 2 ni pesa nyingi sana. Ndio maana serikali muda wote imeshindwa kuzitoa pesa hizo, lakini nia ni nzuri tukifanyie marekebisho baada ya hapo mimi nina imani sana serikali itakuwa inachangia katika kutoa ruzuku.

Nam. 2

Idadi ya Skuli za Sekondari Zanzibar

Mhe. Rashid Seif Suleiman - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi za kujenga na kuongeza idadi ya Skuli za Sekondari nchini mwetu kwa lengo la kuimarisha maendeleo ya elimu.

(a) Je, Mhe. Waziri kuna skuli ngapi za Sekondari za Unguja na Pemba.

(b) Vigezo gani vinavyotumiwa katika kuzifanya skuli za msingi kuwa za Sekondari.

(c) Je, ni wanafunzi wangapi wanaosoma masomo ya sayansi katika skuli hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 2 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Skuli za Sekondari ziliopo Unguja na Pemba ni 226 kati ya hizo 198 ni za Serikali na 28 za watu au mashirika binafsi. Kati ya Skuli za Sekondari za Serikali, Skuli 119 ziko Unguja na 79 ziko Pemba.

(b) Vigezo vinavyotumika katika kuzigawa skuli za msingi na kati na kuzitenganisha kati ya msingi na sekondari ni hivi vifuatavyo:-

i) Kuwepo kwa wanafunzi wa kutosha na madarasa ya kuwezesha kutenganishwa baina ya skuli ya msingi na sekondari.

ii) Kuwepo kwa walimu wa kutosha wa kuweza kufundisha madarasa ya msingi na sekondari bila ya kuathiri ufanisi wa kazi zao.

iii) Kuwepo majengo yanayoweza kugawika na kuwezesha kuwa na skuli mbili tofauti moja ya msingi na nyengine ya sekondari.

c) Wanafunzi wa kidato cha kwanza na cha pili wote wanasoma sayansi. Idadi ya wanafunzi hao ni 45,629. Kwa upande wa kidato cha tatu na cha nne wapo wanafunzi 11,678 wanaosoma masomo yote ya sayansi.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

a) Kwa kuwa katika majibu yake ya swali (b) alitaja vigezo vinavyotumika katika kufungua skuli za sekondari kutoka skuli ya msingi. Kama vigezo hivyo vinafuatwa kwa nini walimu wanashtukizia ndani ya msimu wa kutangaza matokeo kuona kwamba skuli yao inapata darasa la 11 la sayansi wakati hakuna

matayarisho yoyote, inatokezea vipi hata ikawa vigezo hivi wao wenyewe wizara hawavifuati.

b) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alitaja kwamba katika kuweka skuli ya sekondari kutoka msingi kuwe na walimu wa kutosha, lakini hali ya maskuli yetu si ya kutosha walimu wa sayansi. Je, wizara huwa haina taarifa kamili ya walimu walioko katika skuli zao hata ikawa wanafungua bila ya kuwa na walimu wa kutosha.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (anaendelea) Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwenye swali mama, vigezo ambavyo vinatumika katika kuzigawa hizi skuli sio kweli kwamba walimu hawashauriwi, wao wenyewe walimu ndio wa kwanza ambao wanapendekeza na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikenda kutizama kama hivi vigezo ambavyo nimevizungumza hapa vipo ndio tufungue sekondari. Hata Waheshimiwa Wawakilishi wao huwa wa kwanza kuja wizarani kutwambia skuli yetu hii sasa imefikia kuwa ni skuli ambayo tunahitaji kuwa na sekondari. Kwa hivyo, si kweli kwamba Wizara ya Elimu tunazishutikiza, hatuwezi kushitukiza Mhe. Naibu Spika, bila ya kufuatilia au maombi husika kwa watu wahusika kuleta maombi yao.

Swali la pili, nilizungumza kwenye swali langu la jibu mama hapa kwamba kuwe na walimu wa kutosha. Kama alivyosema Mhe. Rashid tatizo la walimu wa sayansi Mhe. Naibu Spika, ni tatizo ambalo tunalo Zanzibar nzima. Kwa hivyo, wale kidogo tulionao katika skuli tunawagawa hivyo hivyo kidogo kidogo kuhakikisha ile azma nzuri ya Idara ya Elimu na skuli yenyewe husika inafikiwa. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi vile vile niungane na Mhe. Rashid Seif wa Jimbo la Ziwani kuwa nitaipongeza serikali kwa kujenga skuli nyingi. Je, Mhe. Naibu Waziri katika skuli hizo wanazojenga hivi sasa atatuhakikishia vipi kuwapa hatimiliki kutokana na maeneo hayo ya maskuli na vyuo kuvamiwa na wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Elimu haisimamii hatimiliki za skuli, suala hili hivi sasa limekabidhiwa rasmi kwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, hati na mali zote za serikali basi ni Wizara ya Fedha ambayo inasimamia hati hizo.

Nam. 30

Tatizo la Kibofu cha Mkojo kwa Wananchi wa Jimbo la Kiwani

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa, wanaume wengi kati ya wananchi wa Jimbo la Kiwani hususan Wadi ya Mwambe, wamekuwa wakisumbuliwa na matatizo ya haja ndogo yaliyosababishwa na changarawe za mawe (*calcium*) wakati wa kujisaidia na sabu nyenginezo. Aidha, pale wanapofanya uchunguzi wa kimaabara, wengi kati yao hugunduliwa kuwa wameathirika katika vibofu vyao vya mkojo.

(a) Je, Mhe. Waziri, kuna sababu zipi zinazopelekea matatizo hayo.

(b) Kwa kuwa tatizo hili ni sugu na linaendelea kupoteza maisha na nguvu kazi ya wananchi wetu. Kwa nini Serikali haifanyi zoezi maalum la kufanya vipimo vya haja ndogo kwa wananchi wote wa jimbo hilo, ili kugundua ukubwa na sababu za tatizo hilo.

(c) Kuna sababu zipi zinazopelekea wanaume waathiriwe zaidi na tatizo la vibofu vya mkojo kuliko wanawake.

(d) Kuna uhusiano gani kati ya matatizo ya mkojo na saratani ya kibofu cha mkojo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa sasa haina taarifa za kutosha za kuwepo maradhi hayo katika Jimbo la Kiwani hasa katika Wadi ya Mwambe. Aidha, uchunguzi wa tatizo hili unafanyika kwa kutumia *"Ultra Sound, X-ray na Cystoscope"* hii inamaanisha kuwa tatizo hilo halichunguzwi kwa vifaa vya maabara kama ilivyoelezwa katika swali la Mhe. Mwakilishi.

(a) Kwa faida ya Mhe. Mwakilishi na wananchi wote kwa ujumla, napenda kuwafahamisha kuwa sababu zinazopelekea kuwepo kwa changarawe katika mafigo na vibofu vya mkojo ni nyingi zikiwemo:-

- Kuongezeka kwa '*calcium'* katika maji au chakula.

- Tatizo la watu kufanyakazi juani kwa muda mrefu, kutoka jasho kwa wingi bila ya kunywa maji ya kutosha kurejesha yale yanayopotea mwilini.

(b) Kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi wa suala hili kwamba wizara yangu haina taarifa za kuwepo kwa tatizo hilo. Aidha, takwimu tunazozipokea kutoka katika hospitali na vituo vya afya kikiwemo kituo kinachotoa huduma za afya kwa wananchi wa Mwambe (Kiwani), hazijaonesha kutokea vifo kwa sababu ya tatizo hilo.

(c) Kawaida tatizo la changarawe ndani vibofu vya mkojo linawaathiri watu wa jinsia zote. Pengine Mhe. Mwakilishi utakuwa umelchanganya na tatizo la kukua kwa tezi la kibofu cha mkojo (*Benign Prostate Hypertrophy*), ambalo kutoka na sababu za maumbile na ni maradhi ya wanaume tu.

(d) Uhusiano mkubwa uliopo baina ya matatizo ya mkojo na saratani ya kibofu cha mkojo ni:-

- Usugu wa maradhi yanayoathiri mfumo wa njia ya mkojo (*urinary system*) kwa mfano kichocho na maradhi ya kuambukiza katika njia ya mkojo yaliyokuwa hayakutibiwa vizuri.

- Mabadiliko ya tezi la mkojo kwa wanaume.

Kutokana na sababu hizo kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha kujitokeza kwa saratani ya kibofu cha mkojo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali la nyongeza lenye vifungu a, b na c.

(a) Kwa kuwa amekiri kwamba wizara yake haina taarifa ya suala hili na kwa kuwa moja ya jukumu la Idara ya Mipango na Utafiti ni kufanya utafiti wa matatizo ya wananchi, na kwa kuwa mimi niliyeuliza swali hili ni mkaazi wa Mwambe na nimeyashuhudia matatizo haya. Je, atakuwa tayari sasa kufanya utafiti maalum kwa watu wa Mwambe ili kujua ukuwa wa tatizo hili.

(b) Amejibu kwamba hakuna vifo vilivyotokezea kutokana na tatizo hili, naomba kumuuliza aliyejibu swali hili na mimi niliyeuliza ni nani mwenyeji wa Mwambe.

(c) Hivyo ikiwa kufanya kazi kubwa juani ndio tatizo moja wapo la mchangio wa suala hili, na kwa kuwa watu wa Mwambe hawana viwanda, nini ushauri wake juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie swali lake la (c)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe, Naibu Spika, ni kwamba Mhe. Naibu Waziri amesema sababu moja inayochangia ongezeko la maradhi haya ni kufanya kazi juwani kwa wananchi ambao hupoteza jasho jingi na kutokunywa maji ya kurejesha jasho hilo. Nimesema kwamba, kwa kuwa wananchi wa Mwambe wanafanya kazi za kilimo zaidi na hakuna viwanda nini ushauri wake juu ya suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe naomba nimfahamishe kitu kimoja, tafiti zinafanywa baada ya kupatikana sababu na nimesema Wizara ya Afya haijapata taarifa. Kwa hivyo, sina msingi wa kujengea kufanya utafiti. Wizara ya Afya inapata taarifa kutokana na rikodi na ripoti zinazotolewa na watu wa Wilaya ambao wanahusika na afya, katika hizo taarifa tunazopewa hamna kitu hicho, kwa hivyo, sina sababu ya kujengea hoja kufanya utafiti. Sio kwamba sitaki, nataka lakini nitafanya utafiti kwa kithibitisho kipi na taarifa hazioneshi hivyo.

Swali la kuwa nani anakaa Mwambe ni wewe mimi sikai huko, vifo vikitokea vinatokea huko mimi sivioni, lakini ingekuwa angalau kumefanywa *postmortem* nikathibitisha kwamba kweli wamekufa kwa sababu hiyo ningekubaliana na wewe, lakini wanakufa huko siwaoni, wanazikwa huko siwaoni halafu unambie wamekufa kwa mawe, hilo sikubaliani nalo.

Suala (c) anasema Mwambe hakuna viwanda, wananchi wanalima kwa hivyo inakuwaje? Kwani wanalima wapi, kivulini hawalimi juani? Na Mwambe si kunakatwa matofali kule watu kutwa wanashinda juani, kubali kwamba jua ndio tatizo kubwa wambie watu watumie maji kwa wingi tatizo litapungua.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Mhe. Hija Hassan katoa taarifa kwamba kuna tatizo hilo katika jimbo lake la Kiwani. Je, Mhe. Naibu Waziri kuna mpango gani wa kulifuatilia suala hili ili kuweza kulijua.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, huwa tunafuatilia taarifa kama hizo kwa kupitia kwenye ripoti zetu za wilaya. Ripoti za wilaya ikionesha hivyo sisi kama serikali na wizara hilo tutalifanyia kazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniruhusu kuuliza swali dogo sana la nyongeza. kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri katika kujibu swali la msingi amesema kwamba hivi vijiwe katika *urinary passages* mara nyingi husababishwa na *calcium* au chokaa, na kwa kuwa Mwambe, Kengeja, Wawi mpaka Micheweni maji yake yana *calcium* nyingi. Sasa swali la mwanzo. Je, anaweza kutupa ushauri gani wa kitabibu sisi wananchi tunaokaa katika *far Eastern belt* ya kule Pemba.

La pili Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri kakiri kwamba wizara yake haijapata taarifa pamoja na mambo yote yaliyotokea Mwambe. Je, isingekuwa vyema kwa wizara yake kuanzisha *mobile doctors* kusudi wakaweza kupita au kuzunguka katika visiwa vya Unguja na Pemba ili kuona matatizo ya magonjwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya haihusiki na maji, nitamuomba Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alishughulikie suala hilo. Kwa sababu yeye ndiye atakayeweza kusema kama kuna *calcium* au hakuna. Sisi tunashughulika na wagonjwa wanaokuja pale baada ya kunywa maji. Kwa hivyo, nafikiri watu wa maji wapo na wameshalisikia naomba walishughulie ni tatizo lao.

Swali la pili ameshauri tufanye *mobile doctors* ili kuweza kuzunguka. *Mobile doctors* wanahitaji watu, wanahitaji vifaa, watu nao wapungufu, lakini kuna *mobile doctors* ambao wanajitolea *ZOP*, nitawaomba katika ziara zao wapite na Mwambe na hizo sehemu ulizozitaja walishughulikie hili.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Saleh Nassor nashukuru kwamba kumbe maeneo mnayoishi mnaelewa kwamba yana *calcium* nyingi sana, katika jibu la msingi la Mhe. Naibu Waziri alisema moja katika sababu ni wingi wa *calcium*. Ulitaka tukushauri ufanye nini? Ni kuchemsha maji kabla ya kunywa, unapochemsha maji *calcium* inabaki unapata maji safi.

Swali la Mhe. Hija kwa sababu umetupa taarifa kwamba kuna tatizo hilo kwenye eneo lako, tutawaomba wataalamu wetu wafuatilie kuona ukweli ukoje.

Nam. 114

Serikali Kuendeleza Kilimo cha Kisasa kwa Wakulima wa Jimbo la Chaani

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mhe. Ussi Jecha Simai) – Aliuliza:-

Wananchi wengi wa Vijiji vya Gamba, Moga na Chaani katika Jimbo la Chaani, wanaojishughulisha na ukulima wa mboga mboga hutegemea mvua na wakati wa kiangazi husitisha shughuli zao za kilimo kwa kukosa maji, hali ambayo huchangia umasikini kwa wananchi ambao kwa kipindi kirefu cha mwaka hukosa shughuli ya kufanya ili kujiongezea mapato.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wananchi hawa ili waweze kujishughulisha na kilimo cha uhakika, kisichokuwa cha msimu kwa kukosa maji.

(b) Je, Serikali iko tayari kuwatafutia shughuli ya kufanya wananchi hawa ili kuongeza kipato chao katika kipindi cha kiangazi.

(c) Je, Serikali iko tayari kupeleka wataalamu kwa wananchi hawa ili pamoja na mambo mengine, kusaidia upatikanaji wa mbegu bora na kutoa mbinu bora za kilimo cha kisasa.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 114 lenye vipengele a, b, na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, katika programu za wizara yangu katika mwaka huu wa fedha, tayari mpango wa kuvuna maji ya mvua umeainishwa vizuri kwa vilimo vyote. Mpango huu tayri umeshaanza kutumika katika baadhi ya mabonde kupitia miradi ya *PADEP* na *TASAF*.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuweka mpango mzuri wa kilimo cha umwagiliaji maji, kuna uhakika kwa wananchi hao kuweza kulima wakati wowote hata wakati wa kiangazi na wataweza kujiongezea kipato chao. Aidha, kuhusiana na suala la kupeleka wataalamu wizara yangu haina pingamizi na hilo na hasa ukizingatia kuwa tunao wataalamu wanatoa huduma na ushauri wa kitaaalam kwa wakulima. Hata hivyo, wizara iko katika maandalizi ya kuajiri wataalamu wapya wa ngazi ya cheti ambao wamemaliza Chuo cha Kizimbani ili kupunguza uhaba wa wataalamu uliopo sasa na juhudi hizo ni endelevu.

Nam. 65

Uendelezaji Sekta ya Mifugo

Mhe. Salmin Awadh Salmin - Aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya mifugo inawajibu wa kupanga na kuratibu maendeleo ya mifugo ikiwa ni pamoja na kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji. Na kwa kuwa utoaji huo wa taaluma utasaidia kuufanya ufugaji uwe wa kibiashara na tija na kuongeza mchango katika pato la Taifa.

(a) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako inatekeleza vipi wajibu huu.

(b) Je, Mhe. Waziri, ule mkakati wa kuyaendeleza mashamba ya mifugo ya Serikali kwa nia ya kuwapatia wananchi mifugo bora, umeishia wapi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake Nam. 65 lenye vifungu a, na b.

Mhe. Naibu Spika, nakubalina na Mhe. Mwakilishi kuwa Sekta ya Mifugo pamoja na mambo mengine inawajibu wa kupanga na kuratibu maendeleo ya mifugo ikiwa ni pamoja na kutowa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji na kuwa na ufugaji wa kibiashara wenye tija na kuongeza mchango katika pato la taifa.

a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inatekeleza wajibu huo kwa kutaaluma ya ufugaji kwa kushirikiana na Programu ya Kuimarisha Sekta ya Kilimo na Mifugo *ASDPL* inayosimamiwa na Wizara ya Mifugo na Maliasili. Hivi sasa skuli mbali mbali za wafugaji zimeanzishwa kwenye Wilaya zetu Unguja na Pemba, jumla yake ikiwa ni 312. Skuli zote hizo zinasaidia sana kutoa taaluma juu ya mbinu bora za uzalishaji, kuwa na ufugaji wa kibiashara na kuongeza pato la taifa. Aidha, katika kupanga na kuratibu Sekta ya Mifugo, wizara yangu hivi sasa imo katika hatua za mwisho za kuipitia Sera ya Mifugo ambayo mabadiliko yake yatabainisha kwa upana zaidi wajibu wa kila mshiriki wa Sekta ya Mifugo katika kuimarisha taaluma, ujuzi na maarifa pamoja na uzalishaji na soko la bidhaa za mifugo.

b) Ule mkakati wa kuyaendeleza mashamba ya mifugo ya serikali kwa nia ya kuwapatia wananchi mifugo bora, bado unaendelezwa kwa kuingia katika mazungumzo na waekezaji wa ndani na nje katika kuanzisha ufugaji wa mkataba baina ya wananchi na wawekezaji kwa kutumia mashamba hayo. Hivi sasa wizara yangu imo katika hatua za majadiliano na wawekezaji kadhaa.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inaamini na ina matumaini makubwa kwamba uwekezaji huu utapoanza utasaidia sana kuendeleza mikakati ya kuyaendeleza mashamba ya mifugo na ufugaji kwa ujumla.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba niulize kwamba Mhe. Waziri katika kutekeleza wajibu huo ambao umeueleza, unao wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ni hakika kwamba nina upungufu mkubwa wa wataalamu, jambo ambalo nalifanya hivi sasa ni kutafuta utaratibu wa kufundisha vijana hasa waliomaliza darasa la kumi na nne katika masomo ya sayansi. Wiki mbili zilizopita wizara yangu ilitangaza katika redio kwamba, wale vijana waliomaliza darasa la kumi na nne katika masomo ya sayansi basi waripoti katika ofisi zangu za wizara Unguja na Pemba kwa ajili ya kutafuta namna ya kuwaendeleza kimasomo ili hatimaye wawe wataalamu bora katika sekta ya mifugo katika visiwa vyetu na wilaya zetu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. serikali ya iliyopita ya awamu ya sita ilikuwa na mtindo ili kuwakwamua watu katika umasikini kuwasaidia kuwapa mifugo kwa ajili ya kufuga kwa kujikwamua na umasikini. Sasa serikali hii ya awamu ya saba mpango huo upo. Kama upo kipindi kilichopita alikuwa mtu anapewa mbuzi mmoja au kuku, au watu 20 wana kuku watano au mbuzi wawili. Je, awamu hii serikali imejipanga vipi. Kwa sababu kuwapa watu mbuzi mmoja ni kuwarudisha pale pale kwenye umasikini. Je, awamu hii wizara yake imejipanga vipi kuwapatia watu mbuzi au kuku hata ng'ombe ili waweze kufanya biashara ya kujiendeleza na sio mbuzi mmoja.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, mpango ule wa awamu ya sita serikali ambapo wizara ilifanya kazi nzuri bado upo na utaimarishwa zaidi. Kama nilivyosema kwamba hivi sasa tumo katika majadiliano na wawekezaji watano, lengo ni kuanzisha uwekezaji wa mkataba baina ya mwekezaji na mwananchi. Sasa kwa utaratibu huu si suala la kupewa mbuzi watatu, wawili au mmoja, hutegemea na nguvu ya mwananchi

mwenyewe na utayari wake wa kufuga. Kwa hivyo, utaratibu upo na utaimarishwa zaidi na muda si mrefu grogramu hizi zitaanza.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yake kasema kuwa kuna mpango wa kuagizishia madume bora ili kupata kizazi bora kwa wafugaji wetu. Na haya ni mambo ambayo yanategemea uwezo wa mirathi ya hizo sifa tunazozitafuta baina ya jike na dume, wakati mwengine tunafanikiwa na wakati mwengine tunafeli na hata vizazi vifuatavyo. Je, Mhe. Waziri badala ya kufanya mpango huu wa *experiment error* ana utaalamu gani anaoutumia wa kisayansi na kuhakikisha kuwa hicho kitakachozaliwa kitaleta tija iliyokusudiwa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuna utaratibu wa kufanya kazi zetu kwa kutumia wana sayansi hatufanyi kwa kubahatisha. Kwa hivyo, madume bora ambao wanakwenda kununuliwa ni aina ya kabila ambayo tayari imeshafanyiwa utafiti siku za nyuma na wameonekana kwamba, kwa mazingira ya nchi yetu yana uwezo wa kuhimili mazingira lakini pia ya kuweza kutoa maziwa mengi. Sasa utafiti umefanywa siku za nyuma, umejaribiwa katika sehemu mbali mbali za nchi yetu na tumefikia muwafaka kwamba hii ni aina ya ng'ombe ambao kwa mazingira ya nchi yetu basi watakuwa na tija kubwa zaidi.

Nam. 24

Mpango wa Kuondosha Meli Zinazofunga Forodhamchanga

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Inaonekana serikali ina mpango ya kuzihamisha meli zinazofunga kwenye eneo la Forodhamchanga na kuzipeleka kufunga karibu na mahali yanapofunga maboti ya abiria, bila ya kufanya upembuzi yakinifu juu ya hasara na faida zitazopatikana.

(a) Je, serikali inafahamu kuwa mahali ambapo meli hizo zinatakiwa kufunga panaweza iwe ni kero zaidi kwa meli za abiria na kwamba wakati wa upepo itakuwa ni hasara zaidi.

(b) Je, serikali inatambua kuwa pale Forodhamchanga meli hizo ni kivutio kikubwa cha watalii ambao huwa wanapanga foleni kuziangalia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-
Bandari ya Malindi ni bandari inayotoa huduma kwa vyombo vya aina mbali mbali vinavyoleta au kuchukua mizigo Zanzibar, zikiwemo Meli za aina ya *"Land Craft"* ambazo baadhi yake zinahudumiwa Forodhamchanga. Matatizo makubwa yanayojitokeza hapo Forodhamchanga yanatokana na ufungaji wa vyombo hivyo vya mizigo katika eneo hilo ni pamoja na:-

- Vurugu na msongamano mkubwa wa magari katika barabara ya Forodhani hasa eneo la karibu na Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*).

- Magari ya mizigo yenye uzito mkubwa zaidi ya tani mbili kuingia katika eneo la Mji Mkongwe kitendo ambacho ni kinyume na Sheria za Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

- Hatari kubwa ya uingizaji wa mizigo au vitu visivyoruhusiwa kuingizwa nchini (ikiwemo silaha na madawa ya kulevya) kinyume cha sheria kutokana na udhibiti mdogo wa Forodha katika eneo hilo.

- Kutokana na udhibiti mdogo wa eneo hilo kunakisiwa kuwepo na upotevu wa mapato ya serikali yanayotokana na uingizaji wa mizigo hiyo nchini.

- Uchafuzi wa mazingira ya eneo hilo pamoja na muonekano mbaya wa sura na haiba ya Mji Mkongwe.

Kutokana na matatizo yote hayo, wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Bandari imefanya utafiti wa kina na kuona kuwa matatizo yanayotokana na ufungaji wa vyombo hivyo hapo Forodhamchanga ni makubwa na ndio sababu ya kuona ipo haja ya kuhamishwa shughuli hizo na kuwekwa eneo la karibu na gati ya abiria.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, eneo limetayarishwa kwa kujengwa Chelezo (*Ramp*) cha kuegeshea vyombo aina hiyo na vitahudumiwa kwa mpango maalum ili kuepusha usumbufu kwa vyombo vya abiria vinavyofunga katika gati ya abiria.

Aidha, udhibiti wa uingizaji na usafirishaji wa bidhaa kiforodha utakuwa ni bora zaidi pamoja na mpango mzima wa utunzaji wa mazingira na fukwe pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe.

Mhe. Naibu Spika, kitendo hicho cha kufunga meli eneo la Forodha Mchanga ni usumbufu mkubwa na ni kero kubwa kwa wananchi, wavuvi wa eneo hilo pamoja na watumiaji wengine wa huduma za benki hasa Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC).*

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na uwepo wa watalii wengi wanaoangalia magari na mizigo mbali mbali inayoshushwa na kupakiwa katika eneo hilo. Inawezekana kwamba uwepo wa watalii hao ikawa ni kwa kutushangaa na sio kwa kupendezewa na huduma hizo katika eneo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kuwa hiyo hali hatoweza kuidhibiti kwa muda huu kutokana na mfano hai ofisi yake iko mbele yake wakati wa saa nane na wakati wa magharibi njia ile haipitiki mpaka kukodiwa askari wa ziada kuja kutatua matatizo ya pale.

(a) Je, atakubaliana nami kwamba hapa anapopazungumza hivi sasa ma-*speed boat* yaliyokuwepo pale hayakidhi eneo lile.

(b) Je, atakubaliana nami kuwa matatizo yoyote yatakayotokea pale shirika lake ndio litakalokuwa dhamana wa usalama wa vyombo vile ili wananchi wapate kujua suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoeleza katika jibu mama Shirika la Bandari linaandaa utaratibu mzuri wa kuweza kusafirisha mizigo. Matatizo yaliyopo ya kutokana na msongamano wa magari Shirika la Bandari tumelizingatia, tumejiandaa na naamini utaratibu ambao tunakusudia kufanya hautokuwa kikwazo wala hautosababisha usumbufu wowote wa misongamano ya gari barabarani.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Mwakilishi a-*declare interest* katika eneo hili. Shirika la Bandari kwa mujibu wa sheria iliyoanzishwa serikalini ndio yenye dhamana ya uingizaji meli katika eneo la bandari, upakiaji na upakuaji wa mizigo ndani ya meli hizo. Kwa mnasaba huo kama litatokezea tatizo lolote kwa vyombo katika eneo la bandari kwa vyovyote ilivyo Shirika la Bandari ndio dhamana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ufungaji na maegesho baharini hutegemea sana na mnara wa mawasiliano

(signal tower). Taarifa nilizonazo sasa ni wiki moja *signal tower* haifanyi kazi. Je, hili ni kweli, kama ni kweli kuna ufanisi gani wa huduma hii bandarini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyingi mawaziri wamekuwa wakisimama na kusema kwamba si vyema na si busara kwa viongozi tuliomo ndani ya jengo hili kuleta taarifa kwa kusikia dhana tu. Naomba sana tunayoyasema tuwe tuna uthibitisho nayo. Napenda kumhakikishia kwamba dhana hiyo anayoisema sio kweli na huduma hiyo bado ipo na inaendelea.

Nam. 85

Idadi ya Watalii Walioingia Nchini Miaka 5 Iliyopita

Mhe: Asha Abdu Haji - Aliuliza:

Inaaminika kwamba SMZ imeanzisha Sekta ya Biashara ya Utalii kwa dhamira ya kukuza uchumi wake.

(a) Je, ni watalii wangapi walioingia nchini mwetu kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.
(b) Katika kapindi hicho Serikali ilikadiria kukusanya kiasi gani ikiwa ni kodi za aina mbali mbali.
(c) Katika makadirio hayo ni kiasi gani cha fedha kilipatikana na kwa kiasi gani kilichangia kukuza uchumi wa Zanzibar.
(d) Pamoja na kwamba vijana wengi wa hapa nchini wamepata mafunzo ya utalii katika vyuo vinavyotambulika na kufaulu vizuri bado wawekezaji wengi wameng'ang'ania kuajiri wafanyakazi kutoka nje. Je, Serikali haioni kuwa kuruhusu jambo hilo ni kuwanyima fursa za ajira vijana wetu ambao ndio hasa wanaostahili kupata fursa hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 85 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya watalii 676,589 wameingia nchini kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kutoka mwaka 2006 hadi mwaka 2010. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo: Mwaka 2006 watalii 137,111, 2007 watalii 143,283, 2008 watalii 128,440, 2009 watalii 134,919, na 2010 watalii 132,836. Hata hivyo, idadi hii haijumuishi watalii kutoka Tanzania Bara ambao hawahesabiwi na Idara ya Uhamiaji kwa kuwa takwimu zetu tunazipata kutoka kwao.

(b) Napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba suala la makadirio ya kodi zinazotokana na utalii zitapatikana kutoka taasisi husika zinazokusanya kodi hizo. Nazo ni Bodi ya Mapato Zanzibar *(ZRB)* na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).*

(c) Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika kifungu (b) suala la kodi za utalii halipo katika Wizara yangu.

(d) Napenda kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu kwamba vijana wetu wanaomaliza mafunzo ya Utalii katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi wanaajiriwa katika Sekta ya Utalii. Aidha, wanafunzi wanaohitimu katika chuo chetu ni kidogo sana kukidhi mahitaji halisi ya uwekezaji uliopo. Katika kukabiliana na changamoto hii, Serikali imefanya juhudi za makusudi kuimarisha Chuo chetu cha Maruhubi ili kiweze kutoa wahitimu wengi na wenye ubora katika soko la utalii. Vile vile jitihada zinafanywa ili kuwapatia walimu mafunzo zaidi ili kumudu changamoto hizo.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amewaajiri walimu wangapi na wana kiwango gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, tumeajiri walimu saba na wenye kiwango cha *degree*.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la 85 (b) kuhusu kiasi cha kodi ambacho kimekusanywa alisema kwamba taarifa juu ya kiasi cha kodi hizo zinapatikana katika taasisi za kodi *TRA* na *ZRB.*

Je, serikali haioni kwamba wakati sasa umefika fedha zile zinazokusanywa kwa ajili ya utalii taarifa zake ziweze kupatikana katika wizara hii inayohusika na utalii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tunakubaliana na Mhe. Mwakilishi lakini tutakaa ili kuyarekebisha kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, tuna tatizo kubwa la uvujaji wa mapato yatokanayo na utalii. Kwa kuwa wizara hii ndio inayohusika na mambo ya utalii kwa maana ya uratibu pamoja na shughuli zote. Hii

inasababishwa kutokana na kuwepo ubabaishaji katika taasisi zinazoshughulika na masuala haya ya utalii. Kwa mfano, suala la Uhamiaji, *ZRB*, tuna watu wenye mahoteli, Shirika la Utalii, pamoja na Kamisheni ya Utalii.

Kwa sababu suala la utalii ni mtambuka unaohusisha taasisi zote hizi na kwa kuwa kuna kitu cha upoteaji wa mapato. Je, wizara yako ina utaratibu gani wa kuzishirikisha taasisi zote hizi ili kuona kwamba mapato haya hayapotei.

Swali (b) kwa vile watalii wengi wanaokuja nchini moja kwa moja hulipia viza zao nje ya nchi katika balozi zetu za Tanzania zilizoko kule. Je, wizara yako ina utaratibu gani wa kuhakikisha fedha zile zinazolipiwa katika ubalozi zinakuja moja kwa moja katika hazina ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna uvujaji wa mapato na suala hili tumeshalizungumza vile vile katika Baraza la Mapinduzi na limeundiwa kamati maalum ili kuhakikisha kwamba uvujaji wa mapato hautokei. Sio kwa sekta ya utalii tu bali kwa sekta zote ambazo zinapitia bandarini na uwanja wa ndege. Kwa hivyo, suala hilo hivi sasa tuko katika kulipitia upya ili kuhakikisha kwamba mapato hayavuji.

Mhe. Naibu Spika, swali (b) zaidi linahusu Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, wao ndio wanaohusika zaidi na mambo ya *policies* za ulipaji kodi au viza. Ni masuala ya Muungano vile vile. Lakini pamoja na hivyo tupo katika kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba fedha zote za watalii wanaokuja hapa basi ziwe zinakuja moja kwa moja. Kwa hivyo, naamini kwamba baada ya bajeti masuala hayo tutakuwa tumeshayarekebisha.

Nam. 58

Ufukiwaji wa Ufukwe Eneo la Maruhubi

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza**:**

Katika eneo la ufukwe usawa na Chuo cha Utalii Maruhubi kuna muwekezaji ambaye ametengeneza bustani kwa kufukia eneo la mchanga wa pwani na kuweka udongo kwa ajili ya bustani hiyo.

(a) Je, ufukiaji huu wa eneo la ufukwe si uchafuzi wa mazingira ya bahari na je, haukiuki masharti ya ujenzi katika maeneo ya ufukwe.

(b) Kwa mujibu wa mipaka ya chuo eneo hilo ni eneo la chuo. Je, ni utaratibu gani uliotumika kumpa muwekezaji eneo hilo ambalo ni mali ya Serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Baada ya kulifanyia ukaguzi eneo husika kwa kushirikiana na Maafisa wa Idara ya Mazingira tumegundua kwamba ni kweli kuna mwananchi ambaye anafukia eneo la bahari hapo Maruhubi kwa madhumuni ya kutengeneza bustani na kutanua hoteli yake.

Mhe. Naibu Spika, mwananchi huyo anafanya hivyo bila ya kibali cha Idara husika na tayari ameshapelekewa amri ya kusitisha zoezi hilo mara moja. Kitendo anachokifanya ni uharibifu wa mazingira hasa ukizingatia kwamba ufukiaji wake hauhusiani na miongozo ya kitaalamu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali inaahidi kuchukua hatua zaidi za kisheria ili kuhakikisha uharibifu huu wa mazingira hauendelei.

(b) Kuhusu suala la mipaka napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba eneo hilo ambalo uharibifu wa mazingira umefanyika, hili lipo nje ya eneo la Chuo cha Utalii Maruhubi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba wamechukua hatua za kisheria juu ya huyo mtu ambaye anafukia hilo eneo. Kwa sababu huyo mhusika anaendelea na utaratibu wake kama ambavyo hakuna habari yoyote. Je, ni hatua zipi ambazo amechukua.

Mhe. Naibu Spika, swali (b) hili eneo tunalolizungumzia la upande wa Chuo cha Maruhubi sijui Mhe. Waziri amewahi kufika na kuona eneo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, katika hatua tulizozichukua ni kumpelekea amri ya kusitisha mara moja zoezi hilo la kufukia katika sehemu hiyo. Mhe. Naibu Spika, tumesema iwapo ataendelea basi wizara yangu itashirikiana na taasisi mbali mbali katika kumchukulia hatua za kisheria si kama tayari tumemchukulia hatua.

Mhe. Naibu Spika, swali (b) tayari nimeona eneo hilo lakini kuona si tatizo, tatizo ni kuvamia na kuharibu mazingira.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kamati yangu ni miongoni ambayo imefanya ziara. Kwa kuwa tumeona uharibifu mkubwa sana ambao umefanywa na mteja huyu. Kwa kuwa si kwamba anaweka bustani tu, anajenga mpaka nyumba za kitalii.

Je, atakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri kwamba ni vyema tufanye ziara maalum kamati ambayo inashughulikia utalii, Waziri anayeshughulikia majenzi, *TRA* wanaotoa kibali cha utalii, pamoja na wanaohusika wote ili kwenda kuhakikisha kwamba pametokea uharibifu mkubwa sana hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimekiri kwamba uharibifu upo na naahidi kwamba nipo tayari kushirkiana na kamati hiyo kufuatilia na kama wanaendelea kumchukulia hatua za kisheria kama nilivyoeleza mwanzo.

Nam. 146

Utayarishaji wa Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna wachangiaji wanne tunavyokusudia saa tano tumwite Mhe. Waziri. Kwa hivyo, tujipange ili tuweze kwenda vizuri na ratiba yetu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipatia nafasi asubuhi hii ya leo kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Naibu Spika, pili nikushukuru wewe binafsi kukiongoza kikao hichi asubuhi ya leo. Mhe. Naibu Spika, mimi katika kuuokoa muda sitozungumza mambo mengi kwa sababu mengi yameshazungumzwa katika mijadala ya jana.

Mhe. Naibu Spika, nikianza mchango wangu nizungumzie vipaumbele ambavyo amezungumza Mhe. Waziri. Kipaumbele ambacho nitakizungumza mimi ni kipaumbele nukta tatu ambacho kinasema Kuimarisha na uongeza uwezo wa Idara maalum za SMZ. Mhe. Naibu Spika, hili ni suala zuri sana kuvipa uwezo vikosi hivi kwa ajili ya kujiimarisha vizuri katika kazi zake za kila siku.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningempa ushauri Mhe. Waziri kuhusiana na kuvipa uwezo vikosi hivi. Mhe. Naibu Spika, moja katika wazo langu kuhusu Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nizungumzie kuhusu habari ya JKU. Mhe. Naibu Spika, JKU wana maeneo makubwa sana ya kilimo hususan katika eneo la Jimbo la Chambani. Eneo la Chambani kuna kambi ya JKU ambayo imeanzishwa muda mrefu sana na ina eneo kubwa la kilimo na kilimo kikubwa walichokuwa wakilima hawa ni mpunga. Lakini kwa hivi sasa kilimo cha mpunga katika eneo hilo kimepitwa na wakati kutokana na hali ngumu ya hewa kwa sababu kuna upungufu wa mvua. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aweke mbinu mbadala ya kilimo na eneo hili ambalo lina ardhi nzuri liweze kulima kilimo cha mboga mboga.

Mhe. Naibu Spika, eneo la Chambani kambi ya JKU yameshafika maji ya mfereji kwa hivyo akiwezeshe kikosi hichi badala ya kulima kilimo cha mpunga ambacho kinakuwa hakina tija wapewe uwezo wa kulima kilimo cha mboga mboga ili kiweze kutoa tija na ubora wa zao hili la kilimo.

Mhe. Naibu Spika, pia katika kuvipa kipaumbele na kuviongoza vizuri vikosi hivi naomba tuvienzi. Miongoni mwa kuvienzi vikosi hivi ni kuwaenzi wale waasisi wa vikosi hivi.

Kwa mfano, kuna watu walioviasisi vikosi hivi tokea vilipoanza, ni vizuri baadhi ya kambi kupewa majina ya viongozi hawa. Kwa mfano, kule Pemba Vitongoji kuna kambi ya jeshi inaitwa *Ali Khamis Camp,* hili ni jina la kiongozi labda aliyeasisi kambi ile. Pia kuna kambi ya jeshi Bavuai bila shaka ni jina la mmoja katika viongozi wa kambi. Katika kambi yangu ya pale Chambani kuna kiongozi wa zamani sana aliyeiasisi ile kambi anaitwa Ndugu Ali Omar. Si vibaya Mhe. Waziri katika kuviboresha vikosi hivi wale waasisi wa kambi za JKU, KMKM, Magereza kuziangalia na kuzipa majina ya wale ambao wamekuwa waasisi ili na wao wajisikie kwamba kambi zao zina thamani kubwa kwa kuthaminiwa wale viongozi ambao wameziasisi kambi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 57 Tawala za Mikoa. Mhe. Naibu Spika, Serikali za Mikoa kuna Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hapa amesema kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Mkoa wa Kusini Pemba umepanga kutekeleza malengo yafuatayo. Lakini katika malengo haya kuna nukta namba mbili anasema “Kukamilisha ujenzi wa jengo dogo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ujenzi wa uzio wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani. Lakini sijaona kwamba kuna ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri afahamu kwamba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake iko katika hali mbaya sana inaning’inia. Kwa

hivyo, katika maelezo yake ya kufanya tathmini labda atueleze kwamba ana mipango gani madhubuti katika kuwajengea jengo madhubuti watu wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake ili na wao wajisikie kwamba wako katika ofisi ambayo inafanyika kazi.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti ya Kamati ya Kushughulikia Viongozi Wakuu wa Kitaifa walieleza hapa kwamba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake iko katika hali mbaya sana. Lakini katika utekelezaji wa mwaka huu 2011/2012 Mhe. Waziri hakueleza kwamba ofisi hii itajengwa au ofisi hii anaihamisha pale na kuiweka mahala ambapo ni madhubuti.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nizungumzie Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli halmashauri hii imeweka mambo mbali mbali ambayo wanatarajia kuyatekeleza katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Lakini nataka nimuombe Mhe. Waziri watu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani katika jimbo langu la Chambani kuna sehemu maarufu inaitwa Giningi. Sehemu ile inachotwa mchanga kwa wingi sana na kuna magari makubwa makubwa ambayo yanapita katika barabara ya Chambani kuelekea huko Giningi. Barabara ya kutoka Kwa Mtora kuelekea kwenye mashimo ya mchanga imechafuka sana na sababu kubwa ni magari mazito ambayo yanaingia kule.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aishauri Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani hawa wawekewe sheria maalum ya kuingia na kutoka na *cargo* zile kwa madhumuni ya kuifanyia ukarabati katika maeneo yale mazito ili wananchi wapate kupita na gari zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kuachiwa magari haya kupita bila ya udhibiti kwa kweli ni kuwarudisha nyuma wananchi wa eneo hili kwa sababu hata gari ya ng'ombe hivi sasa haipiti kwa vizuri kwa mujibu wa mashimo makubwa ambayo yamechimbika kwa sababu ya magari haya mazito yanayoingia na kubeba mchanga.

Mhe. Naibu Spika, naiunga mkono hotuba hii mia fil mia na nakushukuru kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika Ofisi ya Usajili wa Kadi za Utambulisho. Mhe. Naibu Spika, ofisi hii iko kwa mujibu wa sheria nambari 7 ya mwaka 2005.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kufanya kazi zake nzuri katika ofisi hii, lakini bado kuna usumbufu wa kutosha kwa wananchi wetu kutopatiwa kadi hizo za utambulisho ambapo ni jambo muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika uchaguzi uliopita kulikuwa kuna usumbufu wa kutosha na wengi walikosa kupiga kura kwa kukosa kadi za utambulisho wa Mzanzibari Mkaazi. Kuhusu Mkoa wa Kaskazini Wilaya ya Wete, kuna watu waliotangaziwa kufika katika ofisi ya kilimo Uweni ambao walipiga kura mwaka 2005 waoneshe vitambulisho vyao na watu hawa walikwenda ili wapate maelekezo na kupatiwa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Lakini kwa bahati mbaya mpaka kupita kwa uchaguzi wa mwaka 2010 hawajapatiwa kadi hizo na hawakuweza kupiga kura, huo ni usumbufu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na jitihada zote zinazofanyika kusajili kadi hizo mpya, walijitahidi kusajili kadi 6102 lakini bado usumbufu upo. Tunamuomba Mhe. Waziri jambo hili alifanyie kazi, kwa sababu kule tuna kero za Muungano na isijekuwa na kero za vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, kwa sababu ni haki ya kila Mzanzibari kupata hiyo kadi ya Mzanzibari Mkaazi kwa mujibu wa sheria. Lakini kwa utashi tu watu wengine hukoseshwa haki zao kwa makusudi bila kuzingatia kuwa ni jambo muhimu kwa Wazanzibari. Hivi sasa ukitaka kwenda kusajili tu simu yako ni lazima uwe na kitambulisho na kama huna basi unakosa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nije kwenye Idara ya Uratibu Utawala za Mikoa na Serikali za Mitaaa. Mhe. Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ya kuweza kutoa semina kwa madiwani na masheha ambapo masheha 332 na madiwani 141, lakini bado elimu hiyo ya kutoa semina inahitajika sana hasa kwa masheha. Kwa sababu masheha nao wamekuwa ni kero, hawa ni watumishi wa wananchi na waliokuwa karibu na wananchi, lakini kuna utata mkubwa sana katika kufanya kazi zao wanaleta ubaguzi, jambo ambalo hapa tulipofikia halihitajiki tena.

Kwa sasa hivi tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tunafanyakazi kwa pamoja bila kujali itikadi zetu za kisiasa, bado huku kuna masheha wengine wana ukiritimba. Tunaomba Mhe. Waziri na suala hili alichukuwe na atupe maelezo, kwa sababu masheha hawa sifa yao kubwa ni kuwa wawe wanapendwa na wananchi wao, lakini sifikirii kama ni masheha wengi ambao wanapendwa na wananchi wao katika shehia zao, kutokana na kazi zao wanazozifanya kukosa uwadilifu wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nikiwa hapo hapo kwa madiwani. Madiwani ni wanasiasa kama alivyo mwakilishi na mbunge nao ni wana siasa vile vile. Serikali inatumia matumizi makubwa katika uchaguzi mkuu uliofanyika wakiwemo madiwani, lakini kwa bahati mbaya hawa hawana mshahara wanaolipwa, lakini masheha wanalipwa. Imefika wakati kuwaangalia kwa jicho la huruma ili na wao angalau inapifika mwisho wa mwezi na wao wapate kujikimu katika shughuli zao za kikazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nazungumza hapa leo nikiwa ni mwakilishi, lakini mwaka 1995 nilikuwa diwani. Nilikuwa nikienda katika kikao cha Halmashauri ya Wilaya tunakutanika madiwani pale, nikiwaaga watoto wangu kuwa leo mtakula nyama, posho langu lilikuwa ni Shs. 1,500/= pamoja na nauli yangu ya kutoka Madenjani kwenda Bahanasa pale. Mhe. Naibu Spika, ni tatizo hili.

Mhe. Naibu Spika, halmashauri zetu za Zanzibar ni tofauti na halmashauri za Tanzania Bara wana vianzo vingi vya pesa, lakini sisi ni vichache kabisa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri umefika wakati madiwani tuwaangalie kwa jicho la huruma angalau kuweza kupata pesa kidogo na kuweza kujikimu.

Nikitoka hapo Mhe. Naibu Spika, nije katika Baraza la Manispaa. Kwa kweli ukiangalia Baraza la Manispaa wanafanyakazi zao, lakini bado haijafikia mafanikio kama yanayotakiwa katika huu mji wetu wa Zanzibar. Ukiangalia katika soko la Malindi kwenye sehemu ya mnada wa samaki, kule kuna uoza wa kutosha na samaki ni chakula kama chakula chengine, pia samaki wananadiwa katika sehemu ambazo sio nzuri. Waigeni wenzetu wa Tanzania Bara katika soko la samaki Feri, pale wana meza za kunadia samaki na samaki wanawekwa katika maeneo mazuri kwa sababu ni chakula. Sehemu zile Malindi kuna uchafu mwingi sana, ukimweka samaki basi anaweza kupata maradhi ambayo yanaweza kumdhuru mwanadamu.

Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri na hilo ulichukuwe ili ulifanyie kazi. Vile vile katika mji wetu wa Zanzibar umejaa uchafu na sisi tunaringia sekta ya utalii na watalii wanapotoka kwao wanataka wakiingia Zanzibar zile sifa tunazozitoa basi ziwepo. Lakini hapa tunasema Zanzibar ni njema atakaye aje, lakini wakija hapa watalii au watu wengine basi wakiikuta Zanzibar jinsi ilivyooza inatisha. Kwa sababu pahala popote panapokuwa hata ikiwa umekunywa maji ndani ya chupa ukishayamaliza, basi ukitaka kuitupa ile chupa kama pahala pale pako safi huwezi kuitupa sehemu hiyo. Lakini ukikuta pahala panatupwa takataka basi na wewe utaitupa hapo hapo.

Mhe. Naibu Spika, huu ni mfano uliokuwa hai, lakini katika sehemu zetu za mji ni mbaya sana na tunaringia mji wetu wa Zanzibar. Hata Mhe. Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein alipotembelea katika mji wa Zanzibar aliukuta

kimazingira uko katika hali mbaya. Hata wanyama wetu tunashindwa kuwadhibiti, wakifika barabarani badala ya kupishana gari, baskeli na binadamu wa kawaida basi unapishana na ng'ombe, wengine wamefanya kikao chao ni katika barabara hasa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri liangalie jambo hili lina uzito wa kutosha, tunataka mji wetu uwe mzito ili tupate ile dhana ya kuwa Zanzibar ni njema atakaye aje, wageni wakija wakute mazingira ni mazuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mwisho nakwenda katika Halmashauri ya Wilaya ya Wete. Halmashauri ya Wilaya ya Wete, napenda nichukuwe nafasi hii kuwapongeza kwa makusanyo mazuri waliyoyafanya kutokana na makadirio waliyokuwa nayo, wameyapitia kiasi. Wamekusanya mapato na kufikia asilimia 104, tuwapongeze sana Halmashauri ya Wete. Baada ya kuwapongeza, naomba wasijisahau. Katika shughuli za kuleta maendeleo katika sehemu zao basi kuwe na usimamizi bora kwa sababu pesa zinapotea ovyo ovyo za wananchi ambao ni walipa kodi wetu. Tunaomba wawe na usimamizi mzuri wanapopeleka pesa za shughuli za maendeleo. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii adhimu ambayo ningependa nichangie kidogo hotuba ya Mhe. Waziri kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Kwanza ningependa kumshukuru Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imechambua na tumeielewa pia tungependa kuichangia ili tuweze kusaidiana na serikali. Mhe. Naibu Spika, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, napenda nichangie kwenye baadhi ya vifungu ambavyo nahisi labda kwa upande wangu wa afya nikimsaidia waziri itaweza na sisi kutusaidia kama nchi. Jana palizungumzwa sana kuhusu manispaa. Jamanai 'mbaya halisi na wema hakosi'. Manispaa kweli ina matatizo, lakini ina mazuri mengi yamefanyika na tumeyasikia. Kama wangekuwa hawasikii basi sasa hivi mjini tusingewakuta vijana mabarabarani wanasafisha na ng'ombe tungekuwa tunapishana nao. Hilo tatizo sasa halipo la ng'ombe barabarani na vijana wanajitahidi kusafisha.

Lakini Mhe. Naibu Spika, tukizungumzia suala la manispaa tunazungumzia suala ambalo Mnazi Mmoja Hospitali nayo ipo, hiyo nayo ni sehemu ya manispaa. Tunazungumzia kuhusu uchafu. Jamani wananchi wa Zanzibar sasa hivi tumepoteza mwelekeo, hatujui usafi nini na uchafu nini. Hospitali ya

Mnazi Mmoja ina masaa ya kuingia na kutoka yamewekwa, lakini pale hata tukifanya nini uchafu wa hospitali ile hauishi na ni sehemu ya manispaa, hauishi kwa sababu gani.

Hatujui wakati wa kuingia hospitali wala kutoka. Hospitali imekuwa kama forodhani, watu saa zote wametandika mabuthati wamekaa, watu wanaingia bila mpangilio wakizuiliwa wakali. Wakifika pale wanakaa na ma-chipsi wanakula. Mimi huwa najiuliza hivi kweli hawa wamejia wagonjwa. Kweli una mgonjwa wako yuko taaban ICU, utakaa pale utandike ma-chipsi mnakula, zogo moja kwa moja pakupita hapana. Wamechukua nafasi zote za wagonjwa, pale wanatakiwa kukaa *X-Ray* wamekaa wao mabarazani, wakitaka wagonjwa wakae hawawapishi ukiwaambia wakali. Jamani hospitali ni hospitali tupeni nafasi tusafishe mara moja, ibaki safi na tuje kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, wakati huo huo sio hospitali tu pamoja na wananchi, saa nyengine tunawalaumu manispaa kwamba wanalipwa shilingi 6,000/= lakini hawafyagii na kukusanya taka. Mimi nafikiri kazi ya manispaa ni kukusanya taka zilizokwisha kuwekwa pahala wakenda kuzipeleka kwenye madampo. Sio kwenda kufyagia majumbani ambapo sisi wenyewe hatufyagii, kweli hata manispaa itufyagilie majumbani. Utakuta mtu nje ya nyumba yake taka anazikiuka anaingia ndani mwake, sasa tumezidi. Manispaa wacheni wafanye kinachowahusu na wananchi tuchukuwe jukumu letu, tusafishe nyumba zetu, tusafishe mji wetu, tusafishe shehia zetu na manispaa wakusanye taka wapeleke kunakohusika. Tusiwatwike mzigo sio wao halafu tukawalaumu.

Mhe. Naibu Spika, utakuta mtu anakuja hospitali anatema mate pale, unamwambia wewe mbona unatema mate, atakuambia, si mnalipwa. Kweli tunalipwa tukapanguse mate ya watu wanaopita wakitema, hawajui kama mate ni uchafu. Hata kama kweli wanalipwa, lakini jamani na wafanyakazi wa hospitali waoneeni huruma.

Mhe. Naibu Spika, sehemu ya pili iliyozungumzwa hapa ni ya vyoo, hasa magereza. Mimi napenda nimshauri waziri kuwa kama kweli vyoo magereza hakuna, mimi huko sijawahi kwenda, lakini nafikiri kama tunaelimisha wale wanafunzi, moja katika tunachotakiwa kuwaelimisha ni usafi wa mazingira wa kutumia vyoo, Wizara ya Afya tunahimiza hilo. Kwa hivyo, naomba awaambie watu wa magereza wajenge vyoo, hilo litawapunguzia maradhi ya mripuko. Yakitokea maradhi ya mripuko katika mkusanyiko wa watu kwenye sehemu kama zile basi inakuwa ni ngumu kuyashughulikia.

Vile vile tutapunguza pia hilo la ukimwi, kwa sababu matamanio yanatokea wakati binadamu wanapokua wanaishi katika utaratibu kama huu na kwa kuwa

tunaambiwa ukimwi magereza upo. Kwa hivyo, nafikiri njia moja ya kuupunguza ukimwi ni kuwajengea vyoo magereza, ili watu wakatumia vyoo.

Mhe. Naibu Spika, tukizungumzia vyoo sio magereza tu, naomba halmashauri zote pamoja na mabaraza tuliyonayo, wahakikishe majumba yote yana vyoo, hiyo ni lazima ni sheria ipo. Kwa hivyo, wananchi kujenga nyumba zenye vyoo na makaro pia ya maji, sio kutiririsha tu maji katika vichochoro ule sio utaratibu, kwa hivyo tuone ni jinsi gani hilo linafanyiwa kazi. Tunaomba Mhe. Waziri watusaidie watu wa manispaa na halmashauri ili kuhakikisha kwamba nyumba zote zina vyoo, itatupunguzia maradhi mengi tu.

Pia ningependa nimsaidie Mhe. Waziri kumwambia kwamba labda hawa watu walioko kwenye magereza nao wanahitaji elimu, nafikiri ni haki yao. Wangekuwa na angalau sehemu au chumba ambacho watakuwa wanafika pale na kuweza kusikiliza hotuba za viongozi ili wakajua ni matumaini gani yalioko nje ya viongozi wao, wakatamani kurudi huku kuliko kukaa kwenye magereza, wakapata nafasi ya kuelimishwa ukimwi ni nini, wakapata nafasi yakuelimishwa madawa ya kulevya ni nini, hiyo ingewasaidia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama kutakuwa na uwezekano tulifanye hilo kama hali ya fedha itaruhusu.

Kuhusu elimu. Mhe. Naibu Spika, napenda niwahakikishie vikosi, kwamba katika Chuo cha Afya Mbweni kuna nafasi zao, wazitumie hizo kuleta wanafunzi wao kule. Lakini watuletee wanafunzi wanaostahiki katika vyuo vyetu ili tuweze kuwatolea wafanyakazi bora. Tunatoa matangazo, lakini wanachelewa kuwaleta, halafu wakiwaleta wanatukuta tumeshamaliza kazi, kwa kweli inakuwa inatusumbua, kuwaacha tunashindwa na kuwapokea inakuwa ni tatizo.

Mwisho. Mhe. Naibu Spika, jana nimesikia habari ya migogoro nyingi, sijui Mtende na kwengineko. Lakini mgogoro mmoja unazungumzwa siku nyingi tu hapa wa Mchangamle Muyuni, huo sikuusikia nalo ni tatizo Mhe. Waziri. Mwambie Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Mchangamle aishughulikie sivyo watu watauwana. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ndogo na mimi nikapata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, mengi yamekwisha kuzungumzwa tokea jana, kwa hivyo kilichobakia sisi ni kukazia tu ili kuona mambo haya yanakwenda vizuri. Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri Dk. Mwinyihaji Makame, kwa hotuba yake hii nzuri, ameiandaa vizuri na kitabu

kizuri pamoja na wasaidizi wake wote, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wote kwa kuandaa bajeti hii nzuri.

Pia nitumie nafasi hii adhimu kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein, kwa jitihada zake za kuona kwamba nchi yetu inakwenda katika hatua za maendeleo. Juhudi zake tunaziona na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atampa nguvu ili aweze kusimamia yale yote ambayo ameyazungumza na wananchi wana matarajio makubwa sana kutokana na hotuba zake.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka nije katika Idara hii ya Mipango Sera na Utafiti, ikishirikiana na hii Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa. Mhe. Naibu Spika, ni mara nyingi tokea Baraza lililopita hadi Baraza hili tumekuwa tukipata taarifa juu ya suala zima la marekebisho ya serikali za mitaa.

Kwa kweli jambo hili linahitaji lifanyiwe kazi ipasavyo katika kipindi hiki na *Inshaallah* liweze kumalizika. Sera ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na sheria nambari 3 na sheria nambari 4 na ile sheria nyengine, ili ziweze kufanyiwa marekebisho. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, sheria hizi ni za muda mrefu na zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziendane na wakati. Jambo hili tumekuwa tukilizungumza kila wakati na kila mara, lakini naamini katika kipindi hiki linaweza likafanyiwa kazi sheria hiyo na sera hiyo ikaweza kupatikana hapa katika Baraza lako tukufu ili iweze kufanyiwa kazi.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nije katika maeneo ya mikoa, wilaya halikadhalika na majimbo. Kwanza nichukuwe nafasi hii kuzipongeza serikali za mikoa na serikali za wilaya na halikadhalika na halimashauri za wilaya, Baraza la Manispaa pamoja na masheha wetu. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wamekuwa wakifanya kazi vizuri, kwa bidii kubwa na jitihada zao zinaonekana. Kilio hiki cha majengo katika ofisi zetu za mikoa na wilaya zinahitaji kupewa msukumo, Mhe. Waziri nikuombe ulisimamie sana hili, ili kuona afisi hizi za viongozi wetu wakuu hawa wa mikoa basi zinapatiwa fedha za kutosha ili na wao waweze kukaa katika majengo mazuri na yenye hadhi.

Mhe. Naibu Spika, tunapowatembelea wenzetu wa Tanzania Bara, afisi zao za mkoa na wilaya kwa kweli zinapendeza na zina hadhi ukilinganisha na hizi zetu za hapa ambazo Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezilalamikia. Kwa hivyo, naomba suala hili nalo serikali ilipe kipaumbele jambo hili.

Jengine ambalo ningeziomba serikali za mikoa na wilaya, zina wajibu wa kusaidia katika utunzaji wa mazingira. Suala hili Mhe. Naibu Spika, nililizungumza juzi wakati nikichangia hotuba ya Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais juu ya suala la mashirikiano ya pamoja kati ya serikali za mkoa na

wilaya na halmashauri za wilaya pamoja na masheha wote. Suala la uhifadhi wa mazingira ni muhimu sana na kwa sababu tunapozungumzia mazingira ni eneo lote la Zanzibar, sasa hivi kumekuwa na uchimbaji wa mchanga kiholela, kumekuwa na ukataji wa miti kiholela, kumekuwa na uchafuzi wa mazingira katika vianzio vya maji katika maeneo ya mwanyanya na maeneo mengine.

Mhe. Naibu Spika, suala hili linahitaji ushirikiano wa pamoja, serikali za mikoa, wilaya na halmashauri washirikiane na idara hii hii inayohusika na usimamizi wa mazingira, ili kuona mambo haya yanakwisha. Bila ya mashirikiano ya pamoja na wenzetu hawa wa mikoa na wilaya, basi hali yetu itakuwa sio nzuri na jambo hili haliwezi kufanikiwa. Kwa hivyo, niziombe serikali za mikoa na wilaya ili kuona na wao wanachukua nafasi zao kupiga vita huu uchafuzi wa mazingira na hasa katika maeneo ya vianzio vya maji pamoja na uchukuaji wa mchanga.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye Baraza la Mji pamoja na Halmashauri za Wilaya. Kwa kweli wenzetu hawa wa Baraza la Manispaa wanajitahidi katika kuweka mji wetu katika hali ya usafi. Nitumie nafasi hii kuwapongeza kwa juhudi zao hizi wanazochukua. Mji wetu pamoja na kwamba hali yake sio nzuri kabisa, lakini wanajitahidi kutokana na hali halisi ilivyo. Vitendea kazi havitoshi, hawana magari ya kutosha na vifaa vyengine, lakini juhudi wanaichukua na kwa kupitia mradi huu wa ZUSP, mimi naamini kwamba mji wetu huu utarudia katika hali yake ya usafi.

Mhe. Naibu Spika, tunawaomba wenzetu hawa wajitahidi na kwa sababu Baraza la Manispaa ndio kioo, wageni wote wanaoingia Zanzibar basi wanaanzia hapa katika mji wetu wa Zanzibar. Kwa hivyo, wanapoteremka bandarini au uwanja wa ndege basi twabaan waone mji wetu uko katika hali ya usafi, hasa katika maeneo ya Mji Mkogwe nadhani yanahitaji kusafishwa vichochoroni, wachukuwe juhudi ya kusafisha na watumie muda wa masaa 24, kama mjumbe mwenzangu mmoja alizungumza hapa kwamba wagawane, wengine wasafishe mchana na wengine wasafishe usiku. Tutakapojipanga vizuri basi hali ya mji wetu itakuwa safi na wa kuridhisha.

Jengine Mhe. Naibu Spika, ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu pale jua kali kwenye makontena. Tulisikia matangazo ya redio ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini kwamba suala la makontena limeruhusiwa mpaka hapo mahakama itakapotoa uwamuzi. Lakini tulipata taarifa kwamba wafanyabiashara wale wa Juakali wanaozunguka katika maeneo yale ya makontena wale ni marufuku kufanya biashara pale, pamoja na kwamba ni maeneo yao ambayo wanapata riziki zao.

Mhe. Naibu Spika, eneo lile halipendezi kuona watu wamezagaa wameenea katika barabara. Wanafunzi wetu wanaosoma katika skuli za pale Vikokotoni wanapata tabu sana, kwa kweli jambo hili linahitaji kuangaliwa kwa makini ni lazima mji wetu uwe na utaratibu. Hatuwezi tukawaachia watu wakafanya biashara tu ovyo ovyo kila pahala, hakuna hata njia ya kupita. Kwa hivyo, Baraza la Manispaa, Serikali za Mikoa na Wilaya zina wajibu wa kuhakikisha kwamba wale wafanyabiashara wanaozagaa katika maeneo yale wanaondoshwa na wanakwenda katika maeneo mengine, yabakie makontena peke yake kama taarifa zilivyokuja. Watoto wetu wanaosoma katika skuli zile wanasoma kwa tabu sana, wanapata shida hasa wakati wa rises. Kwa hivyo, ni lazima mji wetu uwe na utaratibu. Mhe. Waziri nikuombe sana ulisimamie sana ili tuone kuwa tunakuwa na utaratibu katika kufanya shughuli zetu.

Jengine ambalo ningependa kuzungumzia katika maeneo haya ya Halmashauri za Wilaya pamoja na mabaraza ya miji juu ya masuala mazima ya shughuli za utendaji. Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kwa madiwani wetu kuhusu nafasi hizi zinavyotumika. Kwa mujibu wa taratibu zetu na kwa mujibu wa sheria zetu, watendaji makatibu wa halmashauri, wakurugenzi wa manispaa pamoja na mabaraza ya mji, hawa wanatakiwa wawajibike kwa madiwani wao. Hii ndio sheria inavyosema. Lakini kinachoonekana ni kwamba sasa hivi wamekuwa wao wanafanya mambo bila ya kupata idhini kwenye mabaraza yao. Kweli hiki ni kinyume na sheria.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri nikuombe sana jambo hili ulisimamie na uwafahamishe sana makatibu wetu kwamba wao wanatakiwa wawajibike kwenye mabaraza yao, wao ni watendaji katika taasisi zao, lakini watatenda yale maazimio ambayo tayari yameshapitishwa kwenye mabaraza yao, na watakapofanya hili maana yake wataondosha manung'uniko miongoni mwa madiwani na shughuli zao zitakwenda vizuri. Lakini zile shughuli wanazozifanya kama zitakuwa hazipitii katika maeneo ambayo yanahusika basi zitaharibika na zitakuwa mbaya.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda wako ni mdogo. Mimi naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja na niwatakie kila la kheri, ahsate.

Mhe. Mlinde Mbarouk Juma: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa siku hii ya leo na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku ya leo kukutana hapa tukiwa na hali ya uzima na salama na *Inshaallah* ataturejesha salama.

Mhe. Naibu Spika, napenda niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Bumbwini kwa kuweza kunifikisha hapa na mimi nawaahidi kwamba sitowaangusha. Napenda nichangie katika hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa kuzungumzia Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B. naipongeza sana halmashauri hii kwa kuweza kupita yale malengo ambayo wamejipangia ya kukusanya mapato.

Mhe. Naibu Spika, niwaombe katika ukusanyaji huo wa mapato wawe waangalifu hasa tukizingatia Wilaya yetu ya Kaskazini 'B' ni mashimo tu ya kuchotea mchanga na hii inapelekea hatari ya kukosa wananchi maeneo ya kulima hata kujenga makaazi yao ya kudumu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye ukurasa wa 82 ambapo kuna Chuo cha Mafunzo. Kwa kweli Chuo cha Mfunzo hapa wamejipangia kwanza kupima maeneo yao ya mashamba kama vile Kinumoshi pamoja na sehemu nyengine.

Kwa hivyo, naomba kutoa msisitizo tu kwamba jitihada hiyo wafanye kwa maeneo yote na wala isiwe kwa haya maeneo mawili tu ambayo wameyaainisha, kwani maeneo mengi hayana Hati Miliki na kupelekea uvamizi wa maeneo ya serikali na kuchukuliwa. Hivyo, basi niwaombe na yale maeneo mengine yaliyobakia wafanye hivyo. Mhe. Naibu Spika, nina wasi wasi hata hapa Makao Makuu sijui hiyo Hati Miliki kama ipo.

Mhe. Naibu Spika, nimeangalia bajeti ya Chuo cha Mafunzo na nimeiona. Kwa mfano, mwaka uliopita waliidhinishiwa shilingi elfu tatu, mia saba, sabini na sita milioni na kwa mwaka huu wa fedha wameidhinishiwa jumla ya shilingi 3,938 milioni. Kwa kweli hizi fedha zimeongezeka kidogo lakini sio kwa asilimia kubwa sana, kwa sababu kama kwenye vifungu vyengine vya matibabu na sehemu ya mafuta. Kwa mfano, kwenye matibabu walitengewa shilingi milioni kama 9 kipindi kilichopita na mwaka huu zimepungua.

Sasa hapa sijui kigezo gani ambacho kimetumika kwa ajili ya kuwapunguzia kwenye matibabu na pia kwenye masuala ya matufa. Mhe. Naibu Spika, mafuta kikosi hiki ni jamii, yaani kama ni sehemu ya familia, kwa sababu wanawaweka wanafunzi tena wanakaa kwa muda ambao ni mrefu mpaka wanamaliza kesi zao.

Kwa mfano, kila wiki utawaona wanakwenda kukata kuni kama vile Chaani pamoja na sehemu nyengine na tukadirie kwa wiki wanakwenda siku moja labda watumie lita 15 tu. Sasa kwa kipindi cha mwaka na bajeti hii ya mafuta inavyoonesha watatumia kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwamba bajeti hii tuiangalie vizuri, inaonekana kwamba bajeti ni nzuri, lakini haitoshelezi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mwanzo kabisa ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subuhanahu Wataala*, aliyetuwezesha kuwa wazima katika Baraza letu jipya hili linalopendeza lenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitafa. Kwa kweli ni neema kubwa ambayo ametujaalia Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu sina budi kumshukuru Rais aliyemaliza muda wake Dkt. Amani Abeid Karume kwa kazi nzito kubwa, tena ya kishujaa aliyoifanyia nchi hii na historia ndefu ametuwekea na wala hatuwezi kusahau. *(Makofi)*

Vile vile nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ahadi alizokuwa akitoa, pindipo Mwenyezi Mungu akimuwezesha kuwa Rais ataunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa na tayari tunaona kitu hiki. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, shukurani nyengine ziende kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad kwa utulivu, umakini wake pamoja na hali tuliyofikia muda huu. *(Makofi)*

Pia nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa uchakazi wake mahiri na kutokana na umri wake basi tunauona utendaji wake. Kwa hivyo, ninamtakia kazi njema pamoja na afya njema. *(Makofi)*

Pamoja na hayo, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwa na wizara mbili kwa pamoja na kuziongoza. Kwa kweli Mhe. Waziri ni mchapakazi mahiri bila ya kumpendelea na tumeyaona aliyoyafanya na wala tusimuhukumu kwa mabaya na mazuri tuyatizame aliyoyafanya Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwanafunzi ukimpa kazi nyingi basi mwisho anakuwa si hodari tena kutokana na majukumu unayompa. Kwa hivyo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nasaha zangu kwako kwamba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tumpachika mizigo miwili kwa pamoja. Vile vile Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pia naye tumempachika majukumu makubwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tunao Mawaziri watatu ambao hawana wizara maalum. Kwa hivyo, nasaha zangu tungewapunguzia majukumu mawaziri hawa wenye mizigo mizito na huo ni ushauri tu, kwa sababu mawaziri wanachukua mshahara wa ule wa waziri na wizara zipo. *(Makofi)*

Hivyo, nadhani ni vyema tukawapunguzia majukumu baada ya kufanya majukumu yote kumtikwa mtu mzigo mmoja na mwisho wake hatutegemei kuwa mazuri yatakuwa mabaya. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais huo ni ushauri kutoka kwangu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nitoe nasaha zangu kuhusu Chuo cha Mafunzo. Kwa kweli hali hairidhishi ndani mule kwa binadamu na afya yake, yaani hali ni mbaya na mwisho wake unaweza kulia kutokana na hali ya mule ndani na wala hatuwezi kuyazungumza hapa mengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia utendaji wa wafanyakazi wa Baraza la Manispaa kidogo ni mtihani na huo ni ukweli usiofichika, yaani wakati wanapokamata bidhaa za watu basi unakuwa ni mtihani. Kwa mfano, mimi mwenyewe kwa kushuhudia Bandarini Malindi kuna mtu anauza mchuzi wa pweza, basi mchuzi ule walianza kuunywa pale kabla ya kufika Ofisi ya Baraza la Manispaa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, utendaji ule kuna haja ya kurekebishwa, kwa sababu wanachukua vitu vya watu na wala sijui vinafika pahala gani. Kutokana na hali hiyo, nadhani kuna haja ya kurekebishwa mpaka Sheria za Mahakama yao, kwa sababu sheria yao sijui wanatumia kifungu gani. Kwa mfano, kuna Mhe. Mjumbe mmoja ambaye alizungumza jana hapa mtu kwenda kujisaidia amechezea mwezi mmoja au miwili, kwa kweli ni mtihani usiofichika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nadhani niishie hapa na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nikushukuru sana kwa kupata wasaa huu mwengine wa kuja kufanya majumuisho ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe, katika hotuba yangu hii ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi niliyoisoma hapo juzi.

Mhe. Naibu Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia hotuba hii hapa ukumbini. Kwa upande wa wale waliokosa nafasi tu na walitaka kuchangia, ukweli utajidhihirisha wakati nitakaposoma orodha, yaani nimepata Waheshimiwa Wajumbe 10 walichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sote tumeshuhudia kwamba hii ni wizara kubwa tena ina mambo mengi ambayo ni muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. Kwa hivyo, sisi kama wizara niseme nichango yotu tumeigawa sehemu tatu.

Kwanza tumepata maoni, maelekezo, ushauri wenu juu ya kufanya wizara ifanyekazi zaidi na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kusema tumeboresha, basi tufanye wizara utendaji wake uwe bora zaidi.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana, kwa sababu unapofanyakazi ndipo unapoyaona matatizo, unapoambiwa na watu pamoja na viongozi wenzio basi lazima usikilize. Hivyo, Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba Waheshimiwa Wajumbe mlivyotuasa, mlivyotuelekeza, mlivyotukosoa, basi tunakubali na hayo ni mambo ya msingi kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ninachokuombeni ni kwamba nitajitahidi sana kufanya majumuisho takribani yote lakini si rahisi, kwa sababu nimesoma *speech* ile kwa masaa mawili na kidogo. Sasa nikichukua mmoja mmoja na Waheshimiwa Wajumbe waliochangia hapa ukumbini ni 29 na wale waliochangia kwa maandishi ni 10 na jumla ni 39. Kwa hivyo, nikiwachukua mmoja mmoja nafikiri mtaniba masaa matatu mengine na sauti nafikiri itakwama njiani.

Mhe. Naibu Spika, nitajitahidi kuzungumza kwanza *issues* kubwa ambazo zilizozungumzwa na takriban wengi sana mtaona mambo yalivyojirudia na wengine kama wamekuja kuzidisha, yaani kuyajadili yale mambo. Kwa kweli ni mambo ya msingi na asiyekubali kukosolewa basi huyo ni mtendaji. Sasa sisi kwa roho safi kabisa tunakubali kuelekezwa, kukosolewa pamoja na miongozo mliyotupa na ninaahidi Mhe. Naibu Spika, tutayafanyiakazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, masuala mengine tayari Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameshayatolea kauli kwamba hili tuachiane na tunalifanyiakazi. Kwa hivyo, na mimi hapa nitazidi kusema hapa tunafanyiakazi vipi. *(Makofi)*

Lakini ninachowaomba Waheshimiwa Wajumbe mtuamini kama mnavyozidi kutuamini, kwa sababu bado tupo Barazani isiwe kwamba ninafanya majumuisho leo na kesho ninakimbia wakati tumo humu basi mtakuja kunikamata Waziri na *Alhamdulillah* kila siku najibu maswali, je waziri vipi mbona kimya. Kwa maana hiyo, nimeona nitoe utangulizi huo kwa dakika chache. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima zote naomba niwatambue hoja yangu hii. Kwa hivyo, kama nilivyosema Waheshimiwa Wajumbe waliochangia ni 39,

ambapo 29 wamepata nafasi hapa ukumbi na 10 wamepata nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

1. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa);
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk;
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
4. Mhe. Asha Bakari Makame;
5. Mhe. Panya Ali Abdalla;
6. Mhe. Mohammed Haji Khalid;
7. Mhe. Asaa Othman Hamad;
8. Mhe. Ismail Jussa Ladhu;
9. Mhe. Viwe Khamis Abdalla;
10. Mhe. Abdalla Moh'd Ali;
11. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa;
12. Mhe. Salim Abdalla Hamad;
13. Mhe. Abdi Mosi Kombo;
14. Mhe. Subeit Khamis Faki;
15. Mhe. Asha Abdu Haji;
16. Mhe. Mohammed Said Mohammed;
17. Mhe. Saleh Nassor Juma;
18. Mhe. Hija Hassan Hija;
19. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa;
20. Mhe. Farida Amour Mohammed;
21. Mhe. Mussa Ali Hassan;
22. Mhe. Bikame Yussuf Hamad;
23. Mhe. Ali Salum Haji;
24. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi;
25. Mhe. Hassan Hamad Omar;
26. Mhe. Naibu Waziri Afya;
27. Mhe. Salmin Awadh Salmin;
28. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma;
29. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe hawa wote wamechangia hapa ukumbi na ninawashukuru sana kwa michango yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, waliopata nafasi ya kuchangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Shawana Bukheit Hassan;
2. Mhe. Omar Ali Shehe;
3. Mhe. Fatma Mbarouk Said;

4. Mhe. Nassor Salim Ali;
5. Mhe. Mgeni Hassan Juma;
6. Mhe. Rufai Said Rufai;
7. Mhe. Salma Mussa Bilali;
8. Mhe. Ali Abdalla Ali;
9. Mhe. Wanu Hafidh Ameir na
10. Mhe. Salum Amour Mtondoo

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema nawashukuru sana kwa michango yao na ninaamini muda ulikuwa mfupi, lakini wangependa sana kuchangia hapa ukumbini. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na mambo 13 ambayo haya nilihisi makubwa na takriban Waheshimiwa Wajumbe wote wamechangia.

(i) Kwanza kabisa ambalo limezungumzwa karibu na kila Mhe. Mjumbe ni kuhusu Manispaa,
(ii) *GSO*,
(iii) Mishahara kwa Waheshimiwa Wadiwani wetu,
(iv) Utunzaji wa Masoko,
(v) Vitambulisho utaratibu urekebishwe,
(vi) Vikosi vyetu nakushukuruni sana mmevizungumza kwa upana mkubwa sana, kwamba mmetutolea sifa pale panapo stahiki sifa na mmetukosoa pale ambapo mnaona tufanye vizuri zaidi.

Kwa kweli tunawashukuruni sana na yote mliyotuambia kuhusu Zimamoto pamoja na mapungufu yake tumeyapokea. Vile vile sifa mlizotupa Kikosi cha KMKM na mapungufu yake tumeyachukua.

Lakini zaidi Chuo cha Mafunzo kuhusu mambo mliyotuambia kwenye majengo ya vyuo vyetu, kwamba lazima twende na wakati kwa sababu wale ni binadamu na mambo ya mtondoo yamepitwa na wakati. Mhe. Naibu Spika, kweli tumeyasikia na tayari tumeshaanza marekebisho kama nilivyozungumza. Kwa mfano, ukiende Hanyegwa Mchana, Ole na hata hapa Kilimani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tatizo ni ule mjengo wenyewe wa hivi vyuo kidogo unakazi, kwa hivyo tukihitaji kurekebisha pale basi tunahitaji fedha nyingi kwa ajili ya yale majengo, sasa tunakwenda kidogo kidogo.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana tumeamua kujenga gereza jipya, kwa sababu hapa mrundikano umekuwa mkubwa zaidi na kweli *concern* yenu ya kiafya. Mhe. Naibu Spika, juzi tu tulizungumza kwa ridhaa ya Mhe. Waziri wa Afya, pamoja na Naibu Waziri wa Afya pamoja na Kamishna wa Chuo cha Mafunzo, kwamba tutakapomaliza bajeti hii, basi tutaambatana na Timu ya Afya ambayo ni kabambe, kwa ajili ya kwenda Kilimani na kuangalia marekebisho gani ya afya kwa haraka tuyafanye. *(Makofi)*

Lengo yale mliotuambia kama vile ya maambikizi ya virusi vya UKIMWI pamoja na mengine yote tuweze kuyaepuka na wakati mwengine hata pumzi kidogo ni nzito. Sasa haya Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Chuo cha Mafunzo tumeyasikia. *(Makofi)*

Hali kadhalika kwenye JKU pamoja na Kikosi cha Valantia kama nilivyosema mambo haya yote mliotuambia tumeyasikia. *(Makofi)*

Vile vile Waheshimiwa Wajumbe wengi walichangia katika Mradi wetu wa *ZUSP*. Mhe. Naibu Spika, suala kubwa ambalo nisigenikasau Mhe. Isamil Jussa Ladhu alisema kwamba mbona kulikuwa na tofauti ya maelezo ya kitabu cha Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na maelezo yetu. Kwa kweli Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo yeye ndiye mwenye mradi, kwa sababu wao walitusaidia pamoja na kutuongoza na kuweza kuandika mradi na baadaye tukauuza mpaka tukapata fedha.

Kwa hivyo, *Project Implementation Unity* bado iko Wizara ya Fedha na yale aliyoyasema yeye ndio malengo ya mradi wote. Lakini yale tuliyoyasema sisi ni utekelezaji kwa mwaka huu kwa upande wetu na sisi ndio watekelezaji wakubwa. Kwa maana hiyo, tofauti iko hapo, kwa sababu sisi tumechambua zaidi kwenye utekelezaji na yeye amechambua zaidi kwa mradi mkubwa.

(vii) Uchafuzi wa Mazingira pamoja na Usafi wa Mji. Kwa kweli suala hili tumelikubali na tumelichukua na tumelisikia.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba kweli tumezidiwa na idadi ya watu wetu ni wengi na fursa zetu sio kwenye ufasi wa mji, lakini hata kwenye hospitali, skuli pamoja na sehemu nyengine tumezidiwa.

Kwa hivyo, inabidi lazima tukaze kamba, ili kuweza kwenda na hali ya wakati. Kwa mfano, taka zinazozalishwa hapa mjini kwa siku ni tani 216 za taka kila siku na uwezo wetu wa kusafisha ni tani 90 na *percent* 40 tu. Sasa tujiulize taka nyengine zinakwenda wapi?

Mhe. Naibu Spika, ndio maana baada ya kuona mapungufu hayo ni vyema tuandike mradi, basi tuliandika mradi na *Alhamdulillah* na fikiri niliwahi kusema kwamba jina la Zanzibar linapendeza, yaani nchi za nje ukitamka Zanzibar, basi kila mtu anasema *oh*! *Is a beautiful country*, wanaisifu nchi yetu. Lakini sisi tuliopo ndio tunaojua na wenzetu wanaisifu, kuna mambo tunaweza kuyafanya mambo yakawa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Hiivyo, ninachotaka kusema ni kwamba suala hili tunakubali. Lakini kama mtaona huu mradi maandiko yake na tulivyosoma kuna vitendeakazi vingi ambavyo tutanunua, kama vile magari ya kubebea taka *dusty ben* tutanunua. *(Makofi)*

Kwa kweli namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine kwamba lazima na sisi jamani tubadilike katika suala la uzoaji taka na usafi. Kwa hiyo, hawa baraza la Manispaa pamoja na Halmashauri wao wanatusaidia, lakini mtu kwenye mlango wake au anatupa mapakacha na mambo mengine, hivyo lazima ile nidhamu ya usafi iwepo, yaani tubadilike.

Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Naibu Spika kwamba tusaidiane, kwa sababu hili si la wizara peke yake na hili ni letu sote kwani sisi ndio wenye majimbo. Sasa kila majimbo yetu yakiwa safi basi ndio picha nzuri tutapata sote, hasa Waheshimiwa Wajumbe ambao tuko mjini. Kwa mfano, Mhe. Ismail Jussa Ladhu Jimbo lako la Mji Mkongwe na wewe ndio kioo cha mji wetu kwa watalii. *(Makofi)*

Hivyo, mimi niko tayari na timu yangu tutakuja kwa ajili ya kufanyakazi na Ofisi yako ya Jimbo, ili tuweze kufanikisha masuala ya ufasi. *(Makofi)*

(viii) Suala jengine kubwa ambalo limezungumzwa ni kuhusu Mahusiano ya Kikanda.

(ix) Vile vile kuhusu Makaazi ya Mhe. Rais, yaani tupate eneo jipya la ujenzi wa Makaazi yake, kwa sababu pale kapo barabarani mno na kiusalama si pazuri. Kwa hivyo, hilo tuumelisikia na tutalizungumza na kulitafakari kwa undani zaidi, ili tuone vipi tunaweza kufanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo niliyasema kuhusu usalama na mambo mengine. Kwa kweli juhudi tunazichukua kubwa sana kuona hata magari yanayopita pale hayasimami ovyo, yaani kuna tahadhari nyingi tunazichukua.

(x) Mhe. Naibu Spika, pia kuhusu Ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa. Hizi nazo zimezungumzwa kwa upana wake kama vile majengo mabovu, ofisi vichochoro na suala hili linahitaji kutizamwa kwa undani. *(Makofi)*

Kwa kweli si vyema na hivi sasa imezunguumzwa hapa kwamba Mhe. Mkuu wa Mkoa au Wilaya na Mhe. Salmin Awadh Salmin amezungumza hapa wanakwenda Bara wanaona wenzetu walivyo, yaani ni tofauti na sisi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli na tunaandika *project*, lakini bajeti yetu ni ndogo, inabidi twende kidogo kidogo.

Sasa angalau tunajaribu kufanya marekebisho kidogo na wakati anapokwenda mgeni, basi ionekane kweli amekwenda kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Wilaya. Kwa hivyo, hilo tumelisikia nalo na tutalitilia mkazo. *(Makofi)*

(xi) Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine ambalo Waheshimiwa Wajumbe wamelizungumza kwa uchungu kabisa na kutaka tuchukue hatua zinazofaa kuhusu upotevu wa fedha au kutolewa fedha bila ya stakabadhi. Kwa kweli hili nalo tumelisikia na tumeliona.

Lakini kubwa katika kufuatilia nimegundua kwamba tunalo tatizo la *Internal Auditors* ni wachache mno na wako wizarani tu na hili ni tatizo, kwa sababu tuna-*handle* fedha nyingi tena kwa kitita na inabidi kila *institution* yetu lazima iwe na *Internal Auditor*, kwa ajili ya kuangaliwa matumizi pamoja na mwenendo wa fedha. Mhe. Naibu Spika, naishukuru sana kamati ya *PAC* kwa kutueleza suala hili.

Sasa hili tumeliona na tutatizama vipi tutaweza kulirekebisha haraka iwezekanavyo kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ili tuone kuwa matumizi yetu yanaangaliwa pamoja na kuratibiwa vizuri sana, ili kuondosha ile mianya na wasi wasi wa matumizi.

(xii) Suala la mwisho ni kuhusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba marekebisho yako *slow*. Mhe. Naibu Spika, nakubali na hili tayari tumeshalisema, kwa sababu suala hili kidogo kwa Zanzibar ni jipya na nchi yetu ni ndogo na wala tusiige *model* nyengine ambazo haziko *applicable* kwetu.

Kwa hivyo, tunatizama wenzetu wamefanya vipi na sisi hapa kwetu turekebishe au twende vipi. Kwa maana hiyo, tutashikiriana na nyinyi pamoja na wataalamu wengine, ili tuone kuwa marekebisho haya yanafanywa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema suala hili liko kwenye mpango mzima wa marekebisho ya jumla, yaani *Code Reform* za nchi na imetokana yale mambo ya maslahi ya fedha au marupurupu yetu ya Waheshimiwa.

Kwa hivyo, namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tayari yameanza au kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora atakuja kueleza vizuri mipango ilivyo. Sasa hiyo, ni moja wapo ya marekebisho hayo.

Mhe. Naibu Spika, awamu ya pili ni hii ya Serikali za Mitaa. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba tuko *slow*, lakini nia yetu nzuri na twende taratibu na baadaye tuje na kitu ambacho kitakubalika.

Mhe. Naibu Spika, sasa hayo kwa mtazamo wetu hayo ndiyo yalikuwa mambo mazito, ambayo kila mmoja wetu takriban aliyazungumza. Kwa hivyo, niliona ni vyema nichukue dakika chache kidogo kuyazungumza na niseme kwamba kwa bahati mbaya Mhe. Mjumbe ambaye sikumtaja basi naomba radhi na wala sio lengo langu, kwa kweli wote ningependa niwataje lakini haikumkinika, hivyo niseme wote maoni yenu tumeyapokea. *(Makofi)*

Nikianza kwenye uchambuzi na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa)

kwa niaba ya Mhe. Hamza Hassan Juma lakini amewakilishwa na Mhe. Mwanajuma Mdachi makamo wake, kwa kweli tunaishukuru tena kamati kwa maoni yao, mapendekezo yao waliyotupa na alhamdullillahi tumefanya kazi vizuri kwenye kamati na tutaendelea kufanya kazi , walitoa ushauri mwingi sana hasa kuhusu majengo ya Ikulu, uwekaji wa miundo mbinu mipya ya maji kule Wete, utafutaji wa hati miliki, kuzalisha kazi za kiraia kufuata sheria na taratibu za uajiri, utekelezaji wa ahadi za Rais zote tumezisikia na zote tuna kitengo maalum kile cha *private office* ya Mhe. Rais, wapo waandishi maalum wa Rais ikitolewa ahadi tu wanaiandika na tunaichukua tunaifanyia kazi.

Kuhusu posho nyeti kwa afisi ya vitambulisho nalo tumelisikia, kuhusu ushauri wao wa kuimarisha utaratibu unaohusiana na Tawala za Mikoa pia nao tumesikia, kuhusu ushauri mzuri wa kuwepo utaratibu mzuri wa utumiaji fedha kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje pia nao tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Lakini ushauri mwengine aliouzungumza kuhusu *uni-vise* yaani tusikubali kirahisi maana tutapoteza mapato hiyo ni kweli na sisi kwa sababu tunategemea sana watalii, hili tunalitizama kidogo kwa jicho la upande hili kidogo tunaona si muafaka kwetu. Kwa hivyo ushauri wako tumeusikia na hilo lilikuwa ni *propose* hata wenzetu walikataa, hata nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa hili watu wavuke tu mpakani kiholela limekataliwa tukasema lazima watu wavuke kwa kutumia *passport* kwenda hivi hivi tu haiwezekani.

Lakini pia Tanzania kwenda kwenye mikutano ya Jumuiya ya kikanda ushauri wake tumeusikia lakini hili juzi Mhe. Mwanasheria Mkuu wa serikali tunamshukuru alitoa ufafanuzi mzuri sana, kwamba kwa sasa jamani bado tupo chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa naomba tuavumiliane tunazungumza. Lakini suala la msingi nataka kulisema wenzetu wanatusikiliza kwa kila hoja ya Zanzibar na alhamdulillahi tunawakilishwa vizuri sana wataalam, Makatibu Wakuu, Mawaziri halafu kama kuna mazito hata Rais wetu anaalikwa, kwa hivyo hatudharauliwi na kuwa kama raia wa daraja la tatu, tunaingia tunajadiliana na wenzetu tunazungumza ipasavyo, hata wakati mwengine tunapewa kiti, kwa hivyo hilo ni jambo la msingi kwamba na sisi tuna heshima kubwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti nae alizungumza kwa upande wake Makamo Mwenyekiti na wengine kuhusu suala zima la Baraza la Manispaa, hili nitakuja kulizungumza baadae kwa urefu sana. Lakini naona bora nilimalize kwa sababu lilikuwa ni suala zito sana na wengi wamelizungumza bora nilizungumze kabisa, kuhusu suala la utendaji katika Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, Mhe, Makamo wa pili wa Rais alizungumza kwamba madiwani wamekaa kuhusu taratibu zao na wao wakatoa mapendekezo yao, mapendekezo yao wamempelekea kopi ya barua yeye kwa bahati mbaya nikawauliza wenzangu mbona mimi hamjaniletea, wakanambia tumeituma lakini haijafika. Kwa hivyo bahati mbaya mimi haijanifika lakini hilo sio neno nataka kusema kama alivyosema Makamo wa pili wa Rais wao wametoa mapendekezo yao tumesikia, lakini sasa tokea mlipotuagiza kikao chetu kile ambacho tulijadili suala la Manispaa serikali pale pale ikatoka ikenda kulifanyia kazi suala hili na uthibitisho huo Mhe. Naibu Spika, tarehe 29 Mei, 2011 Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi akaunda atume nzito kabisa, kaniandikia mimi kwamba imeteuliwa Kamati ya kuangalia utendaji wa Baraza la Manispaa na kupendekeza hatua za kuchukuliwa za kurekebisha utendaji wa baraza hilo.

Serikali tarehe 29 Mei, 1011 imeunda kamati hiyo na nataka niwatajie wajumbe wake ili muonea kwamba ile timu uzito wake.

Dokta Khalid Katibu Mkuu Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais -Mwenyekiti kama alivyosema Makamo wa Pili kwamba Katibu wake Mkuu ndio anafanya kazi na ndio dhamana na walipewa mwezi mmoja walete ripoti yao tarehe 20, Jun,2011. lakini bahati mbaya kutokana na bajeti na ziara tulizokuwa nazo za Mhe. Rais wameomba radhi kwamba watachelewa na wanaomba muda zaidi wala sio neno bora wachukue muda zaidi lakini watuletee kitu kizuri.

Wajumbe wengine wa Kamati ni:-

Ndugu Naim Ramadhani Pandu	Yeye ni Mkurugenzi katika Idara yetu ya TAMISEMI
Ndugu Said Hassan Said	Naibu Mwanasheria Mkuu yumo kwenye kamati .
Ndugu Asha Ali Abdalla	Katibu Mkuu Wizara ya Ajira, Uwekezaji na ushirika.
Ndugu Omar Hassan Omar	Mhasibu Mkuu wa Serikali
Ndugu Abrahman Mnoga	Afisa Mradi kwetu huku ndani ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais na

	Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
Ndugu Mwalim Ali Mwalim	Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Majenzi, Nishari na Maji.
Ndungu Mwinyi Ussi Abdalla	Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI
Ndugu Abdi Khamis Faki	Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
Ndugu Kai Bushir Mbarouk	Mkurugenzi wa Utumishi, Wizara ya Katiba na Utawala Boara.

Waheshimiwa Wajumbe tisa wako kwenye kamati hii kwa hivyo nakuonyesheni kwamba serikali ipo makini juu ya suala hili imeunda kamati hii kutoka katika mambo yote, kifedha , Mjimkongwe itizamwe Manispaa kwa undani wachimbue halafu halafu waiambie serikali jamani Manispaa imeoza ivunjeni. Au pana matatizo hapa turekebishe hivi. Kwa hivyo nakuombeni sana Waheshimiwa tusubiri kidogo kamati kama alivyoahidi Mhe. Makamo wa Pili ilete taarifa yake na naamini hutowakaribia na kuwadanganya.

Kwa hivyo waehsmimiwa mimi nakushukuruni sana sana kwa michango yetu kwa sababu mmezungumza kwa uchungu, wengine mmesema Mhe. Asaa Othman Hamad sisahau anasema tutaitoaje pesa nyengine kuipa ruzuku ikiwa hizi zinapenda, nasema zile pesa zaidi ni ruzuku kwa mishahara sasa tusiwanyime ndugu zetu mishahara haya mengine tutayarekebisha nawaombeni jamani tutarekebisha tuone kwamba tunatekeleza.

Halafu tizama basi kuna *point* nyengine hata *World Bank* au Wizara ya Fedha yenyewe waliposaini huu mkataba wakasema bora uje kwetu Wizara ya Fedha tubaki nao sisi kama nilivyosema, wakaona huku kidogo mambo sio mazuri wakasema tungojee kwanza hizi pesa tusipeleke kwa hivyo pesa za mradi zimebaki Wizara ya Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo wao ndio wanazitunza, wanatwambia tu nunueni hiki sasa, fanyeni hichi na hichi kwa hivyo nawaomba wenzangu watufahamu nini dhamira yetu hatumlindi mtu isipokuwa akifanya vizuri tutamsifu na kama kafanya vibaya tutamrekebisha.

Mhe. Spika, nilisema hili bora nisingojee bora nilizungumze moja kwa moja kama nilivyosema waheshimiwa takriban wote wamelizungumza hili, lakini aidha tuliambiwa kwamba kuna deni la Shilingi milioni 700 zimeelezwa na baadhi ya Waeshimiwa wa Baraza kwamba ni malimbikizo la madeni na matengenezo mbali mbali ambayo hayakulipwa kwa manispaa zaidi ya miaka mitano. Haya ni malimbikizo ambayo Manispaa wanadai yapo tunadai sisi malimbikizo haya ni ujenzi wa minara, vibendera posta, michoro ya ukutani, matangazo ya magari na sio gharama za kuweka mabango kama vilivyoelezwa na baadhi yetu au kuleta ughali wa biashara ya matangazo.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi zilizochukuliwa katika vikao vya pamoja baina ya Manispaa, Zantel na wanasheria deni hilo hadi sasa halijalipwa, fedha zilizolipwa ni Shilingi milioni 15 kwa ajili ya matangazo yaliyoanza mwaka 2010, yule aliyesema tumeanza kuzungumza nao na waheshimiwa mmekubali mkasema kweli huo ndio ulikuwa ushauri wetu wa mwanzo kwamba nyinyi bwana bora mfanye na makampuni yenyewe tumekubali na tumeliona tatizo, kwa sababu unajua mikataba ina ufupi kuna vipengele na lazima tukubali kwamba baadhi ya wanasheria wetu wepesi. Ndio maana tukasema ndani ya Baraza la Manispaa tutahakikisha mikataba yote lazima iende kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu na pia hata kutia mikataba ile kamati ya Baraza la Manispaa waelimishe isiwa mtu mmoja peke yake anamaliza, kwa hivyo mimi nilisema nilisisitize na mlivyotushauri tumesikia.

Halafu kulikuwa na ujenzi wa hizi kazi anazofanya Mkurugenzi wa Manispaa ni kweli nafikiri imezungumzwa na waheshimiwa wengi hapa, kwamba Mkurugenzi anawajibika kwa Baraza la Manispaa lakini nawaombeni tufahamu jamani yeye yule ndio mtendaji Mkuu kama Katibu Mkuu kwenye Wizara, lakini kweli nakubali mlivyosema anapaswa awajibike kwa Baraza la Manispaa awajibu afuate maelekezo sasa kama kidogo anateleza basi hapo anateleza kibinaadam na t umesikia tutamrekebisha.

Mhe. Shimba alisema kwamba kuna ajira hivi karibuni kuna wafanyakazi wengi tu waliajiriwa lakini Mkurugenzi kachukua peke yake hizo nafasi hata yeye kataka hakupata, nataka kusema kwamba ni kweli Baraza la Manispaa hivi karibuni liliendelea na juhudi za kuombea serikali ajira wafanyakazi 83 kutoka katika ajira ya kutwa kwenda ajira ya kudumu, juhudi hizo zilianza tokea mwaka 2003 na sasa zimefanikiwa na utekelezaji wake utanza karibuni hivi. Lakini wafanyakazi hawa ambao miongoni mwao wameshatumikia Baraza la Manispaa zaidi ya miaka kumi, hata hivyo suala la uwezo wa Manispaa juu ya taratibu za ajira kwa wafanyakazi ni miongoni mwa mambo ambayo yatafanyiwa mapitio katika mpango mzima wa marekebisho ya serikali za mitaa, hili tumeliona kweli kuna matatizo uajiri na hata mmetwambia kuna maofisa pale wanafanya kazi sio zao.

Sasa hii kamati yote hayo itapitia halafu itatizama na itatushauri ipasavyo kweli sio jambo zuri mtu kasomea utaalam wa bustani ukamuweke ofisini inakuwa haina maana wala haipendezi kwa hilo tumelisikia na tutalirekebisha Mhe. Makam Mshimba Mbarouk.

Lakini kulikuwa na ajira nyengine za juzi juzi tu hapa kupitia huu mpango wa LO wa usafi wa mitaani na hiyo tujaribu sana waheshimiwa kuwashirikisha kwenye majimbo yenu na kwenye wadi zenu, lengo letu ni kwamba usafishaji wa eneo basi wasafishaji watoke katika eneo lile hilo ndio lengo letu, isiwe mtu anasafisha Kwamtipura anatoka jimbo langu la Dimani itakuwa haitii sura nzuri anaesafisha pale akae maeneo yale yale awe analitunza na analipenda lile eneo hasa aone pale ikiangushwa karatasi tu basi dhamana yeye. Sasa hili Mheshimiwa Mshimba tunakushukuru tumelisikia.

Lakini kulikuwa na suala jengine la kanuni za masuala ya malipo ni kweli maduka yanalipa shilingi lefu sita za taka utaratibu wa kisheria na kanuni za Manispaa zimeelezwa mpango unaorahisisha kutoa ada hizo, kuondoa usumbufu kwa wafanyabiashara kupata huduma ya kuondoa taka taka hizo. Ada hizo ziko tofauti kwa sekta za biashara mfano maduka ada yake Shilingi elfu sita, maduka makubwa Shs. 9,500 hoteli na skuli zimewekwa kwa glass maalum. Mfano Class (A) shs 50,000 Class (B) Shs. 60,000 ambapo utaratibu umefuata kupitia katika Baraza Kuu mwezi Disemba, 2009, katika utaratibu wa ukusanyaji wa mapato soko la Mwanakwerekwe mapato ya ndani ya soko yanatozwa na muhisika wa kitega uchumi hicho, pia biashara zote za nje mapato yanatozwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa pale, hivyo ni kweli inawezekana kuwepo na risiti za rangi tofauti za Manispaa na Halamashari ya Wilaya ya Magharibi, lakini la msingi kwamba risiti zote ziwe za Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa upande wa biashara wa nje na ziwe na nembo ya Baraza la Manispaa kwa ndani, vyenginevyo nawaomba wafanya biashara wetu watusaidie wasikubali na wasitoe pesa wawe wabishi hasa lazima ipatikane risiti yenyewe kabisa.

Kuhusu upande wa Manispaa kama nitasahau siwezi kuyazungumza yote moja baada ya moja lakini kama nilivyosema suala la *management* ya Manispaa tunakubali kwamba kuna matatizo, na hili nimelikubali tokea wakati ule kwamba tuna matatizo hilo silikatai, kwa hivyo kama kuna matatizo basi tunakubali kwamba tutalifanyia kazi. Sasa hatufanyi kazi kama Wizara tunafanya kazi kama Serikali kuu kuona kwamba kioo cha mji wetu kinakuwa safi.

Waheshimiwa sasa naomba nizungumzia suala la majengo ya Ikulu, kwa upande wa majengo ya Ikulu hapa naona moja kwa moja niende kwa rafiki yagu Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa sababu yeye alinambia hatokubali kama

sikumpa maelezo mazuri, sasa na mimi nimeona nichukue buku moja kwa moja na buku hili tukianza ukurasa wa 131 pale kuna kifungu kimeandikwa 220700 Matengenezo ya Ofisi na nyumba hapa buku limekosea kwa hivyo marekebisho yafanywe ni marekebisho madogo mdogo kama vile balbu ndio kifungu hiki kwa hivyo kidogo hapa buku limekosea.

Lakini pia kwenye ukurasa wa 134 kifungu 0901 pale imeandikwa idara ya kazi maalum, wameikosea jina lake ni Idara ya Uratibu Idara maalum ya SMZ ambayo imetamkwa wazi wazi kwanye hotuba ukurasa wa 76 kwa hivyo hapo ndipo palipokosewa hiyo ni idara mpya, kwenye hotuba yetu tumeizungumza hiyo,

Kwa upande wa maendeleo uliuliza pesa zile ziko je, ukiangalia kwenye ukurasa 633 shilingi 300 milioni ni matengenezo ya nyumba za Ikulu na nyumba za Serikali, Shs. 150 milioni mradi wa marekebisho ya Serikali za Mitaa na Shs. 100 milioni Mradi wa Mawasiliano, jumla zote 550 milioni. Sasa nilihisi hili bora nilizungumze mapema ili kidogo aweze kulifahamu Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Spika, labda sasa niende kwa Mhe. Rashid Seif yeye alizungumza mengi na kubwa alizungumza kwamba tubadilike mimi nakubaliana nae katika suala zima la kubadilika na alikuwa na maoni yake juu ya suala la jela, mimi nasema hilo tulizungumze baadae lakini Baraza hili ndio lililopitisha sheria ya kuitwa Chuo cha Mafunzo na madhumuni yake kama walivyosema Waheshimiwa tokea enzi za Mzee Karume wale wanafunzi au wafungwa wapate mafunzo ya kujitegemea ili warudipo wakajirekebishe upya hilo ndio suala la msingi, suala la watoto wadogo hilo tumelisikia na kama nilivyosema Baraza la Manispaa nalo tutalifanyia kazi.

Pia aliuliza bilioni 39 zimetolewa kwa Mji wa Unguja na bilioni tatu tu zilizopelekwa Pemba kulikoni mambo yamepangwa pangwa vipi, ninachotaka kumueleza Mheshimiwa kwamba mradi huu wa ZUST chanzo chake hasa umeanza katika wamu mbile za usafi wa mji wa Mkongwe, kulikuwa na awamu ya kwanza ikaja na awamu ya pili. Sasa *base* au *project* hizo enzi za nyuma ndio ukabuniwa huu mradi mkubwa huku ndio chanzo chake, sasa tukaona kufanya peke yetu kwa sasa kwa mradi huu itakuwa sio vyema kwa hivyo ndio tukazingatia tukasema basi tuingize na Pemba na wao kwa kuanzia ili kama tunasaidia utendaji wa Halamashauri zao, sasa binaadam tumeona kwamba tumeshafanikiwa mradi huu tumeanza basi tunaweza kuandika mradi mwengine kwa kuombea sasa miradi ya Pemba lakini hii iliandikwa zaidi kwa Unguja kwa matatizo tuliyokuwa nayo ya kutuwama maji na michirizi na misingi, hili nimesema bora nalo Mheshimiwa nimuwekee uwazi kabisa.

Suala la Madiwani tumesikia, changamoto kwenye Zimamoto wanasema Waziri hakipendi mimi nakipenda kweli kweli najua ni hatari ni lazima moto hujui kitatokea nini, kwa hivyo t unakipenda na kila jitihada serikali inafanya ili kuona kwamba suala hili la kikosi hiki tufanya yanayofaa.

Mhe. Asha Bakari Makame nawe tunakushukuru kwa michango yako mizuri kabisa na niseme kwamba kama ulivyosema dhamira sio kukomoana au kumkomoa mtu lakini ni kuelekezana mambo yetu yaende vizuri, nakubali kauli yako na hii ndio nilisema mwanzo kabisa kwamba tunakubali kukosolewa ili tuone kwamba mambo yanakwenda vizuri.

KMKM tuliambiwa tuionee huruma tunakubali, mageuzi ya kilimo JKU na Mafunzo hayo pia tumesikia na tutajitahidi tunakwenda nao wanafanyakazi nzuri data nafikiri tumeziona kwenye kitabu za ujenzi, lakini ulitushauri mambo ya fanisha kutoka nje basi tumesema tutatizama kadri ya uwezo wetu uko je lakini suala la kwamba na wao tuwape soko fanicha zitoke hapa hapa nalo tumesikia. Lakini ulinisisitiza kwamba tubadilike kitabia mambo yetu tufanye kwa kisasa zaidi nalo tumekubali na tumesikia.

Aidha ulizungumza upande wa Mwanakwerekwe kibanda cha nyama tumejaribu kufuatilia kibanda hicho umekusudia kipi hasa, sasa nakuomba baadae tutoke mimi na wewe twende hasa Mwanakwerekwe mguu kwa mguu ukatuonyeshe hiki tusiende karibu pale lakini utatwambie kile basi tutatizama utaratibu wa kusuluhisha.

Mhe. Panya Ali Abdalla umezungumza mengi hasa nyumba ya mzee Mkokotoni tumesikia na sio nyumba ya Mkuu wa Mkoa tu lakini nyumba zote kweli, Afisi za Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kama nilivyosema tumesikia tuna matatizo ya bajeti lakini tutazifanyia kazi ipasavyo. Umetoa pongezi nyingi sana kwa vikosi tumezipokea, aidha upande wa KMKM na Mafunzo nao umetoa fikra nyingi tu nazo pia tumezipokea.

Mhe. Moh'd Haji Khalid yeye alisema uharibifu wa mazingira Muwambe udhibitiwe hiyo tumesikia na nafikiri kauli imeshatoka na hata kwenye kitabu chetu tumesema tuhakikishe kwamba mazingira yale uchafuzi wake tuudhibiti, kulikuwa na agizo kidogo waheshimiwa wengine walikuwa wanasema labda tupige marufuku sasa tukishapiga marufuku kule kuna ajira za watu sio chini ya elfu tatu, sasa lazima tufikirie tunawatoa pale lakini tunawapa kazi nyengine. Hata tulipokwenda na Mhe. Rais akaagiza kwamba atukae pamoja wataalam wetu wa Mazingira, Watalam wa Wizara ya Kilimo na Maliasili na wale wenyewe wachimbaji tuone, kwa sababu wao waliambiwa wachimbe mita tatu na wao wanasema tatu ni kidogo twende mpaka sita chini, sasa sita chini kule ndio mbali zaidi sasa tumeagizwa tukae pamoja, kwa sababu ile almasi

yenyewe ile dhahabu iko huko chini sasa tutajitahidi tukae pamoja tuone kwamba wanachimba vizuri na tunayatunza vipi yale mazingira baada ya machimbo.

Mhe. Subeit mfano mzuri ni kwako na watu waliambiwa waende wakasome kwako baada ya kuchimba mkawa mnayatunza vizuri, ila wamesema tutajitahidi t utapeleka watu wende wakasome tuone watu wanayatunza vizuri.

Mhe. Asaa Othman Hamad najua umesema mengi lakini kote huko ulizunguka na kurudi kwenye Manispaa tu na nafikri nimeshaeleza mengi sana kwenye Manispaa na tutajitahidi, kuhusu utatu tutafaidika vipi si wewe tu hili hata Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hija Hassan Hija nae aliuliza tunafaidika vipi, lamsingi kwamba soko limepanuka na biashara zetu za Zanzibar hapa sasa zinatoka leo kuna meli zetu nyingi zinakwenda kuuza bidhaa Comoro, kuna watu wanasafirisha hapa kwenda zao Malawi, Zambia wapo hapa biashara zinatoka. Sasa hii itarahisisha kwa sababu haya mambo ya *tariff* yataondoshwa kodi zile kati ya mipaka yetu zitaondoshwa ndio utatu wenyewe huo, kwa hivyo soko letu litatatuka wafanyabiashara wetu nashukuru wanafanya kazi nzuri sana.

Kwa hivyo hili litaturahisisha hata kutoka nje ya mipaka sasa hawa watu wakorofi kidogo wanaotubana wataona haya wenyewe watazuia hapa wakati mambo yanakwenda zake huko, kwa hivyo wafanya biashara wetu watapa faida kubwa zaidi na zaidi na mifano ipo leo ngano ya bakharesa ipo Malawi, ipo Ruanda, ipo Malawi hii ngano, Michele hii inayokuja hapa unaikuta Comoro kuna meli hapa zinakwenda Comoro na kurudi biashara imekuwa kubwa sana. Kwa hivyo zaidi tutafaidika huko. Lakini pili tutafaidika upande wa miundo mbinu na utalamu wa miundo mbinu mingine na sisi tutakuwa na fursa zaidi tukiingia humo.

Mhe. Spika, nizungumze suala la GSO Mhe. Asaa yeye nafikiri amezungumza, Mhe. Hija na hasa kubwa walizungumzia kwamba Baraza la Wawakilishi nalo linapaswa kuchunguzwa.

Mheshimiwa kinachozungumzwa hapa ni usalama wa nchi, usalama wa dola. Hatuingii mambo ya ndani ya uendeshaji wa *activities* za Baraza la Wawakilishi au nini. Hii ni usalama wa nchi. Dhamana tumewapa hawa watu wawachunguze watu kwa usalama wa nchi na hata majengo. Mathalan tuchukulie wapo *security* pale wanachunguza na *screen* yetu tunapopita wana mashine yao. Wale ni wa serikali, tuseme tuwaondoe kwa sababu ni Baraza la Wawakilishi. Hapa tunataka tusaidiane vyombo vyetu, mambo yetu yaende vizuri, hilo ndio suala la msingi. Hatuna haja kwamba tuingie Baraza la Wawakilishi tuchunguze mambo.

Mhe. Spika, Mhe. Jussa alizungumza mengi lakini na yeye alitoa pongezi tumezipokea na yale aliyoyataka nimajaribu sana kuyarekebisha. Alizungumza kwamba kila mwezi Mhe. Rais aongee. Si vibaya lakini sisi tumejiwekea utaratibu na mwenyewe Mhe. Rais na ameshauri aongee kila baada ya miezi mitatu. Sasa ikitokezea haja ya kuongea kabla ya miezi mitatu atafanya hivyo.

Suala la vitambulisho waheshimiwa wengi wameongea na zaidi wamesema kidogo kuna usumbufu. Hilo tumelisikia na huu usumbufu ndio maana tukasema tujenge ofisi za Wilaya ili mambo yote yawe *facilitated* kule. Kuna mashine za kisasa kule, zitasaidia sana, watu tumewaajiri wapo kwenye Afisi za Wilaya. Hiyo kero tumeisikia na tutaifanyia kazi.

Mhe. Jussa pia amezungumza mbona bajeti ime – *shoot* mwaka huu. Ime *shoot* kwa sababu huko nyuma mambo yote tulikuwa tunayatumia kwenye Bajeti ya Maendeleo, mwaka huu kwenye Bajeti ya Maendeleo imepunguzwa sana. Mwaka jana tulipata bajeti ya shilingi 800 mwaka huu iko 150, yameonekana mambo mengi ni ya kawaida kwa hiyo imepelekwa kwenye *recurrent* mwaka jana ilikuwa 910, mwaka huu ime *shoot* mpaka kufikia 1.248 bilion. Matumizi yametoka kule kwa sababu mengi ni ya kila siku, tumehisi yapelekwe kule na serikali. Sisi tumekubali. Zaidi ya kwamba kuna shughuli za kufatilia na shughuli nyenginezo za kawaida.

Suala la *Direspora* waheshimiwa kama walivyosema tumelikubali. Lakini kulikuwa na suala la msingi kwa nini viongozi wetu au wageni wetu hawaji wanaishia Bara tu, tukaambiwa Rais Bush, Rais Abdul Gul wa Uturuki, Hu Jintao, *Foreign Minister* wa *United State*. Kwa kawaida haya mambo zaidi yanapangwa kati ya nchi kupitia ubalozi wake aliyekuwepo Tanzania. Yeye ndiye anakaa anawasiliana na kwao. Na hasa tatizo kubwa ni muda. Lakini kilio tumekisikia waheshimiwa na tutachukua juhudi ili kuwasiliana na wenzetu kuwambia jamani mkizungumza Tanzania basi lazima muiunganishe na Zanzibar ndio mnapata *United Public of Tanzania*. Ukisema mgeni anakuja Tanzania lakini anafikia Dare-es-Salaam na kurudi kwa kweli haipendezi.

Mhe. Viwe tunakushukuru kwa yote uliyozungumza, hasa Baraza la Wete umesema kusitiwe tena kifungu, itiwe barabara ya lami. Tumesikia lakini tujue kama lami ni ghali kilomita moja tunaambiwa shilingi milioni 800. Tukasema ngoja tuanze kidogo kwa fusi baadaye tutakuja.

Mhe. Abdalla Mohammed wa Mkoani tunakushukuru sana kwa maoni yako yote kuhusu usafi. Baraza la Manispaa, Diaspora, mengi tumeyasikia.

Mhe. Mtando pia na wewe tunakushukuru kwa mchango wako na kama ulivyosema kwamba hii ni *process* ya serikali za mitaa, kama tulivyoanza sasa

hivi kwa *public service reform* tunatarajia mambo yake yataanza karibuni. Na hii yetu ya Serikali za Mitaa tutaifanyia *Pilot project* au kuanza kutekeleza tukijaaliwa labda mwaka ujao na mwaka huu tutakamilisha haya mambo yote.

Halafu gari la mawasiliano Ikulu nafikiri lipo kwenye mpango na nafikiri mwaka huu wa fedha tutalinunua tuone Rais wetu anapokwenda pale pale imekamilika, anafunga spika anahutubia na watu.

Vitambulisho ulizungumza kama ulivyosema, hilo ulilozungumza kule Tunguu ni *temporary office*, itarudi Dunga. Kunafanywa matengenezo tu. Pia na wewe umezungumzia suala la mazingira Saateni, mazingira yake ni mabaya. Tutajitahidi hasa wakati wa mvua kuyarekebisha. Pili ulizungumza Mahakama pale Baraza la Manispaa. Mahakama ya mwanzo kama zilivyo Mahakama nyengine na hiyo inajitahidi kwa hizi kesi za Manispaa kutusaidia.

Mhe. Salum Abdalla Hamadi wa Mtambwe, tunakushukuru sana kwa yote uliyotuchangia hasa vitambulisho vya Mzanzibari na mengine. Lakini umesema kwamba magendo ya karafuu hili tulipige vita sote na wewe kule upo kwenye njia. Tusaidiane lisiwepo ili tupate *revenue* kwa nchi yetu tuweze kuendeleza. Sasa hivi bei ni nzuri na serikali nayo itajitahidi kufanya vitu vyake.

Mhe. Abdi Mosi Kombo (Captein), tunakushukuru sana, yote uliyosema tumeyapokea. Lengo letu kila Wilaya ipate Kituo cha Zima Moto kwa hiyo Matemwe kama itaangukia kule riziki yako basi tutakuwekea matemwe, ili kurahisisha mambo. Serikali imeshafanya mambo mazuri sana, tayari hapa pwani tumeshapata ruhsa na tumeshapata sehemu ya kuweke kituo. Hata Uwanja wa Ndege wenzetu wameshatwambia washatupa sehemu ambayo tutaweka kituo kizuri. Lakini kile kituo chetu kikubwa cha Zimamoto tumeshapata sehemu Magogoni lilipokuwa jengo la Afisi ya Mhe. Makamo wa Rais. Pale ndio patakuwa Kituo chao Kikubwa kwa sababu pale barabara iko wazi, itakuwa rahisi wao kutoka na kuingia. Tunajitahidi kufanya kazi na Mikoa ili tuone hili suala linakuwasilishwa ipasavyo.

Mhe. Subeti nakushukuru sana, umezungumza yote, ukazungumza suala la nyumba ya Ikulu ya Micheweni. Kweli lengo ile nyumba ilikuwa iwe Ikulu na tutatizama vipi tutakwenda nayo na ule ujenzi ulikwama kweli, kulikuwa na matatizo sasa ujenzi ule tutaukwamua tuona itakuwaje hatima yake ya baadaye, itakuja sio kwamba tumeitupa ile nyumba.
Kuzungumza suala la kupigiwa saluti na vikosi vyetu au heshima hawaitoi ipasavyo. Hilo naomba radhi kama ilitokezea sio lengo lao. Unajua wakati mwengine Mheshimiwa Subeti, hata miye unanibabaisha maana siku nyengine unavua kofia unapiga suti nzuri nzuri unakuwa unabadilika, sio picha yako ya kawaida ile. Sasa labda upige picha mbili suti bila ya kofia, halafu na nyengine

upige na kofia yako ile watu waiyone. Mhe. Subeit *concern* yako tumeipata, tutawaelimisha vijana wetu kwa kweli wengi wapya, tuone kwamba mnapata mambo mnayostahiki.

Mhe. Asha Abdu Haji, tunakushukuru sana na wewe, michango yako ni mizuri uliyotupa. Wilaya ya Kusini pesa walizopata ni kidogo na *reforms* zile tumesikia tutaziyashughulikia ipasavyo.

Mhe. Mohammed Said jimbo la Mpendae suala la mchirizi wako wa Migombani umesema kwamba hausafishwi. Tumesikia hicho kilio na tutahakikisha kwamba tunamuweka mtu *permanent* ule msingi unasafishwa ili muda wote yawe maji yanakwenda vizuri. Pia ulizungumza suala la risiti za Manispaa kama ulivyozungumza aina za risiti ziliopo.

Mhe. Saleh Nassor Juma, tunakushukuru kwa mengi uliyozungumza na kwa kweli ulivyounguruma huko nimekusikia na nimekufahamu. Lakini zaidi nyumba ya ma RC na ma DC kama mlivyosema tutajitahidi sana kuzijenga kadiri tutakavyopata pesa kuziweka katika hali nzuri.

Ulizungumza suala la ajira vijana wanavyochukuliwa wanachukuliwa vipi. Nitaunganisha na Mhe. Mshimba, vijana hatuendi kwa itikadi nafasi zikija zinapelekwa Mikoani na huko tena kuna utaratibu wao wanakwenda kwenye *screaning* mpaka wanafanyiwa *medical check up*. Tatizo ni nafasi huwa chache na msongamano unakuwa mkubwa na manung'uniko yapo hatukatai.

Pia umezungumzia suala la mtondoo tumelisikia na hilo na tunalipiga vita vikali sana. Hata kwenye kitabu tumezungumzia *strategic plan* ya kurekebisha mwenendo mzima wa Chuo cha Mafunzo.

Halafu kulikuwa na kwiri moja ya *audit* kwiri nimeisema ya shilingi mia 390 na pesa nyengine ambazo ma *audit* kwiri, yale yote yameshajibiwa na tatizo ni kwamba Kamati ya PAC iliakhirisha kikao chake kwa hivyo nafikiri hawakuweza kuiwasilisha. Watu wetu hawakuweza kutoa ripoti. Vyote hivyo vimeshapatikana nafikiri ikikutana PAC wataoneshwa hizo audit kwiri watajibiwa.

Mhe. Hija alizungumzia Kamata inaishia kujibu upande mmoja vipi tutafaidika na Uhusiano wa Kimataifa na wa Kikanda na vipi tutaridhia misaada ya kimataifa kwa masuala ambayo kuwa sio ya Muungano. Ni lazima tufanye mipango tuone haya mambo yanakuja moja kwa moja isiwe wanamaliza wenzetu wa SMT kwenye Bunge.Unajua kuna tatizo la Katiba, hayo yatakaporekebishwa tuta *press* na sisi haya mambo yaje na kwetu moja kwa moja kwa sasahivi *mandate* hatuna.

Tunakushukuru kwa *slogan* yako kwamba kero isiwe suluhu ugomvi. Ulizungumza mengi kuhusu Baraza la Manispaa. Tumeyasikia vitendea kazi vitaongezwa, umetaja humu namna ya vitendea kazi. Lakini tunakushukuru mtaro *Botanic Garden* upo na umo kwenye mpango, utajengwa ule na usiwe na wasi wowote na mitaro mengine iliyounganishwa na jirani zako wa Jang'ombe na Mpendae pia itashughulikiwa. Soko la Mombasa matumizi mbadala. Tumelisikia suala hilo na tutakaa na wenzetu tuone. Unajua mambo ya soko tuyafatilie tuone yakoje.

Mhe. Farida tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri uliyoutoa na ulizungumzia suala la msingi au upanuzi wa jengo, kwenye Halmashauri ya Wete. Ule ni utanuzi wa jengo, jengo ni dogo kwahiyo wanataka kulitanua. Wanakiwanja pale wanataka kukichukua ili waweze kuongeza kidogo.

Mhe. Mussa wa Jimbo la Koani tunakushukuru kwa maoni yako yote na maelekezo yako. Na historia uliyotupa ya nyuma yote tumeisikia.

Mhe. Bikame Micheweni hakutupwi kila juhudi tunafanya. Kuna mradi mkubwa sana wa JP5 tunakusudia kuna mambo ya Afya, Mji, Kilimo, Elimu na Maendeleo ya Wanawake na Watoto, kuona hali za wananchi wa Micheweni zinanyanyuka. Huu ni mradi wa UN na umeona mwenyewe mpaka radio Jamii imekuja, Tangi kubwa la maji, miundombinu yote itarekebishwa. Kwa hiyo hatukutupi Micheweni.

Mhe. Ali Salim tunakushukuru sana kwa kutoa uzoefu wako mkubwa wa miaka 10 uliyokaa pale katika Baraza la Manispaa. Na nakubaliana na wewe kwamba kweli mengi mazuri yamefanywa lakini ndio unapofanya mazuri ndio binaadamu kuna mengine unateleza. Mkurugenzi wetu ni mtu wa fedha, mtu wa *revenue*, kahamasisha ukusanyaji mkubwa wa mapato yametoka shilingi milioni 400 yamekwenda mpaka bilioni moja zaidi ya asilimia 82. Tunamshukuru sana kwa hili. Kama nilivyosema binaadamu ana kasoro zake, kwa hiyo tuchukulie kasoro zake hizi tujitahidi kukaa naye tuone kwamba tunakwenda vizuri.

Mhe. Mohammed Mbwana wa Chambani na wewe tunakushukuru. Umesema kwamba jengo la Chakechake ni bovu, tumekubali si hilo tu. Lile sasa tutaliacha kwanza na wameshaahamia jengo jipya pale ili wastirike wasije wakaangukiwa na jengo. Azma kama itayimkinika tulitengeneze upya.

Mhe. Hassan Hamadi wa Kojani na wewe tunakushukuru kwa yote uliyozungumza. Matatizo ya usajili wa vitambulisho urekebishwe. Tunakubali na tutayafanyia kazi.

Mhe. Dr. Sira (Naibu Waziri wa Afya) tunakushukuru sana suala ulilozungumza la Mchangamle kwamba tusidharau mgogoro wa kule. Tunashukuru lakini leo nilisikia tu kwenye vyombo kwamba mgogoro wa Mtende umeshakaa sawa au umeshatia sura nzuri. Tutajitahidi kuona kwamba hii migogoro mengine tunaiweka sawa.

Mhe. Salmini Awadh na wewe tunakushukuru sana kwa maoni yako na umesisitiza kwamba wafanyabiashara wa njiani kwa kweli waondoke. Hilo ni kweli na kweli linakera haitii haiba nzuri mjini. Tujitahidi tufanyebiashara pale palipokubalika, pasipokubalika basi mtu akubali na tumeshatenga mahali wale wa njiani mle waondoke waende zao Saateni, kama wanabaki pale kwa kweli haipendezi, si jambo zuri. Tusitafute polisi tukaanza kusukumana hali hiyo imeshapitwa na wakati. Nafikiri tutajitahidi kuwaelimisha wenzetu na naomba Mheshimiwa tusaidiane ili tuwaelimisha wenzetu. Mtu akiambiwa hapa usifanye biashara basi asifanye, si jambo zuri.

Ulizungumza Makatibu na Wakurugenzi wanawajibika kwa nani. Nimeshazungumza kwamba kweli wanawajibika kwa halmashauri hizi zetu za Wilaya.

Mhe. Mlinde na wewe tunakushukuru. Bajeti umeizungumza ya Chuo cha Mafunzo imepunguzwa lakini imeongezwa kwa upande mwengine kwa sababu kinajengwa Chuo cha Mafunzo kipya kwa hivyo imeongezwa kule. Shughuli zao hazitosita, shughuli za mfano chuo cha Mafunzo zipo nyingi kwenye *baiter first charge iterms*. Ikishakutoka mishahara tu basi na fedha zile zinatoka.

Mhe. Jaku tunakushukuru sana na pongezi zako wa wastaafu na wamesikiliza sana suala la Chuo cha Mafunzo na nafikiri mbali ya kazi zao za uanasiasa wewe ni mfanyabishara mzuri na una huruma. Kwa hiyo tutakuomba tusaidiane kuwashajihisha wafanyabiashara wengine ili tusaidie kuinua hali katika sehemu kama hizi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema michango ilikuwa ni mingi na ningechukua zaidi muda, lakini muda hauruhusu. Naomba niwaombe radhi kwa wale ambao sikuwagusa moja kwa moja au mchango wao sikuugusa. Naomba wachukulie kwamba tumeukubali na hii michango yenu itakuwa ni *working document* yetu kwa mwaka ujao wa fedha. Tutakaa tuone vipi maoni yenu tunayafanyia kazi ili mwakani tukirudi tusije mkatukosoa tena kwa haya. Naomba sana kwa heshima na taadhima mtukubalie mambo yetu yaende vizuri tutumie, tuukaribishe mradi mpya na tufanye kazi pamoja.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 17 – JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201	Utawala Unguja	15,000,000
Jumla ya Fungu		**15,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 18 – CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201	Utawala Unguja	27,500,000
Jumla ya Fungu		**27,500,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 07 – OFISI YA USHIRIKIANO WA KIMATAITA NA URATIBU WA ZANZIBARI

Kifungu 0601 Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa

Mhe. Ismaill Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye ufasaha. Katika suala la Afisi ya Ushirikiano wa Kimataifa nilikuwa naomba maelezo ya ziada tu kidogo katika suala hili la Viongozi wa Kimataifa wanapotembelea nchi zetu ambazo nilizungumza.

Nategemea idara hii kwa upane wa Zanzibar ndiyo itakayokuwa ina ratib shughuli zote za Ushirikiano wa Kimataifa bila shaka, kwa kushirikiana na

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ya Jamhuri ya Muungano. Katika maelezo yake Mhe. Waziri kasema kwamba suala hili watalifatilizia. Akasema suala hili pia linategemea kiasi kikubwa Afisi za Kibalozi zenyewe za zile nchi ambazo viongozi wale waliotembelea wanatoka.

Pamoja na kwamba wanaratib lakini bado na ile nchi inayotembelewa inakuwa na nafasi yake ya kuzungumza kile ambacho labda wangependa wakione na maeneo mengine. Nilitaka kujua kiasi gani Idara ya Ushirikiano wa Kimataita au Afisi ya Ushirikiano wa Kimataifa inashirikishwa katika Program hizi na Wizara ya Mambo ya Nje. Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo. Tumelizungumza hili tu, lakini kuna malalamiko makubwa kwamba Wizara ya Mambo ya Nchi kiasi kulani inadharau kwa upande wa Zanzibar. Mara nyengine katika kutia saini mikataba hii ya nje tuliwahi kusikia na pengine Dr. Mwinyi haji mwenye mzoefu alikuwa Wizara ya Fedha huko nyuma panakuwa pana michezo inafanyika.

Tuje katika hili la viongozi wa nchi za Nje kutembelea hapa, ambalo ndio ilikuwa hoja yangu ya msingi. Naomba maelezo je, Ofisi hii ya Ushirikiano wa Kimataifa Zanzibara huwa inashirikishwa na Wizara ya Mambo ya Nje katika kupanga ratiba za viongozi hawa ili kujua hatakama kwa masaa machache kama ilivyokuwa huko nyuma kuwa viongozi hawa wanafika Zanzibar. Nilikuwa naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Jussa alipochangia suala hili aliomba viongozi hawa wa Nchi za Nje au wageni wa kiserikali waje Zanzibar.

Nilimueleza inavyotumika na tatizo hasa nilisema ni muda. Kwa sababu na sisi tume *request* sana, jamani tunapozungumza *United Public of Tanzania* basi na Zanzibar, sasa kama mgeni anaishia Dare-es-Salaam huku hafiki sio vizuri. Tatizo ikawa ni muda na kushirikishwa kama wamepangwa wanakuja basi tunashirikishwa kwenye ofisi yetu hii ndogo ya Mambo ya Nje ya hapa, tunapanga nao na hata kule Bara tunakwenda. Anapokuja yule mgeni tunaalikwa kwenye vikao. Rais wa Mwisho Waziri Mkuu wa India juzi, mimi na Mhe. Mohammed Aboud tulialikwa kwenye mazungumzo yale . lakini hata kwenye mipango kama anakuja Zanzibar basi tunaalikwa. Lakini kama haji Zanzibar huwa hatualikwi.

Nataka kusema hilo tumelisikia Mhe. Jussa na kwa kushirikiana na Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais naomba hili Mhe. Mwenyekiti tutalichukua kama Kiserikali tuone kwamba hichi kilio cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kinafika kwa wenzetu. Ili waweze kuchukua hatua zifaazo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa maelezo fasaha ya Dr. Mwinyi Haji, labda kwa sababu ametupa maelezo ya ziada na mimi nililizungumza hili kwamba katika hii ziara ya mwisho ya Waziri Mkuu wa India bwana Manmohan Singh amesema viongozi hawa wawili wameitwa kushiriki katika mazungumzo. Katika mchango wangu nilizungumza kwamba India imetenga dola bilioni 5 mwaka huu kwa nchi za Kiafrika na katika kufatilia vyombo vya habari Tanzania ilipata sehemu fulani ya fedha hizo, ilitangazwa katika ziara hii. Sijui unaweza kutwambia katika hizo Zanzibar tumefaidika na tumepata kiasi gani.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mhe. Jussa tulishiriki mazungumzo pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kweli Zanzibar na sisi kwenye *package* tumeomba misaada kwenye vikali, tumeomba msaada kwenye miundombinu na tumekubaliwa lakini *figure* sijui kiasi gani. Kwa hiyo *package* inayotengenezwa tumeomba, pia tumeombwa mradi wa maji wa Mkoa wa Dar es Salaam na sisi tukalaumu kwa nini na sisi hatukuingizwa, tukaambiwa ata mnaweza ku-*request*. Kwa hiyo *room* ipo ya ku-*request* zaidi, tumefaidika lakini sina *figure* ya uhakika labda baadae tutashirikiana na Mhe. Waziri wa Fedha tunaweza kumpatia maelezo zaidi ya fedha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee.

Kifungu 0601

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia idara hii kwenye ushirikiano wa Kimataifa nilizungumzia zaidi kuridhia itifaki mbali mbali ikiwemo sarafu moja. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu ameonesha kwamba masuala haya ya itifaki yatamalizika pale baada ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo tunategemea kuishughulikia wakati wowote. Lakini mimi wasi wasi ni kwamba itifaki ya sarafu moja itatekelezwa mwaka 2013, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaanza mwaka 2014 au 2015 itakuwa tayari itifaki imetekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikahoji nini nafasi yetu kwa Zanzibar kwenye Bodi ya Sarafu Moja wakati hivi sasa BoT Maafisa wako 80 Zanzibar ni mmoja tu. Mhe. Mwenyekiti, hili sikupata jibu naomba Mhe. Waziri anisaidie kwa hili nafasi yetu kwa Bodi ya Sarafu ya East Afrika nafasi ya Zanzibar itakuwa ni ipi, wasi wasi ni kwamba Bodi itakuwa imeanzishwa, Katiba haijatoa majibu na itakuwa Wazanzibari wametengwa kwenye sarafu moja kama chombo muhimu cha uchumi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hija ni kweli alipochangia aliuliza hili suala. Lakini Mhe. Hija namuomba tukumbuke kwamba sasa tunatumia sarafu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi tuki-*request* sarafu nyengine sasa hivi lazima tuzame na upande mwengine hivyo mambo siju yatakuwaje. Kwa hivyo, kama tutataka tutumie sarafu nyengine basi hilo tulilete ili tuzungumze kwenye taratibu zetu tuone vipi tunaweza tukalipeleka. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa sasa hili nafikiri sio wakati muafaka sasa hivi sote tuko Tanzania na sarafu yetu na tunazungumza na wenzetu wa Jumuiya ya Kikanda.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Waziri hakunifahamu sizungumzii haja ya kuwa na sarafu yetu peke yetu, nazungumzia Bodi kama chombo ambacho kinasimamia uchumi, hivi sasa Bodi ya Sarafu Tanzania iko chini ya BoT ambayo BoT wajumbe 80 Zanzibar kuna Mjumbe mmoja. Je, wakati huu wa sarafu moja ya nchi tano Zanzibar itawakilishwa vipi wakati Bodi ya Sarafu itakuwa ni moja kwa nchi tano hivi nafasi ya Zanzibar ni ipi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nikizungumzia Bodi ya Sarafu ambayo inasimamiwa na Benki Kuu basi ile Bodi ya Benki Kuu na Wajumbe wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamo na tuna haki ya kukataa na kukubali mambo kwa niaba ya serikali yetu. Kwa hivyo, tuna uwakilishi mzuri tukichukulia *propotional wise* anavyozungumza yeye kwa nchi tano iko hivi je nchi kubwa itakuwaje. Hilo nafikiri linazungumzika lakini kama nilivyosema kwenye majumuisho yetu kwamba Zanzibar bado tuna sauti kwenye Tanzania yenyewe, tuna sauti hata kwenye Jumuiya kama jambo linalihusu Zanzibar wanasema hatulitaki basi halipitishwi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi si mwana uchumi, lakini kwa kadiri ya ushamba wangu wa uchumi siamini kwamba nchi tano zitatuwakilisha vizuri kwenye Bodi hii ya pamoja. Lakini kwa sababu Mhe. Waziri na serikali ina amini hivyo na Wazanzibari wanasikia basi tuendelee.

Kifungu 0601	Uratibu wa Uchumi na Ushirikiano wa Kimataifa	671,000,000
	Jumla ya Fungu	**671,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 08 – OFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu 0501	Baraza la Mapinduzi	838,808,000

FUNGU 10 – OFISI YA RAIS IKULU

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	365,467,000
Kifungu 0401		

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kuhusiana na ugawanaji wa rasilimali za idara mbali mbali katika wizara hii ikiongozwa na hii Idara ya Mipango na Sera kama tulivyokubaliana, nilisema kwamba kifungu cha Zima Moto ni kidogo ukilinganisha hata na fungu linalopewa Kikosi cha Valantia Zanzibar. Lakini Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alionesha kuipenda tu hiyo Idara ya Zima Moto, lakini hakuonesha dalili kwamba imepunjwa na atafanya jitihada hebu atueleze hasa wazi wazi amekusudia nini kuipenda. Mhe. Mwenyekiti, maana kumpenda mtu ni kumpa unachokipenda na wewe, lakini yeye anaipenda kwa maneno tu hebu tueleze anaipenda vipi hii idara.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana kwa maelezo mazuri ya Mhe. Rashid Seif Suleiman nataka kusema kwamba Kikosi cha Zima Moto tutaendelea kukitizama kwa jicho la huruma ili mambo yake yaende vizuri kwa manufaa ya nchi yetu na maeneo yetu. Kama ninavyompenda yeye rafiki yangu basi nitakipenda kikosi hicho.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuamini sana Mhe. Waziri lakini sijui niseme hii ni mara ya mwisho kumuaminiau vipi. Labda tuiambie na serikali kwamba kuungua kwa nyumba ni mtaji watu wanapata viwanja vya kujenga wengine. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimwambia Mhe. Waziri anipe maelezo kuhusu Ikulu ya Micheweni Pemba kwa bahati nzuri amesema tu kama hatukuisahau Ikulu ya Pemba, bali ilioko Micheweni tutaifanyia matengenezo lakini hakuniambia muda gani na wakati bajeti ya serikali ndio inapitishwa mwaka huu. Kwa hivyo, nataka anieleze vizuri ili nijue kama lile jengo sasa litamalizwa na lianze kufanya kazi, mimi anijuilishe tu baada ya kupitishwa bajeti hii litajengwa kwa mtaji gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Subeit ni kweli

alipochangia alionesha nia yake kwa jengo lile na namuahidi kwamba tutalishughulikia kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, wajua mimi Mhe. Waziri namuheshimu sana kwani rafiki yangu kwa hiyo nilitaka akishatoa maelezo hapa ndio tayari ameshajifunga. Kwa hivyo, nataka anipe ule usahihi kwa sababu wote wa Pemba na Waunguja wanasikia kwa ujumla. Kwa hivyo, mimi nataka anipe ule usahihi tu kama hili jengo Mwenyezi Mungu akijaalia mwezi fulani tunaanza kulishughulikia.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru tena Mhe. Subeit nasema kwamba tutalitengeneza ndani ya mwaka wa fedha ujao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa ameshalicheleweshа lakini inshaallah nampa fursa huo mwaka wa fedha hauko mbali, nimeisikia ahadi yake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyengine tena na hapa pia nataka niseme namshukuru sana pia Mhe. Waziri kwa marekebisho aliyoyafanya katika vitabu hivi kwani vimetusaidia sana kuondosha ule utatanishi ambao ulikuwepo. Mhe. Mwenyekiti, suala langu ni katika masuala ya fedha ni kuwa katika mchango wangu nilizungumzia mambo mawili. Moja lilikuwa ni suala la ruzuku inayokwenda Baraza la Manispaa na tukasema kwamba ukiilinganisha ruzuku na makusanyo takriban yanalingana, nikahoji kwamba ikiwa hali ni hii hivi kuna haja hasa ya kutoa ruzuku kwa Baraza la Manispaa.

Kwa hivyo, mimi niseme nimeikamatia hapa kwenye fedha kwa sababu tumeambiwa hapa ndio kuna masuala ya kifedha tuulizie hapa. Nimelipekua sana hili buku sijaona popote hiki kifungu cha Baraza la Manispaa kupewa ruzuku, labda atatusaidia yeye. Mhe. Mwenyekiti, suala langu la kifedha linakuja hilo kwamba katika kuidhinisha mapato ikiwa wao wanakusanya bilioni moja na wanachoombwa ruzuku ni pesa hizo hizo bilioni moja. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika maelezo yake ametwambia kwamba hizi zinakwenda zaidi katika mishahara nilikuwa nataka kujua hizi nyengine ambazo zinakusanywa na Baraza la Manispaa huwa zinafanya shughuli gani ikiwa za ruzuku zote zinakwenda katika mishahara.

Pili, nilizungumzia hapo hapo suala la huu mradi wa *ZUSP* na nikasema kwamba nikitizama maelezo ya Mhe. Waziri yaliyokuwemo katika kitabu chake ukurasa wa 45-46 yanatafautiana katika baadhi ya *component* na yale ambayo Mhe. Waziri wa Fedha aliyataja katika kitabu chake cha bajeti ukurasa

wa 61-62. Kwa hivyo, amesema kwamba unakwenda kwa awamu, haidhuru katika ile hotuba ya bajeti ya serikali haikusema hivyo ilizungumza kwa jumla tu hayo maeneo, mimi nilitaka anihakikishie tu kwamba katika haya maeneo ambayo yametajwa kwanza katika kitabu cha hotuba ya Waziri wa Fedha yalitajwa maeneo ya Mji Mkongwe ikiwemo Kiponda, Vuga, Malindi na Shangani. Lakini katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais ametaja maeneo ya Kiponda na Shangani. Mimi nataka anihakikishie kwamba haya maeneo yote manne yaliyotajwa hapa yamo katika mradi bado.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika component hiyo hiyo bado kuna suala zima lile ujenzi wa utanuzi wa ukuta wa Forodhani ili kuweza kutumika kwa waendao kwa miguu kutoka Msikiti wa Ijumaa Malindi hadi bustani ya Forodhani wenye urefu wa mita 340. Kwa hivyo, haya sikuyasikia kama yamo katika programu hii ni ya miaka mingapi na kama inaanza katika mwaka huu wa fedha pia anieleze. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba maelezo ya mambo hayo mawili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Jussa kwa uchambuzi wake. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema unajua huu mradi ni mkubwa na hizi *activities* zimekwenda kwa mujibu wa *life circle* ya mradi. Kwa hivyo, hazitokwenda kwa mpigo zote, na kama mradi wa taa hiyo mitaa iliyotajwa ya Mji Mkongwe huko lazima tuanze huko kwanza baadae tunakwenda na Ng'ambu lakini mji wetu wote tunataka ung'are cha kusisitiza ni kwamba tunakwenda kwa awamu.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusisitiza ni kwamba wenzetu hawa wa Wizara ya Fedha wao ndio wenye maandiko ya mradi sisi tumeshirikiana kuundaa, lakini wao ndio watakaosimamia huu mradi kifedha na mpaka *plan work* na kuna pesa nzuri tu zimetengwa zaidi ya bilioni tatu za kusimamia mradi. Mhe. Mwenyekiti, hayo yote tunakwenda nayo na sisi ndio watekelezaji, kwa hiyo sisi tuliotamka ni yetu ya mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu fedha wanazokusanya kwanza nashukuru serikali inatupatia ruzuku kwa sababu ya mishahara na kulipa *income tax* na kodi nyengine. Kwa kweli kama sio hivyo tusinge-*survive* na hiyo zaidi imetokana kwamba vile vianzio vyetu vikuu vimechukuliwa na serikali. Hiyo ni kwa sababu tulikuwa wazembe lazima tukubali, makusanyo waliyokuwa wanakusanya Manispaa ni madogo wenzetu wa ZRB makusanyo yale yale wanayakusanya vizuri na wanayatunza vizuri na imesaidia sana kwenye *revenue* ya serikali. Kwa hivyo, yale mengi nafikiri yanakwenda kwenye *revenue* ya serikali na sisi tukitaka kama kuomba kuna mambo fulani tunazungumza na Wizara ya Fedha basi yanatekelezwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na maelezo hayo naomba tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	240,000,000
Kifungu 0701	Huduma za Rais Unguja	520,000,000
Kifungu 0801	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	200,000,000
Kifungu 0901		

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilitoa malalamiko jinsi vikosi vyetu vya Zanzibar nikalalamika kuwa huwa wanatuondolea heshima na nikatoa mfano wa mimi mwenyewe niliposhikwa ukosi. Lakini Mhe. Waziri amezungumza kama mimi nahitaji suluti, hivyo naomba niweke sawa kama mimi sihitaji suluti heshima sio suluti tu kuna aina nyingi za kuheshimiwa. Kwa hivyo, mimi ninapoondolewa heshima leo kesho ataondolewa heshima mwenzangu, hivyo kwa kuweka sawa mimi sihitaji suluti nahitaji tuheshimiwa heshimiwa ziko za aina nyingi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana rafiki yangu Mhe. Subeit kwa kweli niseme mwisho nilirekebisha nafikiri kama alinisikia nilisema ile suluti limetokezea tu lile neno, lakini hasa nikasisitiza ni heshima kwamba sote tunastahili heshima ndani ya Baraza hili pamoja na yeye, nikamtania kidogo nikamwambia wakati mwengine huwa unapiga suti na wakati mwengine hupigi huwa hawakutambui. Lakini kwa kweli nasisitiza kuwa tutawaelekeza wapiganaji wetu wote na tutawapelekea picha za waheshimiwa na tutawaambia haya suala hili, mimi nakubaliana na wewe mheshimiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, alipokuwa akitoa majumuisho yake Mhe. Waziri kuna suala moja la askari mmoja nilimtaja walifukuzwa hilo namuomba Mhe. Waziri kama amepitikiwa naomba kidogo anijibu ili nipate kujua kwa sababu huyo ni kijana wangu aone kama mimi namtimizia wajibu wake katika kumtetea haki yake.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mhe. Mshimba alipochangia alielezea kufukuzwa kazi kinyemela nakumbuka alitumia neno hilo hilo hasa kuwa kijana huyo amefukuzwa kazi. Kwa hivyo, kwa bahati mbaya hatukupata zile *particular* zake na unajua tena ukiwa na majumuisho kidogo unakuwa na pirika sikuwahi kumfuata kupata maelezo zaidi. Kwa hivyo, nitamuomba Mhe. Mshimba baadae atupe *particular* zake halafu tutalifuatilia kwa undani kabisa na hili naomba tuwe pamoja ili tulimalize.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia sehemu hii nilichangia kuhusu kikosi maalum cha kuzuia magendo na nashukuru Mhe. Waziri kanipa faraja kwa kunambia kuwa tushirikiane katika kuzuia magendo, lakini sivyo nilivyochangia. Nilisema kuwa karafuu nyingi huwa zinakamatwa za magendo na wakamataji huwa wanaziuza hizi karafuu, lakini sijui ni kiasi gani cha fedha kinarudi serikalini. Hivyo kwa kuwa hii ndio wizara yake nilitaka kujua kuwa ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana kwa karafuu zilizokamatwa angalau msimu huu uliopita.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Salim ni kweli alipochangia alizungumza hili suala na ukweli kwamba sina hasa hesabu kamili ya hizo pesa zilizorudi serikalini, lakini ninachotaka kusema kwamba tulionesha kwenye hotuba yetu kiwango cha karafuu zilizokamatwa na zile moja kwa moja zinachukuliwa na shirika. Lakini kuna utaratibu maalum ambao umekuwa ukitumika wa wale wanaosaidiana kukamatwa karafuu zile na mheshimiwa mwenyewe nafikiri analifahamu utaratibu huo unaotumika na namuomba tusaidiane kama nilivyosema tukomeshe haya mambo yasiendelee kwani yamepitwa na wakati sasa hivi tuko kitu kimoja zaidi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, sijui kuwa hili ndio jibu sahihi mimi nimeuliza idadi ya fedha zilizokwenda serikalini mbali zilizokwenda katika sehemu nyengine lakini sikupata jibu sahihi. Lakini kwa sababu halipo basi naomba tuendelee.

Kifungu 0901	Idara ya Uratibu Idara Maalum ya SMZ	145,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1,858,463,000
Kifungu 1601	Kitengo cha Ofisi ya Usalama wa SMZ	49,858,000
Kifungu 1801	Kitengo cha Mawasiliano na Habari	80,690,000
	Jumla ya Fungu	**3,459,478,000**

FUNGU 17 – JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu 0201	Utawala Unguja	4,668,000,000
	Jumla ya Fungu	**4,668,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda uliobaki hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu ya kupitisha vifungu vya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hivyo naomba Baraza lako liridhie kutengue kanuni ya muda ili tuweze kukamilisha kazi iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubali kuongeza muda wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

FUNGU 18 – CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu 0201	Utawala Unguja	3,938,000,000
Jumla ya Fungu:		**3,938,000,000/-**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 29 – KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Kifungu 0201	Utawala	6,687,000,000
Jumla ya Fungu:		**6,687,000,000/-**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 32 – KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa umakini wako na kumbe kazi unaiweza. Mhe. Mwenyekiti, nilipozungumzia ndugu zangu wa Zimamoto nilimuomba Mhe. Waziri kwamba, kwa vile kikosi hiki kinafanya kazi kubwa ya kuokoa wananchi basi waongezewe mafunzo. Na nikasema kwamba kuna wasi wasi kuwa vitendea kazi wanavyopewa hata magari hayana kiwango. Sasa Mhe. Waziri naomba anitosheleze, wana magari mangapi na

mangapi yana kiwango kwa mujibu wa kazi yao. Kwa sababu nilihoji kwamba ziko taarifa kuwa kuna magari hata *tank* za maji hayana. Sasa naomba anitoe wasi wasi katika hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Hija Hassan, ukweli kwamba magari si mengi lakini yanakidhi haja. Tunajitahidi sana hivyo hivyo tunaomba na tunaingiza pesa zetu tunayanunua. Tatizo labda ni kwamba magari yako mbali ya sehemu ya matukio, ndio nikasema tunafanya jitihada sasa kusogeza huduma karibu na wilaya, tunataka kila wilaya pawe na gari.

Hilo Mhe. Mwenyekiti, tunajitahidi tutashirikiana na Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa tuwe na huduma za karibu zaidi ili ikitokea ajali ya moto tuwe tunaharakisha hataka, lakini kwa vifaa kidogo si wabaya na nafikiri hata katika kitabu cha bajeti tumeona mambo tuliyoyafanya na mali tulizookoa. Tunajitahidi upande huo na nilizungumza mpaka bandarini tumeshapata *site* tunajenga na kituo, halikadhalika tunakwenda na Mkoani vile vile na Wete pamoja na Chake Chake. Kwa hivyo tutajitahidi Mhe. Hija ku-*improve* huduma zetu na hivyo vifaa alivyosema vyengine tutajitahidi kufanya kazi kwa karibu zaidi. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri na ningemshauri kwamba kati ya Zimamoto ni kazi ya kitaalamu. Kwa hivyo, baada ya kupokea ripoti kwa maandishi ningemshauri akakaanao ili wakasikiliza mahitaji yao ili ufanisi wao uweze kuendelea. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia kifungu, lakini naomba nipate ufafanuzi na mimi kidogo. Kwa sababu nilipochangia sehemu hii ya Zimamoto nilitamka kuwa naionea huruma sana idara hii haina baba wala mama, na nikazungumza kuhusu habari ya usafiri kama alivyozungumza mwenzangu. Sasa Mhe. Waziri ametupa maelekezo hapa. Je, magari haya yakiwa wilayani yatakuwa na ma-*tank* ya maji au ni magari ya kupiga mbio tu kwa kila wilaya? Kwa sababu Zimamoto madhumuni hasa ni kuwa na magari ambayo yana ma-*tank* ya maji ya kuzimia moto, sasa naomba ufafanuzi hapa, magari haya yatapelekwa kila wilaya kwa kuwa wakisikia kumeungua sehemu wapige mbio au magari haya yatakuwa na ma-*tank* japo kama yale ya mafuta tu angalau tuwe na kitu ambacho kinaweza kutusaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana dada yangu Mhe. Asha Bakari kwa ushauri wake mzuri kwamba haya magari lazima yawe kamili, nakusudia lazima yawe na maji ni silaha moja wapo kwa moto kwa tulivyozowea, bila ya maji yatakuwa

hayana maana. Naomba niungane naye kwamba tunajua tuna matatizo ya maji baadhi ya sehemu au sehemu nyingi kabisa na hilo serikali inaliendea mbio italirekebisha, lakini bado ziko sehemu magari haya yanapata nafasi yanakwenda yanajaza maji.

Lakini pia nataka kusema kwamba ikiwa gari lipo halina inakuwa haina maana, imekuwa kama una bunduki unakwenda kulinda haina risasi haina maana. Kwa hivyo, nakubaliana na ushauri wake kwamba tutajitahidi muda wote hayo magari yawe na maji ili kujiweka tayari kwa matukio yote.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,883,000,000
Jumla ya Fungu:		**1,883,000,000/-**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 34 – KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu 0201	Utawala Unguja	2,452,634,000
Jumla ya Fungu:		**2,452,634,000/-**

(Kijifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 37 - MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Kifungu 0401	Mipango na Sera	202,164,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Mjini	310,374,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Magharibi	231,462,000
Jumla ya Fungu:		**744,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juuvkimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 38 – MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	208,807,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Kati Unguja	290,568,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Kusini Unguja	241,625,000
Jumla ya Fungu:		**741,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 39 – MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	194,568,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Kaskazini 'A'	267,686,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Kaskazini 'B'	199,766,000
Kifungu 0701	Wilaya ndogo Tumbatu	47,980,000
Jumla ya Fungu:		**714,000,000/-**

(vijifungu Vilivyotajwa hapo juu Vimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 40 – MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	178,122,000
Kifungu 0402	Baraza la Mji ChakeChake	330,000,000
Kifungu 0403	Baraza la Mji Mkoani	190,000,000
Kifungu 0501	Wilaya ya ChakeChake	256,189,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Mkoani	209,689,000
Jumla ya Fungu:		**1,164,000,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juuvkimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 41 – MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu 0401	Mipango na Sera	193,600,000
Kifungu 0402	Baraza la Mji Wete	250,000,000
Kifungu 0501	Wilaya ya Wete	255,000,000
Kifungu 0601	Wilaya ya Micheweni	215,400,000
Kifungu 0701	Wilaya ya Kojani	36,000,000
Jumla ya Fungu:		**950,000,000/-**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati Bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 33 – OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu 0201	Utawala Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii nyengine. Katika mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, nilihoji juu ya kupanda kukubwa kwa bajeti ya Afisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Tukiangalia eneo la *estimate* utakuta sehemu kubwa iko katika utawala Unguja. Nilisema

kwamba, kwa mwaka uliopita palikuwa pana shilingi 910,000,000/- lakini mwaka huu imefika shilingi 1,248,000,000/-.

Katika majibu yake Mhe. Waziri alisema kwamba hiyo inatokana na kuhamishwa fungu la kazi za maendeleo kuwa zimepungua sana, kwa hivyo kutegemea kwamba shughuli zake zitafanywa kupitia bajeti hii ya shughuli za kawaida. Lakini nilipokuwa nikisubiri kwa hamu yale maelezo niliyoyaomba kwamba inafanya shughuli gani? Mhe. Waziri alikuwa kajibu kuwa kuna kazi nyingi zanini na nini, sasa ile zanini sikuipata hivyo naomba maelezo ili niongezee.

Ninapoangalia vifungu tuangalie kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 600 juu kwenye kasma 220500, Vifaa na Huduma za Ofisi. Unaona kuna kupanda kwa kazi kubwa sana kwa matumizi ukilinganisha na mwaka uliopita. Sasa kama nilivyosema katika mchango wangu ukilinganisha shughuli ambazo zinafanyika mwaka huu haziwezi kulinganishwa na shughuli zilizofanyika katika miaka iliyopita wakati idara ilikuwa inaanza kazi na ilikuwa inafanya kazi kubwa sana ya kuwasajili kwa wingi wale tuliopo. Sasa usajili wa sasa hivi ni wa ku-*up date* tu. Sasa naomba nitoe mifano Mhe. Mwenyekiti, nieleweke hoja yangu.

Vifaa vya kuandikia vimeshuka kutoka shilingi milioni tano mpaka milioni kumi kweli voti hiyo, lakini vifaa vya kompyuta kutoka shilingi milioni 15 mpaka 55 milioni, ufukizaji kutoka shilingi milioni nne mpaka milioni kumi, utoaji na usafirishaji wa mizigo shilingi milioni tatu mpaka nane. Kwa hivyo, katika fungu hilo Mhe. Mwenyekiti, utaona kuna kupanda sana.

Lakini pia fungu jengine ambalo limenitisha katika hiyo hiyo sehemu ya utawala Unguja ni kasma 200800 Matengenezo ya Zana. Katika fungu hili mwanzo kumetoka shilingi milioni kumi mwaka uliopita hadi 65 milioni mwaka huu; inayofuata ununuzi wa *spare* na zana kutoka shilingi 11 milioni hadi 160 milioni mwaka huu.

Lakini pia nikiangalia kasma 263100 Ruzuku kwenye ushauri nasaha kwenye UKIMWI, ofisi hii sijui ina maambukizi makubwa kwa sababu imetoka shilingi milioni mbili hadi 12 milioni mwaka huu. Sasa nikitizama na Pemba kwa mfano, nikilinganisha tu katika ushauri nasaha zilikuwa shilingi milioni mbili mwaka jana mwaka huu zimebakia hizo hizo shilingi milioni mbili, lakini hapa zimeongezeka kutoka shilingi milioni mbili hadi 12 milioni, napata wasi wasi kidogo.

Nimalizie katika mifano yangu katika ukurasa wa 601 Ununuzi wa Mashine na Zana, fungu 311200 kwenye kifungu kidogo 311207 ununuzi wa kompyuta. Hii

imeongezeka kutoka shilingi milioni tisa mwaka jana hadi shilingi 50 milioni mwaka huu. Sasa ndio maana nikasema Mhe. Mwenyekiti, tunapoyaangalia haya hasa ukilinganisha na shughuli zenyewe za idara kwa mwaka huu ukilinganisha na mwaka uliopita naomba tupewe maelezo ya hili fungu kuongezeka pamoja na maelezo ya waziri kwamba fungu la maendeleo limepungua. Lakini hili la utawala Mhe. Mwenyekiti, linatupa wasi wana na naomba maelezo ili niruhusu fungu hili liweze kuendelea kutumika.

Mhe. Waziri wa Nch (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Ismail Jussa kwa uchambuzi wake mkubwa kabisa. Nataka kusema na nafikiri tulizungumza kwamba ofisi zetu sasa zinatanua kazi zake kwenye wilaya zote kumi. Katika kutanua huko kunahitajika matengenezo ya ofisi kule, kunahtiajika kununua zana na hizi ni zaidi ya kompyuta kuna *serves* wenyewe wanasema mimi hata sizijui kompyuta maalum hizo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna vifaa vya kisasa kabisa ambavyo vimemaliza muda wake wa matumizi ya miaka mitano, kuna *special equipments* miaka mitano vimemaliza unatupa, unajua mambo ya *electronic* haya vimeshapitwa na wakati, kwa hvyo lazima upate vyengine. Kuna ma chemicals yake, kuna na vitu vingi kabisa. Nafikiri sio siri yeye Mhe. Mwakilishi na ni mtaalamu haya mambo ya kompyuta anayajua na hasa hii *language* ya vitambulisho.

Pia kuna kazi bado ya kubadilisha vitambulisho kuwapa watu vingi vingine zaidi. Kwa hivyo, ile *volume* ya kazi imetanuka ndio maana mahitajio ya fedha nayo yakazidi. Hiyo ndio sababu kubwa kabisa. Nashukuru kuwa mwenyewe kakiri kuwa mwengine mmeoneshwa wazi. Kwa hivyo, tumetanuka sasa tunakwenda wilayani *in full swing* na waheshimiwa wamezungumza vizuri kwamba kuna usumbufu, sasa tunataka tuondoshe hayo mambo yote kabisa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo yake Mhe. Waziri. Kwanza haya ya *serves* sikuyahoji kwa sababu yana fungu lake, nalo pia limepanuka lakini nikasema kwa sababu ya mahitaji haya inawezekana yakaingia akilini, lakini haya niliyoyahoji yalikuwa ni vifaa vyenyewe. Lakini sasa naomba nikubaliane na waziri kwa maelewano mamoja, kwamba tutapokuja kuletewa baadae *Inshaallah* mwakani hapa tupewe *break down* ya vitu hivi tujue hasa fedha hizi zimetumika vipi kuliko haya maelezo ya jumla jumla ambayo yanakuwemo katika vitabu vyetu vya bajeti.

Sikusudii katika hapa, lakini suala langu lililobakia niliuliza pia *kasma* 263100 Ruzuku ya Ushauri Nasaha *HIV* nataka kuuliza pia UKIMWI umetanuka katika

ofisi hii kiasi cha kutoka shilingi milioni mbili mpaka 12 milioni wakati Pemba imebakia vile vile.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, unajua unapofanya ushauri nasaha ni zaidi semina, watu kupimwa kwa hiari nayo kidogo inataka kuwaelimisha watu. Halafu kama nilivyosema wakati ule tulijikita zaidi kwenye makao makuu Unguja na Pemba, sasa tunakwenda kiwilaya, zaidi shughuli zimetanuka kiwilaya. Nataka Mhe. Jussa anifahamu hivyo, unajua unapotoka kiwilaya gharama zinazidi. Kwa hivyo, naomba anifahamu hivyo kwamba hizi shughuli nazo zinatanuka ndio nia yetu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Waziri katika hilo, namuona sana kaka yangu, katika hili niruhusu tusiendelee kukwama kwa hoja moja tu au kwa makubaliano mamoja, kwamba hili fungu atalifuatilia yeye binafsi. Kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti? maelezo yake anasema kwamba kwa sababu tunakwenda katika Mawilaya lakini nimetoa mfano Wilaya haziko Unguja tu pia Pemba ziko.

Lakini ninapokwenda katika utawala Pemba fungu la ushauri nasaha kwenye ukimwi ilikuwa milioni mbili mwaka jana zimebakia milioni mbili mwaka huu. Kwa hivyo, hapa tu Unguja zimetoka kutoka milioni mbili mpaka milioni kumi na mbili. Kwa hivyo, kwa maelezo haya kwamba tunakwenda katika Wilaya nilitegemea hata Pemba pia lingetanuka. Hivyo nasema ili tusiendeleze mjadala nakubali kwamba tuipitishe bajeti hii, lakini alifuatilie binafsi ili tuje kupata malezo ya milioni kumi na mbili hizi kuhusu idara hii katika mambo ya ukimwi. Ahsante sana.

Kifungu 0201 Utawala Unguja

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi namshukuru Mhe. Waziri alipokuwa akijibu amesema kama watatatua matatizo kuhusu suala hili la vitambulisho, lakini nilimueleza kuhusu wazee wetu ambao wameshafikia umri zaidi ya miaka 60 na wazee hao wanapokwenda kule tunakuwa tunawapa usumbufu. Pia Mhe. Mwenyekiti, nilimwambia Mhe. Waziri kuwa wazee wana fungu lao la heshima na wakifika wanaambiwa wakachukue *affidavit* Mahakamani, huwa wanakwenda wanachukua lakini mimi nishahidi kwa sababu nilimpeleka mzee wangu na ikakataliwa.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri atwambie watendaji wake ambao kuwa watakuwa wanakataa kufuata sheria kwa sababu sheria inasema wazee akifika umri zaidi ya miaka 40 basi huyo sio lazima ende na cheti cha kuzaliwa. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimekwenda na mzee wangu binafsi tena mzee wenyewe zaidi ya 60 na *affidavit* akenda nayo na hakupewa. Kwa hivyo, atwambie hapa

kwani Wazanzibari wote wanasikia mtendaji atakayekuwa kaitengua sheria kama hii afanywe nini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, namkubalia Mhe. Subeit kwamba matatizo kwenye utendaji yapo na yanatokezea sasa anavyozungumza kwamba haya mambo yanatokezea basi mimi naona yakitokezea kama watendaji pale wamekataa basi atuarifu, kwani kuna Mkuu wa Wilaya, kuna Mkuu wa Mkoa, kuna Waziri hivyo atuarifu tutaingilia kati tuyamalize. Mhe. Mwenyekiti, mambo kama hayo yasimalize zoezi zima kwani hayo ni matatizo ya kiutendaji tu hivyo namuomba sana na sio mengi hivyo yakitokezea kama hayo basi tuwasiliane tutaingilia kati tuyamalize.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, unajua matatizo kama hayo nafsi huko Wilayani nako yanachangiwa, mimi nilitaka kwa sababu Wazanzibari wanasikia na yeye ni Waziri anayeongoza hii wizara nilitaka mimi atoe tamko la kwamba wazee kama hawa wenye umri zaidi ya miaka 60 wakifika wasiteswe. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka hilo Wazanzibari wote walisikie na endapo mtu atavunja sheria basi ashtakiwe.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kimsingi kama nilivyosema matatizo kwenye utendaji yapo, sasa kutoa tamko halafu hatujui hao wazee wanaokwenda pale wengine labda siku hazikutimia kwa sababu yule ofisa nae ana dhamana. Kwa hivyo, tusimdharau yule ofisa lazima ana *quiry* pengine ana sababu za msingi. Sasa namuomba sana Mhe. Subeit Khamis Faki ikitokezea tuambizane na sisi tutaingia wakubwa, lakini tusitoe tamko tu ghafla kwamba waachiwe tu waende itakuwa sivyo hivyo. Ninachosema kwamba taratibu zifuatwe limetokea tatizo tuitane tutalimaliza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli karani kama na yeye anaangalia hoja zake za msingi. Lakini sheha ameshampa barua, kishamtaka aende akachukue affidavit Mahakamani kishakwenda kuchukua kishakuja nayo tena karani ana tatizo gani hapo na hayo masharti kayatoa yeye. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri asiogope kutoa kauli kwa sababu atakuwa anawalinda na anawapa nguvu, kwa hivyo atamke Wazanzibari wamsikie.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nadhani aliyetimiza masharti hatobughudhiwa, kwa hiyo tunakuomba Mhe. Mwakilishi tuendelee, waheshimiwa wenzako wapo na umesema waziri yupo na yeye yuko tayari kukusaidia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, wapo watu na kwa ushahidi sisemi tu hivyo mimi kwa kiburi. Nakwambia mimi nina mama yangu binafsi

mkwe wangu niliyemuolea mtoto wake na tumekwenda na cheti tumeshakwenda kuchukua si kwamba nasema tu mimi. Nasema kwa ushahidi kamili na katimiza masharti yote ni mtu anayejulikana, ni mke wa Marehemu Mzee Issa Kombo walio wengi humu wanamjua, nakwenda nae na amekwenda kuchukua *affidavit* na kakoseshwa.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Waziri nadhani ungesema aliyekuwa katimiza masharti asibughudhiwe basi imetosha.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka atoe tamko tu watu wasikie wote.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, natamka sana wasikie wote kama alivyoshauri Mhe. Subeit Khamis Faki. Kwamba yeyote ambaye hana matatizo hatobughudhiwa na ambaye ana matatizo mkuu wa kituo kakwama atuite viongozi wa juu tutalimaliza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Waziri anatuongezea matatizo tutoke Pemba tuje tumtafute Unguja. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tatizo limetokea Micheweni Pemba mimi nije nimtafute Mhe. Waziri Unguja heee. Mhe. Mwenyekiti, sasa namuuliza Mhe. Waziri anaona tatizo la nini yeye kutamka watu wakasikia kama sasa sheria inataka kufuatwa. Kwani anaona tabu ya nini, ni jambo dogo tu hili atoe tamko watu wote wasikie kama sasa sheria ni hivi inavyofuatwa basi, kuna tatizo gani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, natoa tamko mtu yeyote ambaye amekwenda kusajiliwa kenda na vitambulisho vyote sheha kampitisha hakuna tatizo basi atamalizwa, mwenye tatizo natoa tamko kwamba aende kwa viongozi. Kuna Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa, Waziri watakwamua hakuna tatizo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, tamko lililotolewa ni sawa na mtu yeyote aliyekuwa hana matatizo. Mimi nazungumza suala la wazee wetu ambao ni wazee wenye heshima ya wazee. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,094,500,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	153,500,000
Jumla ya Fungu		**1,248,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 10 - Ofisi ya Rais Ikulu

Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	550,000,000
Jumla ya Fungu		**550,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 17 - Jeshi la Kujenga Uchumi

Kifungu 0201	Utawala Unguja	450,000,000
Jumla ya Fungu		**450,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 18 - Chuo cha Mafunzo

Kifungu 0201	Utawala Unguja	400,000,000
Jumla ya Fungu		**400,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 29 - Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo

Kifungu 0201	Utawala	200,000,000
Jumla ya Fungu		**200,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 34 - Kikosi cha Valantia

Kifungu 0201	Utawala Unguja	100,000,000
Jumla ya Fungu		**100,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 38 - Mkoa wa Kusini Unguja

Kifungu 0201	Utawala Unguja	20,000,000
Jumla ya Fungu		**20,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 39 - Mkoa wa Kaskazini Unguja

Kifungu 0401	Mipango na Sera	60,000,000
Jumla ya Fungu		**60,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 43 - Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho

Kifungu 0201	Utawala Unguja	150,000,000
Jumla ya Fungu		**150,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubali makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wanyooshe mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe tunawashukuru kwa kazi tuliyoifanya lakini kabla sijaahirisha kuna tangazo nimeletewa na Mnadhim wa chama cha CUF kwamba wajumbe wake wote tukimaliza kuahirisha kikao hapa wabakie pana maelezo muhimu.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 7:37 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOTUBA YA BAJETI YA OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema na kuweza kufika hapa kuendelea na shughuli yetu hii muhimu kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hekima, busara, uadilifu, atupe muelekeo mwema na mashirikiano zaidi ili tuweze kufanikisha majukumu yetu kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba sasa nitumie nafasi hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kushinda Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba mwaka 2010 kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), na kupata fursa ya kuzitekeleza sera za CCM katika kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

Aidha, naomba nimpongeze kwa kuwa Rais wa kwanza wa Zanzibar chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ushindi alioupata umedhihirisha kukubalika kwake kwa wananchi walio wengi wa Zanzibar na uwezo mkubwa alionao katika kujenga umoja na mshikamano. Katika kipindi kifupi cha uongozi wake imedhihirika kwamba anao uwezo wa kuleta maendeleo makubwa kwa haraka na kuilinda amani tuliyonayo na kudumisha utulivu nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumjaalia afya njema, maarifa na hekima katika uongozi wake ili aendelee kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa

alioupata katika uchaguzi uliopita wa mwaka 2010 na kumuwezesha kuendelea kuiongoza Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa amani na utulivu, na hii inaonyesha jinsi wananchi walivyo na imani kubwa kwake katika kuwaletea maendeleo na kuimarisha uchumi. Tangu kuanzishwa kwa Ofisi yetu tumekuwa na ushirikiano mzuri kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambazo yeye anaziongoza.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza, Makamo wa kwanza wa Rais Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamo wa pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo. Kutokana na nafasi zao wana majukumu makubwa ya kuwatumikia wananchi katika ngazi za juu walizokabidhiwa na ni imani ya wananchi wetu kwamba, wanayamudu vyema majukumu hayo kutokana na umahiri na ukomavu wao katika masuala ya siasa, uongozi na usimamizi wa masuala ya maendeleo ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kukupongeza wewe mwenyewe, kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi,

KUAHIRISHWA BARAZA KABLA YA WAKATI WAKE

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuliahirisha Baraza hili kwa muda mfupi hadi hapo umeme utakaporejea.

(*Saa 10:05 Baraza liliahirishwa kwa muda kutokana na kukatika katika kwa umeme)*

(Saa 10:08 Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumpongeza Mhe. Spika wa Baraza letu tukufu, kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, kwa mara nyengine hii ni kuonekana uwajibikaji na ufanisi wake mkubwa katika kuliongoza vyema Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi zetu kwa viongozi hao wakuu wa Kitaifa, sasa ninapenda kuchukua fursa hii kuipongeza na kuishukuru sana Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Uenyekiti wa Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa jimbo la Mfenesini na Makamu wake Mhe. Panya Ali Abdalla na wajumbe wote kwa ujumla kwa kuteuliwa kwao kuwa katika kamati hii na kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri waliotupatia katika shughuli mbali mbali, hususan wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2011/2012 hatua ambayo, imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bajeti hii katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi yangu inatoa pongezi maalumu kwa Wananchi wote wa Unguja na Pemba kwa kuamua kwa pamoja kuwa na mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Hatua hii inaonyesha kupanuka kwa demokrasia na kuimarika kwa Utawala Bora. Uamuzi wao umepelekea kudumisha zaidi amani na utulivu katika nchi yetu, kukua kwa demokrasia na kuipa sifa kubwa Zanzibar kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba aliyoitoa Mhe. Rais wakati wa uzinduzi wa awamu ya nane ya Baraza la Wawakilishi, ameahidi kuimairisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya Watumishi wa Umma ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi, maandalizi ya miundo bora ya Utumishi wa Umma, kusimamia maadili kwa watumishi katika ngazi mbali mbali na kwamba mkazo zaidi utawekwa katika kuwaelimisha wafanyakazi na wananchi juu ya Sheria za Utumishi wa Umma kwa ujumla, ili kila mmoja ajue wajibu wake.

Pia ameahidi kurejesha nidhamu kazini, uwajibikaji, kuzuia rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, kufanya ukaguzi wa mahesabu ya serikali kwa wakati na kuhakiki orodha ya wafanyakazi ili kubaini kama kuna wafanyakazi hewa. Mambo hayo ni miongoni mwa changamoto iliyopewa Ofisi yetu, kuyasimamia ili kupatikane ufanisi na kuondosha malalamiko ya wananchi juu ya upatikanaji wa huduma bora na kwa wakati.

MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi yetu ina jukumu la kusimamia utendaji wa Watumishi wa Umma ili kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu, ufanisi na kuimarisha Utawala Bora nchini. Katika kutekeleza majukumu hayo, Ofisi itakuwa na kazi ya kusimamia, kudhibiti, kuratibu na kutathmini utekelezaji na uongozaji wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuzingatia misingi ya mipango ya kitaifa kama vile Dira ya 2020, MKUZA, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010 - 2015 pamoja na mikataba na makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufanikisha majukumu yake Ofisi itasimamia vyema Sheria na Kanuni, kufanya mapitio ya Sera, Miongozo na Matoleo mbali mbali ya Kiutumishi na kuandaa sera mpya na miswada ya Sheria itakayoweka mfumo bora wa Utumishi wa umma. Aidha, Ofisi itaandaa mikakati ya kuzuia rushwa, kusimamia maadili ya Viongozi, kuratibu shughuli za haki za binaadamu na kusikiliza malalamiko ya wananchi katika maeneo mbali mbali ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo kamili ya majukumu ya kila Idara yamefafanuliwa katika taarifa za Idara husika.

MUUNDO WA OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeundwa na Idara nane nazo ni: Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu, Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu, Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi, Idara ya Utawala Bora, Idara ya Nyaraka na kumbukumbu za Taifa na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, ofisi inasimamia taasisi tatu ambazo ni; Tume ya Utumishi Serikalini, Chuo cha Utawala wa Umma na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, Ofisi inatarajia kuwa na Taasisi ya Maadili ya Viongozi na Kuzuia Rushwa, Kamisheni ya Utumishi na Idara itakayosimamia mawasiliano ya elektroniki *"e - Government"*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi za Ofisi yangu kwa Viongozi Wakuu na wananchi kwa ujumla na kuelezea majukumu na muundo wa ofisi. Sasa kwa ruhusa yako naomba nifanye mapitio ya utekelezaji wa shughuli za mwaka 2010/2011, Maelezo ya Mpango wa Kazi wa mwaka 2011/2012 na maombi ya fedha za utekelezaji wa mpango huo kwa kila Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kutoa huduma pamoja na uongozi wa Rasilimali Watu katika Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Huduma za uongozi na Utawala wa Rasilimali Watu katika masuala ya ajira, maendeleo ya watumishi, kupandisha vyeo, kufanya tathmini ya Rasilimali watu na Utawala Bora. Kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa na kuweka kumbukumbu za masuala mbalimbali yanayohusu watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara inatoa huduma za manunuzi, uhifadhi wa vifaa, huduma za uhasibu, uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, mapato na matumizi, matayarisho ya ulipaji wa mishahara na uwekaji wa kumbukumbu za pencheni na kiinua mgongo kwa wastaafu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara imefanya manunuzi ya vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi na kugawa vyumba

"Partition", ili kuwapatia nafasi wafanyakazi kwa utekelezaji wa majukumu yao. Katika kuijengea uwezo Ofisi, jumla ya wafanyakazi 28 wenye fani tofauti wameajiriwa katika nafasi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, Idara imepanga kuajiri watendaji wa kutosha na wenye sifa kulingana na mahitaji ya Ofisi, kuweka kumbukumbu za kiutumishi kwa watendaji na kufanya tathmini ya utendaji wa kila mtumishi pamoja na kuandaa ripoti ya hali ya Utumishi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria. Vile vile, Idara itaendelea kutoa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa vya Ofisi, kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi na kupima ufanisi wa utendaji kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 736,847,000/= kati ya hizo Tzs. 525,525,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na Tzs. 211,322,000/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kutoa huduma na utaalamu wa uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti, ufuatiliaji na tathmini ya programu na miradi ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kutayarisha na kuzifanyia mapitio Sera, kufanya tafiti, kuhamasisha wafanyakazi kuhusiana na mapambano dhidi ya Ukimwi, uwiano wa jinsia na walemavu pamoja na kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Ofisi. Vile vile, Idara inajukumu la kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa Zanzibar na kuandaa mbinu za kutafuta rasilimali na misaada mbali mbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara, imezifanyia mapitio sekta za Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetayarisha rasimu ya Mpango Mkakati wa Ofisi wa miaka mitatu (2011-2014) na Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati - MTEF wa Ofisi pamoja na Sera, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Aidha, Idara imetayarisha rasimu ya awali ya Sera ya Usafiri kwa Viongozi, Watendaji Wakuu na Watumishi wengine wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu na Miradi inayosimamiwa na Ofisi, kufanya mapitio ya Mpango wa Matumizi ya Muda wa Kati - MTEF na tathmini ya Mpango kazi wa Mwaka, kukamilisha Sera ya Usafiri kwa Viongozi, Watendaji Wakuu na Watumishi wengine wa Umma, kutayarisha Sera ya mawasiliano ya elektroniki *"e - Government"* na kufanya utafiti wa

namna Watumishi wa Umma watakavyofaidika na huduma za Bima ya Afya. Vile vile, Idara inakusudia kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa wa Ofisi kwa njia ya kompyuta - *"Management Information System".*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 276,033,000/= kati ya hizo Tzs. 203,033,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na Tzs. 73,000,000/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya Idara hii ni kuratibu mafunzo ya muda mrefu, wakati na mfupi kwa Watumishi wote wa Umma wa ngazi mbali mbali ambayo hugharamiwa na Serikali na Washirika wa Maendeleo. Vile vile, Idara inajukumu la kuanzisha na kutoa miongozo na ushauri wa kitaalamu kuhusu maandalizi ya mfumo wa kusimamia mafunzo kwa Watumishi wa Umma katika Wizara na Taasisi za Serikali. Aidha, Idara inajukumu la kusimamia mikataba kati ya Serikali na Waajiriwa wanaokwenda masomoni ili mfanyakazi anaporejea masomoni apangiwe muda wa kuitumikia Serikali baada ya kumaliza masomo yake. Jukumu jengine la Idara hii ni kuandaa na kutunza daftari la taarifa za taaluma za wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya watumishi 83 wamepatiwa mafunzo katika fani mbalimbali, kati ya hao 62 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na 21 ya muda mrefu (kiambatisho nambari 1 kinahusika). Idara imefanikiwa kupata orodha ya vyuo vyote vinavyotambulika na Baraza la Elimu ya Juu na Ufundi - NACTE kwa nia ya kuwataka Maafisa mafunzo kutumia vyuo hivyo kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi wao. Katika kuwajengea uwezo watumishi wa Idara, ziara zenye lengo la kubadilishana utaalamu zimefanyika katika Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dar-es-Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara itaendelea kuratibu mafunzo kwa Watumishi wa Wizara na Taasisi zote za Umma, kuandaa Sera ya mafunzo, kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa umma - *"Trainning Need Assessement"*, ili Wizara na Taasisi ziweze kuratibu mafunzo kutokana na mahitaji sahihi ya Utumishi wa Umma. Idara itaendelea kuwajengea uwezo maafisa mafunzo wa Wizara na Taasisi za Umma kwa kuwapatia mafunzo ya uandaaji wa Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo na Mpango wa Mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 58,887,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kupanga, kuratibu na kusimamia Mipango ya Rasilimali Watu, kuandaa Mpango wa Urithishaji - *"Succession Planning"* na Mipango ya Viongozi katika Wizara na Taasisi za Umma kwa madhumuni ya kukidhi malengo na mahitaji ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu mengine ya Idara hii ni kuchunguza uwezo uliopo wa Rasilimali Watu yaani *"Human Resource Capacity Assessement"* ili kugundua mahitaji ya ziada ya uwezo wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma, kuratibu na kusimamia mpango wa miaka mitano wa Rasilimali Watu na mpango wa mwaka mmoja mmoja utakaotokana na mpango wa miaka mitano, kuweka kumbukumbu za watumishi wa Umma yaani *"Human Resource Database"* na ikama *"Norminal Roll"* za Watumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ilihakiki na kufanya Mapitio ya Makisio ya Mishahara - *"Norminal Roll"* za Wizara na Taasisi za Umma. Maombi ya nafasi mpya 5,265 yaliwasilishwa na jumla ya nafasi 2,476 zimekubaliwa kulingana na mahitaji ya Wizara na Taasisi za Umma na kwa mujibu wa hoja zilizojengwa na taasisi husika. Ili kufanikisha maandalizi ya mahitaji ya wafanyakazi ya baadae, Idara ilifanikisha zoezi la kuweka kumbukumbu za wastaafu ambapo, katika mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya wafanyakazi 533 wanategemewa kustaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara imepanga kuwapatia mafunzo Maafisa Utumishi wa Wizara na Taasisi za Umma juu ya namna bora ya matayarisho ya Makisio ya Mishahara - *Nominal Roll,* kusimamia Mageuzi ya Serikali za Mitaa kuanzisha Utaratibu na Mbinu za Urithishaji wa kazi - *"Job Succession Planning"* ufuatiliaji na utekelezaji wake, kufuatilia uwezo wa Rasilimali Watu ili kugundua mahitaji ya ziada na uwezo wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma, kukusanya na kuweka kumbukumbu na taarifa za msingi za wafanyakazi wa Utumishi wa Umma na kuziingiza katika Mfumo wa Taarifa za Wafanyakazi - *"Human Resource Database"*.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 208,550,800/= kati ya hizo Tzs. 78,985,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na Tzs.129,565,800/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kupitia na kusimamia miundo na mifumo ya Wizara na Taasisi za Umma kwa mujibu wa Sera na Sheria zilizopo ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma. Vile vile, kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kuendeleza na kutunza Orodha ya Malipo ya Mishahara ya Wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara kwa mwaka wa fedha 2010/2011 imeweza kukamilisha Miundo ya Utumishi "*Scheme of Service"* kwa kufanya uchambuzi wa kazi na kupanga madaraja kwa kada zote.

Mhe. Mwenyekiti, katika kujenga uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Idara iliandaa warsha kwa Kamati ya Katiba na Sheria na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili waweze kuipitia na kuichambua kwa ufanisi. Sheria hiyo imejadiliwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi. Vile vile Idara imeendesha Semina kwa Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi na Maafisa Utumishi wote wa Utumishi wa Umma kwa lengo la kujadili majukumu na muelekeo wa utekelezaji wa masuala ya Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inategemea kufanya matayarisho ya kutengeneza mkataba wa kutoa huduma kwa wananchi *"Service Charter"*, kushirikiana na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya Wizara, kuratibu na kushauri kuhusu ajira za Wageni ndani ya Utumishi wa Umma, kuanzisha na kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi *"Performance Management System"* katika Wizara, Idara na Taasisi za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, Idara pia imepanga kufanya mapitio ya kazi na majukumu yanayotekelezwa na Wizara na Taasisi za Umma, kutayarisha Sera ya Mishahara kwa Watumishi wa Umma, kufanya utafiti juu ya masuala ya Mishahara na Maposho, kutoa mafunzo na kufanya ukaguzi wa wafanyakazi na mishahara kwa watendaji wa Idara na kupitia Miundo ya Utumishi wa Umma *"Scheme of Services".*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tzs. 505,699,900/= kati ya hizo Tzs. 61,453,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na Tzs. 444,246,900/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTAWALA BORA:

Mhe. Mwenyekiti, Utawala Bora ulianza mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, ambapo kulianzishwa Wizara ya kuweka Hali za Wananchi Sawa na baadaye kuanzishwa Baraza la Wawakilishi, ili wananchi waweze kuwakilishwa vyema katika kutunga sheria na maamuzi. *(Makofi)*

Katika kuimarisha zaidi Utawala Bora, wakati wa Awamu ya Sita ya Uongozi wa Zanzibar, ilianzishwa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba na Utawala Bora. Halikadhalika na Awamu ya Saba ikaanzishwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa lengo lile lile la kuimarisha Utawala Bora Nchini. *(Makofi)*

Aidha Ilani ya Uchaguzi inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa, Ibara ya 186, imeweka msisitizo wa kusimamia Utawala Bora nchini, kuimarisha Demokrasia, kulinda Haki za Binaadamu, kufuata Sheria pamoja na Kanuni za Sheria hizo na Ibara ya 189 imeweka mfumo wa kufuatwa katika Kuzuia Rushwa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, idara ina jukumu la kujenga na kusimamia utekelezaji wa misingi mbali mbali ya Utawala Bora ikiwa ni pamoja na Sera, Sheria na Kanuni, ili kuhakikisha haki za binaadamu zinalindwa, uwazi, uwajibikaji, maadili ya viongozi, amani na utulivu unaimarishwa. Majukumu mengine ya idara hii ni kutoa elimu ya uraia kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuzingatia misingi ya Utawala Bora katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, idara imetayarisha jumla ya vipindi 9 na kurushwa hewani na Sauti ya Tanzania Zanzibar vikiwa na lengo la kukuza uelewa wa wananchi juu ya dhana nzima ya Utawala Bora, Haki na misingi ya Haki za Binaadamu.

Mhe. Mwenyekiti, idara inakamilisha uundwaji mpya wa Kamati ya Utawala Bora ya Kitaifa na Kamati za Mawizara zitakazosimamia masuala ya Utawala Bora. Kamati ya Kitaifa itakuwa na jukumu la kutoa taarifa za robo mwaka za Utawala Bora zitakazoingizwa katika ripoti ya mwaka ya Utawala Bora Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Rasimu ya Sera ya Utawala Bora pamoja na Mkakati wake zimeandaliwa. Hivi sasa ofisi imo katika hatua za mwisho za kuikamilisha Sera ya Utawala Bora, ambapo Mkakati wa Utawala Bora utafanyiwa kazi baada ya kukamilika sera hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa shughuli za idara ni kupokea malalamiko kutoka kwa taasisi na wananchi mbali mbali. Jumla ya malalamiko tisa yamepokelewa na yamefanyiwa kazi na baadhi yake yameshakamilika na kupatiwa ufumbuzi (kiambatisho nambari 4 kinahusika).

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya majukumu ya idara ni kusimamia misingi ya Haki za Binaadamu hapa nchini. Katika kuimarisha misingi hiyo idara ilitayarisha Muongozo wa Haki za Binaadamu ambao hivi sasa unatumika. Aidha, idara inafanyakazi kwa mashirikiano na Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora.

Katika kukuza mashirikiano yetu na tume hiyo hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya vikao vya mashirikiano na kujuana, ambavyo vimeonesha dalili kubwa ya mafanikio. Tume hiyo ambayo ni chombo cha Muungano imeweka taarifa ya Zanzibar katika sura ya nne ya taarifa ya mwaka 2007/2008.

Mhe. Mwenyekiti, idara katika jitihada za kuwajengea uwezo wafanyakazi wake, imeweza kuwapatia mafunzo tofauti yakiwemo mafunzo ya Uongozi na Upatanishi wa Migogoro kwa kushirikiana na *NGO* ya Kimataifa ya *"Search for Common Ground"*. Mafunzo ya muda mrefu yalihusisha Shahada ya Uzamili ya Sheria na Biashara wakati mafunzo ya muda mfupi yalihusisha Haki za Binaadamu na Uongozi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, idara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuimarisha Utawala Bora, kutoa elimu ya uraia, mafunzo ya Utawala Bora kwa Watendaji Wakuu wa Utumishi wa Umma.

Pia idara inakusudia kuhamasisha na kutoa mafunzo juu ya Utawala Bora na Haki za Binaadamu katika Shehia, Vijiji na Taasisi mbali mbali za Umma, kuandaa kongamano kwa ajili ya kuadhimisha siku ya Haki za Binadamu, kutayarisha na kusambaza ripoti ya mwaka ya Utawala Bora na kutafsiri Muongozo wa Haki za Binaadam kwa kutumia Nukta Nundu kwa Wasioona. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 145,526,000/=. Kati ya hizo shilingi 115,526,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na shilingi 30,000,000/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008. Kabla ya hapo ilikuwa ni kitengo cha Nyaraka katika Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar. Kutokana na muundo mpya wa serikali, taasisi hii imekuwa Idara kamili chini ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina majukumu ya kuhifadhi Nyaraka na Kumbukumbu za Serikali kama Urithi wa Taifa, kuhifadhi Nyaraka muhimu za kihistoria na kutoa huduma za utafiti, kutumia mbinu za kitaalamu kwa kuzifanyia matengenezo kumbukumbu zilizo katika hali mbaya, kuendeleza, kusimamia na kuelekeza utumiaji bora wa kumbukumbu katika Ofisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, idara pia ina jukumu kubwa la kutoa taaluma juu ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu ili zipewe umuhimu unaostahili.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na uwelewa mdogo kwa watendaji wetu juu ya utunzaji wa kumbukumbu, ambapo katika sehemu zetu za kazi unaweza kukuta majalada ya kumbukumbu mbali mbali yamewekwa ghalani yakiwa katika magunia na kuchanganywa na vitu vyenye mafuta kama vile vifaa vichakavu vya magari, betri mbovu na kadhalika, kwenye sehemu ambazo wadudu kama vile panya na mende wanaishi na kuzaliana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kutowekwa vyema kwa kumbukumbu kunaathiri sana ufanisi na utendaji ndani ya ofisi zetu. Inachukua muda mrefu na wakati mwengine kutoonekana kabisa hati au nyaraka zinapohitajika kwa ajili ya kufanya maamuzi muhimu.

Aidha, hoja nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinahusu kukosekana kwa kumbukumbu kutokana na kutoonekana au kuharibika, hali inayopelekea kuwa na hoja za ukaguzi, ambazo zingeweza kuepukwa kama kumbukumbu zingetunzwa vizuri. Tungeweza pia kupunguza kwa kiasi kikubwa migogoro ya ardhi, upotevu wa Mali za Umma, madai na kesi katika vyombo vya kisheria kama tungeweka vyema kumbukumbu zetu.

Mhe. Mwenyekiti, idara katika mwaka wa fedha 2010/2011 imehudumia jumla ya watafiti 91 (kiambatisho nambari 2 kinahusika), imezifanyia matengenezo nyaraka 160 (kiambatisho nambari 3 kinahusika) zilizokuwa katika hali mbaya. Vile vile imefanya ukaguzi wa majalada 11,246, imekusanya kumbukumbu tuli na imetoa ushauri na maelekezo muhimu kuhusiana na mfumo bora wa

Utunzaji na Uhifadhi kumbukumbu katika Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali.

Taasisi zilizofanyiwa kazi hizo ni Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais; Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali; Shirika la Biashara la Taifa *ZSTC* na Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA*.

Mhe. Mwenyekiti, idara imetoa mafunzo ya vitendo ya uhifadhi na utunzaji wa kumbukumbu kwa wanafunzi 62 wa Chuo cha Utawala wa Umma wanaosomea Fani ya Usimamizi wa Kumbukumbu katika kiwango cha Cheti. Vile vile, jumla ya wafanyakazi watatu wamehudhuria mkutano wa kanda ya Afrika Mashariki na Kusini juu ya masuala ya Nyaraka na Kumbukumbu, mjini Maputo-Msumbiji. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, idara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 inakusudia kuandaa Sera ya Udhibiti wa Kumbukumbu, kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni, kutoa mafunzo kwa Maofisa Kumbukumbu, ili waweze kuzijali kumbukumbu, wajue namna ya kuzitunza, matumizi bora na mipaka ya matumizi.

Aidha, kuendelea kufanya kazi za ukaguzi wa kabla na baada ya udhibiti wa Kumbukumbu na Nyaraka, kuwajengea uwezo wafanyakazi watano katika Fani ya Udhibiti wa Kumbukumbu, kati ya hao wawili katika ngazi ya Cheti na watatu katika ngazi ya Diploma. Vile vile, idara itawajengea uwezo wafanyakazi kwa kushiriki katika mikutano ya kitaifa, kimataifa na semina, kuandaa vikao viwili vya Bodi ya Ushauri wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa na kuweka mazingira bora ya ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 idara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 460,249,300/=. Kati ya hizo shilingi 159,559,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na shilingi 300,690,300/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

OFISI KUU PEMBA:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya Utawala, Sera, Sheria na Kanuni mbali mbali za Utumishi. Pamoja na hayo, kutoa miongozo kuhusu ajira, mishahara na maslahi ya Wafanyakazi, kuimarisha Utawala Bora, Haki za Binaadamu, kusimamia shughuli za Kuratibu Hifadhi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kuimarisha ufanisi wa kiutendaji na majukumu, ofisi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 imepata wafanyakazi 10

kujaza nafasi za msingi kwa baadhi ya kada kwa njia ya uhamisho na kufanya manunuzi ya vifaa kwa matumizi ya Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wa ofisi, jumla ya wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo wakiwemo wafanyakazi wawili katika ngazi ya Diploma, mmoja Fani ya Uongozi wa Raslimali Watu na mmoja katika Fani ya Uhifadhi wa Kumbukumbu. Vile vile, wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya ngazi ya Cheti, mmoja Fani ya Uongozi wa Raslimali Watu na mmoja Fani ya Ufundi wa Umeme.

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa kwa upande wa Pemba kimewahudumia wananchi 52, ambao walihitaji huduma ya kutambua kumbukumbu zinazohusiana na migogoro ya ardhi, mirathi na mashamba, pia imezifanyia matengenezo nyaraka 350 zilizokuwa katika hali mbaya.

Vile vile kitengo kimefanya ukaguzi, kutoa ushauri wa kitaalamu na maelekezo muhimu kuhusiana na Utunzaji na Uhifadhi Kumbukumbu kwa Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Mazingira, Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Idara ya Ardhi na Usajili, Ofisi za Mahakama ya Chake-Chake, Wete na Mkoani, Idara ya Wakfu na Mali ya Amana pamoja na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi inakusudia kuimarisha shughuli za kiutendaji kwa kuajiri watendaji wenye sifa kulingana na mahitaji, kuwapatia mafunzo wafanyakazi 9 ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada katika fani mbali mbali.

Vile vile kuratibu mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa Watumishi wa Umma, kutoa elimu kwa watendaji wakuu wa Wizara naTaasisi za Umma na jamii juu ya misingi ya Utawala Bora, elimu ya Uraia na Haki za Binaadamu pamoja na kufuatilia uwezo wa Rasilimali Watu, ili kugundua mahitaji ya ziada na uwezo katika Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imekusudia kufanya uchambuzi wa kazi, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miundo ya utumishi katika taasisi za serikali, kuendelea kuweka mazingira bora ya kazi kwa kununua na kuhifadhi vitendea kazi vya Ofisi.

Aidha, Ofisi imepanga kuanzisha Kituo cha Uhuishaji wa Kumbukumbu, Kuimarisha Masjala, kutoa elimu kwa watendaji wakuu juu ya namna Bora ya Utunzaji wa Kumbukumbu, kutoa mafunzo kwa watunza kumbukumbu pamoja na kuanzisha vituo vya kumbukumbu vya Wizara na Taasisi za Umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 ofisi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 182,770,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI:

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Utumishi ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 117 ya Katiba ya Zanzibar, na majukumu yake yamefafanuliwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011. Chombo hichi kina kazi ya kusimamia na kutoa maamuzi ya haki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazoongoza masuala ya Utumishi wa Umma, kutoa miongozo na ufafanuzi wa masuala ya kiutumishi, kusikiliza rufaa za wafanyakazi na kuzipatia ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 katika kusimamia Haki, Fursa, Sheria, Kanuni na Miongozo ya kazi Serikalini, Tume imesikiliza jumla ya rufaa saba za wafanyakazi na kutolewa maamuzi. Kati ya hizo rufaa nne maamuzi yake yamekubaliana na madai ya wafanyakazi na rufaa tatu maamuzi yake yamekubaliana na maamuzi ya waajiri.

Katika kuijengea uwezo tume, mfanyakazi mmoja amepatiwa fursa ya masomo katika kiwango cha Shahada ya Kwanza katika fani ya Utawala wa Umma. Kwa maelezo zaidi ya utekelezaji wa kazi za tume (angalia kiambatisho nambari 5).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, tume imepanga kuwaelimisha wafanyakazi juu ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi Serikalini katika sehemu za kazi, kutayarisha mafunzo maalumu kwa maafisa wenye kushughulikia masuala ya uajiri Serikalini juu ya Uajiri na *HIV/AIDS*, Uajiri na Jinsia pamoja na Uajiri na Ulemavu. Pia kusimamia haki za wafanyakazi wa serikali, na masuala yote ya kiutumishi yakiwemo uajiri, kupandisha vyeo, kuthibitisha kazi, kuvusha vizingiti.

Aidha tume itaendelea kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar, katika kuandaa mafunzo na mitihani ya kitaalamu kwa wafanyakazi wa serikali, ili kuwajengea uwezo wa kitaalamu katika taaluma wanazozifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 tume inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 141, 265,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA:

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria namba 1 ya mwaka 2007 na jukumu lake kuu ni kutoa mafunzo ya kiutawala kwa Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Katika kufanikisha jukumu lake hilo chuo kinafanya tafiti zinazohusiana na Utumishi wa Umma, ili kubaini kasoro na kuzitafutia ufumbuzi kwa njia ya mafunzo kwa madhumuni ya kuimarisha Utumishi wa Umma wenye tija kwa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, chuo kinatoa jumla ya kozi nane katika ngazi za msingi, Cheti na Stashahada katika Fani za Rasilimali Watu, Ununuzi na Ugavi, Utawala wa Umma, Uhifadhi na Uwekaji Kumbukumbu, Sheria na mafunzo ya Kompyuta.

Mhe. Mwenyekiti, chuo kimepata usajili kutoka Baraza la Elimu ya Juu na Ufundi (*NACTE)*. Vile vile, chuo kimeandaa mitaala kukidhi mahitaji ya taaluma kwa Watumishi wa Umma na matakwa ya Baraza la Elimu ya Juu na Ufundi (*NACTE)*. Hadi kufikia Machi 2011, jumla ya mitaala mitano imethibitishwa na *NACTE* katika kada za Utunzaji Kumbukumbu (Cheti na Diploma), Uhazili (Cheti) na Usimamizi wa Rasilimali Watu (Diploma).

Aidha, Chuo kimetoa nafasi kwa watumishi 169 mwaka 2009, 191 mwaka 2010 na Watumishi 151 mwaka 2011 kujiunga na mafunzo ya Utawala, Utunzaji kumbukumbu na Kompyuta. Vile vile jumla ya wanafunzi wa kawaida 447 wanaendelea na masomo yao katika fani za Utawala wa Umma, Uhazili, Sheria, Uwekaji Kumbukumbu, Ununuzi na Ugavi katika ngazi ya Cheti na Stashahada. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuwajengea uwezo wafanyakazi wa chuo, jumla ya wafanyakazi wanne wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu wakiwemo wakufunzi wawili wanaosomea Shahada ya Uzamili, mmoja anaesomea Stashahada ya Uzamili katika fani ya *"Economic Diplomacy"* na mmoja anaesomea mafunzo ya Kompyuta katika ngazi ya Stashahada ya juu.

Vile vile, mkufunzi mmoja amepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani ya "*Data Base Design and Implementation"* pamoja na "*Multimedia and Graphic Design"* na wafanyakazi watatu wamepatiwa mafunzo ya ndani juu ya Utunzaji na Uwekaji Kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma – Tunguu unaendelea ambapo, asilimia 50 ya jengo imekamilika ikiwemo kumwaga zege la jamvi la ghorofa ya kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 kinakusudia kufanya Uchambuzi Yakinifu wa mahitaji ya chuo, ili kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano, kuwajengea uwezo wafanyakazi wanne wa chuo kwa kuwapatia nafasi za masomo ndani na nje ya nchi, kuinua maslahi ya wafanyakazi kwa kuandaa Muundo wa Utumishi.

Vile vile kuandaa kozi mpya na kupitia mitaala ya chuo ili itimize mahitaji ya Utumishi wa Umma pamoja na matakwa ya Baraza la Elimu ya Juu na Ufundi (*NACTE)* na kuwajengea uwezo Watumsihi wa Umma kwa kuwapatia mafunzo ya Utunzaji Kumbukumbu na Uhazili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 chuo kinaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 855,490,000/=. Kati ya hizo shilingi 470,000,000/= ni ruzuku kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida na shilingi 385,490,000/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ipo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kifungu 112. Kiutendaji ofisi inaongozwa na Sheria ya Fedha Nambari 12 ya mwaka 2005, Sheria ya Manunuzi Nambari 9 ya mwaka 2005 na Sheria ya Ukaguzi Nambari 11 ya mwaka 2003.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la ofisi ni kuidhinisha utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali na kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo na rasilimali nyengine kutoka serikalini au kwa Washirika wa Maendeleo kupitia Miradi, Programu mbali mbali na kutoa taarifa za ukaguzi katika Baraza la Wawakilishi.

Lengo kuu la ukaguzi ni kuleta ufanisi katika upatikanaji wa Rasilimali za Umma na Matumizi yake, ili kuondoa ubadhirifu, wizi, matumizi mabaya ya rasilimali na kutotimiza wajibu wakati wa utekelezaji wa majukumu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011, ofisi imefanikiwa kutayarisha muongozo wa kazi za ukaguzi unaozingatia viwango vya Kimataifa, ambao ni dira kwa kazi za ukaguzi kwa taasisi pamoja na kuwaelimisha wafanyakazi husika juu ya taaluma zinazohitajika katika kufanikisha utumiaji wa muongozo huo.

Vile vile, ujenzi wa jengo la Ofisi kwa Unguja umekamilika na ofisi imenunua jengo lilioko mbele ya Makao Makuu ya Ofisi, ili kupata nafasi zaidi. Kwa

upande wa Pemba, Ofisi inamiliki kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi chenye ukubwa wa mita za mraba 589 katika Shehia ya Tibirinzi - Chake Chake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ofisi pia imetayarisha na kuwasilisha ripoti ya mwaka 2008/2009 ya Ukaguzi wa Hesabu Serikalini. Takwimu za ripoti za ukaguzi katika kipindi hicho, zinaonesha kuwepo kwa mafanikio makubwa ya kiutendaji na kupungua kwa kiasi kikubwa cha matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, matayarisho ya ripoti ya mwaka 2009/2010 yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, mafunzo ya msingi ya *"Risk Based Audit"* yametolewa, ambayo yamewajengea uwezo wafanyakazi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhakiki maeneo hatarishi kwa upotevu wa mapato ya serikali. Kwa upande wa usimamizi wa matumizi ya serikali, mafunzo hayo yatasaidia kutambua maeneo hatarishi ya matumizi ya fedha yanayofanywa kinyume na utaratibu.

Vile vile, watendaji wa ofisi wamepatiwa elimu ya ukaguzi katika maeneo mbalimbali yakiwemo; Ukaguzi wa Thamani *"Value for Money Auditing",* Ukaguzi wa Kompyuta "*Computerized Auditing"* na Ukaguzi wa Mazingira *"Environmental Auditing". (Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imejipangia kuandaa Mpango Mkakati wa Pili wa mwaka 2011 – 2014, ambao utalenga kutekeleza na kushughulikia matumizi na maendeleo ya ofisi, kuifanyia mapitio Sheria ya Ukaguzi Nambari 11 ya mwaka 2003 ili iendane na mazingira kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar. Aidha, kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya Ukaguzi Yakinifu, Ukaguzi wa Kompyuta na Ukaguzi wa Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,283,928,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida. *(Makofi)*

MASLAHI YA WAFANYAKAZI:

Mhe. Mwenyekiti, Rasilimali Watu (Wafanyakazi) ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sera na Mipango mbali mbali ya kitaifa inapiga hatua. Katika kuzingatia hilo serikali imekua ikichukua hatua mbalimbali za kuwaendeleza kielimu na maslahi kwa kufanya marekebisho ya mishahara ya Watumishi wa Umma.

Serikali imekua ikifanya juhudi za kuwaendeleza watumishi kielimu, ili kukabiliana na mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia na mifumo mipya ya uendeshaji wa Sekta ya Utumishi wa Umma. Kwa upande wa maslahi, Serikali imefanya juhudi mbali mbali zikiwemo kuunda Kamati zenye lengo la kuangalia maslahi ya Watumishi wa Umma, ili waweze kukabiliana na gharama za maisha; ikiwemo Kamati iliyoongozwa na Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Rais wa Awamu ya Saba Dkt. Ali Mohamed Shein katika Kampeni za kuomba ridhaa ya kuongoza nchi, aliahidi kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kuimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya Watumishi wa Umma kwa kadri hali ya uchumi wa Zanzibar utakavyoimarika. Kuanzishwa kwa Ofisi Maalum yenye hadhi ya Wizara kushughulikia masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ni miongoni mwa hatua za awali za utekelezaji wa ahadi hizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba, kabla ya mwaka 2007, mishahara na maposho ya watumishi yalikuwa yametenganishwa, baadhi ya maposho yalikuwa yanalipwa kama malipo mengineyo chini ya vifungu mbali mbali vya matumizi. Utaratibu huu ulisababisha kuibuka kwa aina mbali mbali za maposho kila wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ilipitisha uamuzi mwaka 2007 wa kuunganisha maposho na mishahara *"consolidation"* na kuweka viwango maalum vya mishahara kwa kufuata viwango vya elimu na kada husika na mishahara ikaendelea kulipwa kwa utaratibu huo hadi sasa. Utaratibu wa kuunganisha mishahara na maposho ulivuruga mpangilio wa ngazi za mishahara na haukutoa fursa kuwa na nyongeza. Aidha, utaratibu huo uliwaweka wafanyakazi wenye kiwango cha elimu cha aina moja katika ngazi sawa bila kuzingatia uzoefu na muda wa utumishi tokea alipopata cheti husika, hali ambayo ilileta malalamiko kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na kutatua matatizo yaliyotajwa hapo awali na kuzuia wataalamu kuacha kufanyakazi katika Utumishi wa Umma, Serikali imepitia upya Miundo ya Utumishi *"Scheme of Service"* ya kada zote, Miundo ya Mishahara *"Salary Structure"* yenye kuzingatia elimu na uzoefu wa Watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mapitio hayo, Serikali imeamua kupandisha kima cha chini cha mshahara kwa asilimia ishirini na tano (25%). Aidha, kwa wale wafanyakazi wa kima cha chini ambao wanaendelea na utumishi wao, pamoja na wale wa ngazi nyengine, mbali na kurekebishiwa mishahara yao kwa

mujibu wa ngazi zao za mishahara, mishahara yao itakua na ziada itakayozingatia elimu na muda wa utumishi wao. Upandishaji huo wa mishahara umezingatia pia nyongeza walizozikosa wafanyakazi tokea mwaka 2007, ingawa hakutokuwa na malimbikizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia ufinyu wa bajeti, utekelezaji wa mabadiliko haya ya mishahara mipya bila ya malimbikizo, utafanywa kuanzia mwezi wa Octoba 2011.

Mhe. Mwenyekiti, Hatua maalum zitachukuliwa za kuyafanyia mapitio maposho mbalimbali ambayo yanaendelea kulipwa kila mwezi. Wizara,Idara na Taasisi za Serikali, hazitakuwa na mamlaka ya kupanga na kuidhinisha maposho bila ya kupata kibali maalumu na kwa utaratibu kama utakavyo fafanuliwa hapo baadae. Nimatumaini yangu kuwa wafanyakazi wataongeza juhudi na maarifa katika kutoa huduma bora ili kuimarisha uchumi wetu na maendeleo ya Taifa.

SHUKURANI.

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kutoa shukurani zangu za dhati, kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kwetu na kutukabidhi jukumu la kuisimamia Ofisi yake inayohusika na Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pia kwa miongozo anayotupa kila mara inayotuwezesha kutekeleza majukumu yetu bila matatizo.

Mhe. Mwenyekiti**,** naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano mazuri tuliyonayo katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, naomba kuishukuru kamati ya Katiba na Utawala kwa mashirikiano yao ambayo, yametuwezesha kuwasilisha katika Baraza lako tukufu hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani maalum tunazitoa kwa Katibu Mkuu Kiongozi, kama mkuu wa watumishi wa umma, kwa miongozo yake katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani kwa Bodi ya ushauri ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa pamoja na Baraza la Chuo cha Utawala wa Umma, kwa kusimamia vyema majukumu yao na ushauri wanaonipatia katika kufanikisha majukumu ya Taasisi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, shukrani zangu za dhati nazitowa kwa watendaji wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora hususan Katibu Mkuu, Naibu

Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi zinazojitegemea, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wote wa Zanzibar na Jumuiya za Vyama Huru vya Wafanyakazi kwa mashirikiano na maoni yao wanayotupatia katika kuimarisha mazingira bora ya utumishi na maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Tumbatu kwa kuonesha imani yao kwangu na kunichagua kwa mara nyengine tena kuwa mwakilishi wao, na hatimae kwa imani hiyo hiyo, Mheshimiwa Rais akaniteua kushika wadhifa nilionao. Nawaahidi kwamba nitatekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa ujasiri na uaminifu. Pia naishukuru familia yangu hususan Mke wangu kwa uvumilivu wao kutokana na muda mwingi ambao, nalazimika kulitumikia Taifa na kuwa mbali nao pia na moyo wanaonipa na kuniongezea ujasiri wa kutekeleza majukumu yangu.

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio niliyoyaeleza katika hotuba hii, yamechangiwa na wengi na kwa namna mbalimbali. Kwa hivyo shukurani maalum nazitoa kwa Viongozi na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Ofisi ya Rais Utawala Bora za Jamhuri ya Muungano. Aidha, nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo: Norway, USA, Japan, Korea, China, Uingereza, India, Singapore, Uholanzi, Malaysia, Australia, Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola, Tume ya haki za Binaadamu, Benki ya Dunia, UNDP, ADB, ILO, na wengine wote ambao tunashirikiana katika kujenga Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar.

HITIMISHO.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi yetu ina mafungu mawili ya bajeti fungu nambari 11 la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na fungu nambari 44 la Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inategemea kukusanya jumla ya Tzs.5,000,000/= kupitia fungu nambari 11 ikiwa ni ada ya ukaguzi. Aidha, kwa upande wa matumizi ya kazi za kawaida, inategemea kutumia jumla ya Tzs. 3,280,931,000/=, kati ya hizo Tzs. 1,283,928,000/= ni matumizi ya fungu11 na Tzs. 1,997,003,000/= ni matumizi ya fungu 44, na fedha zilizotengwa kwa Matumizi ya Maendeleo ni Tzs. 1,574,315,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muhtasari Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inategemea kukusanya jumla Tzs. 5,000,000/= kwa upande wa

mapato na kwa upande wa matumizi, jumla ya Tzs. 4,855,246,000/= zinategemewa kutumika kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Mwenyekiti Kamati ya Katiba Sheria na Utawala: Mhe. Mwenyekiti, **n**apenda kuchukuwa fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujalia neema ya uhai pamoja na afya njema miongoni mwetu na kutuwezesha kukutana tena jioni hii ya leo katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, katika kutekeleza majukumu yetu muhimu ya kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada huu muhimu wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka 2011/2012 kwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa jimbo la Mji Mkongwe kwa imani kubwa waliyoionesha kwangu kama walivyodhihirisha kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuwawakilisha katika Baraza hili tukufu. Nataka niwahakikishie kwamba nitatekeleza dhamana zangu kwa uwezo wangu wote na kutimiza ahadi zangu zote kwao kama ambavyo nimeshirikiana nao katika kipindi kifupi tokea uchaguzi kuanza kuzitekeleza. Nawahakikishia kwamba sitowaangusha na nitaendelea kuwa Mwakilishi wao makini.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vile vile kumpongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Haji Omar Kheri kwa namna alivyotuwasilishia Hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka 2011/2012, hotuba ambayo imetoa mwanga na kuonesha azma ya Serikali katika kufanya mageuzi makubwa ya utumishi wa umma na maslahi ya watumishi wa umma pamoja na kusimamia utawala bora hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niwapongeze watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Joseph Meza, ambao kwa namna moja au nyengine wamekuwa washauri wazuri kwa Mheshimiwa Waziri lakini pia wametoa mashirikiano ya dhati na kutoa ufafanuzi kwa masuala mbali mbali kwa Kamati yetu muda wote tulipokuwa tunafuatilia utekelezaji wa kazi za Ofisi hii. Wamefanya kazi nzuri na kamati inathamini sana utekelezaji wa majukukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa kupitia kwa makini mapendekezo hayo ya makadirio. Mheshimiwa Mwenyekiti ili kuzipa nguvu shukurani zangu hizo napenda kuwatambua Wajumbe hawa kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina wajumbe nane (8) ambao walihusika kikamilifu katika kupitia Makadirio haya yaliyowasilishwa hapa leo. Wajumbe hao ni:

1.	Mhe. Ali Abdalla Ali	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4.	Mhe. Mussa Ali Hassan	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Khamis Silima-	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
8.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
9.	Ndg. Nasra Awadh Salmin	Katibu
10.	Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora *(OR-UUUB)* ni miongoni mwa Taasisi mpya zilizoanzishwa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 kwa lengo la kusimamia Utumishi wa Umma katika kuwahudumia wananchi na kuimarisha Utawala Bora ikiwa ni pamoja na kutoa mwongozo kuhusu uongozi na utekelezaji wa Utumishi wa Umma yakiwemo masuala ya kuanzisha matumizi ya mbinu mpya za uongozi na utekelezaji katika maeneo mbali mbali ya Utumishi wa Umma, mbinu ambazo zinahusisha kukusanya, kuchambua na kudhibiti taarifa na takwimu mbali mbali zinazohusu uongozi na utendaji wa Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, Ukiacha majukumu mbali mbali yanayofanywa na Idara zake, Ofisi hii ndiyo inayohusika na kusimamia mageuzi ya Utumishi Serikalini *(Comprehensive Public Service Reform)* yanayoshirikisha mageuzi ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reform)* na kuchunguza uwezo uliopo wa Rasilimali Watu ili kugundua mahitaji ya ziada ya uwezo wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma Zanzibar, pamoja na kutoa ufafanuzi wa miongozo na matoleo kuhusu masuala yanayohusu maposho mbali mbali, ajira na stahiki nyenginezo kwa Watumishi wa Umma na Watumishi wengine ambao stahiki zao zinasimamiwa na kupangwa na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na majukumu hayo, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora pia imepewa majukumu mengine ya kuimarisha na kusimamia

misingi ya Utawala Bora nchini ikiwa ni pamoja na kuzifanyia ukaguzi fedha na rasilimali zote zinazotolewa katika Mfuko wa Hazina wa Serikali na washirika wa maendeleo, pamoja na kuhifadhi nyaraka muhimu za kihistoria na kumbukumbu za Serikali kama urithi muhimu wa Taifa.

Mhe Mwenyekiti, Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kukamilisha muundo wake katika muda mfupi tokea ilipoanzishwa na kuonesha dalili zote za umakini wa hali ya juu katika kujipanga kutekeleza majukumu iliyopangiwa. Kamati inaihakikishia Ofisi hii kuwa itaendelea kufanya nayo kazi bega kwa bega kwa lengo la kufanikisha majukumu yake yote kwa kiwango cha hali ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, Uanzishwaji wa Ofisi hii umekusudiwa kutimiza malengo yaliyoelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein, katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi la Nane ambayo ni pamoja na kuimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya watumishi wa umma ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi, maandalizi ya miundo bora ya Utumishi wa Umma, kusimamia maadili kwa watumishi katika ngazi mbali mbali, kurejesha nidhamu na uwajibikaji kazini, kuzuia na kupambana na rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, kufanya ukaguzi wa hesabu za serikali kwa wakati na kuhakiki orodha ya wafanyakazi ili kubaini kama kuna wafanyakazi hewa.

Mhe. Mwenyekiti, Ili kuweka msingi madhubuti wa utekelezaji wa malengo hayo yaliyoelezwa na Mheshimiwa Rais, Serikali iliwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi mwezi Januari mwaka huu, mswada wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 ambao ulifanyiwa kazi kubwa na Kamati yetu na Baraza kwa ujumla na hatimaye ukapitishwa. Mswada huu umetoa matumaini makubwa kwa wananchi na washirika wa maendeleo kwamba Zanzibar sasa itaingia katika zama mpya za utumishi wa umma uliojikita kujielekeza katika matokeo ya kazi, kujielekeza kwa mpewa huduma, kujielekeza katika kushiriki, kujielekeza katika thamani ya fedha, ugawaji wa madaraka, na wajibu wa kuitumikia mamlaka ya nchi. Kamati ingependa kujua Mswada huo ambao umepitishwa muda mrefu sasa umefikia wapi na lini utaanza kutumika ili kuanza kuzaa matunda hayo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora imekuja na habari njema ambazo zilikuwa zikisubiriwa kwa hamu kubwa na watumishi wa umma na wafanyakazi kwa ujumla hapa nchini ambazo ni zile zinazohusu kupandishwa kwa viwango vya mishahara na kurejeshwa tena kwa utekelezaji wa miundo ya utumishi *(Scheme of Service*) na miundo ya mishahara *(Salary Structure)* yenye kuzingatia elimu na uzoefu wa watumishi baada ya kuipitia upya. Kamati imepokea kwa faraja

kupandishwa kuanzia mwezi Oktoba 2011 kwa kima cha chini cha mshahara kwa asilimia 25% pamoja na kurekebishwa kwa mishahara ya wafanyakazi wa kima cha chini na watumishi wa umma wa ngazi nyengine wanaoendelea na utumishi wao, ambapo pia mishahara yao itakuwa na ziada itakayozingatia elimu na muda wa utumishi wao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba huu ni mwanzo tu na kwamba Serikali itaendelea kupandisha viwango vya mishahara na kuinua maslahi mengine ya watumishi wa umma kadiri uchumi utakavyokuwa ukiimarika, jambo ambalo halina shaka kutokana na mipango thabiti iliyopo na uongozi makini wa Serikali ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa.

Kamati inatumia fursa hii kupitia Baraza lako tukufu kuwataka wafanyabiashara kutoigeuza hatua hii njema ya Serikali kuwa kichocheo cha tamaa binafsi kwao na kupandisha bei za bidhaa kwani wanaelewa kuwa hatua hii inatekelezwa bila ya Serikali kupandisha viwango vya kodi au kuanzisha kodi yoyote mpya katika mwaka huu wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaipongeza Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kuonesha matumaini katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hii imetokana na kufanikiwa kutayarisha rasimu ya Mpango mkakati wa Wizara wa miaka mitatu (2011-2014) na Mpango wa matumizi wa Muda wa Kati – *MTEF*. Vile vile, Idara imeratibu utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Utumishi wa Umma na Sera ya Usafiri kwa Viongozi, Watendaji Wakuu na Watumishi wengine wa Umma.

Kamati inapongeza malengo ya mwaka huu wa fedha ya kutayarisha sera ya mawasiliano ya kielektroniki *(e-Government)*, kufanya utafiti wa namna watumishi wa umma watakavyofaidika na huduma za Bima ya Afya, na kuanzisha mfumo wa utoaji wa taarifa wa Ofisi kwa njia ya kompyuta (Management Information System).

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inatambua kwamba Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ingependa kufanya mambo makubwa zaidi lakini inakwazwa na ufinyu wa bajeti. Kamati inaishauri Ofisi kupitia Idara hii kuwa wabunifu na kutumia vyema mvuto na umuhimu unaotolewa kwa maeneo mawili wanayoyasimamia – yaani Mageuzi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora – kuandaa mapendekezo ya miradi ya maendeleo na maeneo mengine yanayohitaji kufanyiwa utafiti na kuandaliwa sera na kuyafikisha kwa nchi washirika wa maendeleo na jumuiya za kimataifa ambazo zinaweza kusaidia uimarishaji wa maeneo haya mawili muhimu kwa maendeleo ya nchi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imetiwa moyo na utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu kwa kufanikiwa kupata orodha ya vyuo vyote vinavyotambulika na Baraza la Elimu ya Juu na Ufundi – *NACTE* kwa nia ya kuwataka maofisa waratibu mafunzo kutumia vyuo hivyo kwa kuwasomeshea wafanyakazi wao. Kamati imevutiwa na mpango wa Idara kwa mwaka ujao wa fedha wa kuandaa Sera ya mafunzo, kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa watumishi wa umma *(Training Need Assessment)* ili Wizara na Taasisi ziweze kuratibu mafunzo kutokana na mahitaji sahihi ya Utumishi wa Umma.

Kamati inatambua kuwa kuna tatizo kubwa la watumishi wengi wa umma aidha kutokuwa na sifa au kuwa na chini ya viwango vya sifa zinazotakiwa kushikilia nafasi walizo nazo. Kamati inashauri kuwa Idara hii iandae mpango maalum utakaohakikisha kuwa kila Wizara na Taasisi za Serikali zinakuwa na programu ya kudumu ya kuwaendeleza kimafunzo watumishi wake *(manpower development programme*) ili waweze kuongeza ujuzi na hivyo kumudu kazi zao na kutimiza matarajio ya wanaofuata huduma za utumishi wa umma, wawe wananchi au wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza hapa nchini. Ripoti ya Urahisi wa Kufanya Biashara Zanzibar ya 2010 *(Doing Business in Zanzibar 2010)* imebainisha maeneo kadhaa ambayo Zanzibar bado iko nyuma katika kuvutia biashara na uwekezaji, na mengi kati yao yanahusika na kutokuwepo kwa ufanisi kazini na urasimu wa kupita kiasi. Ni jukumu la Idara hii kuzisaidia Wizara na Taasisi zote za Serikali kubadilisha hali hii ya utendaji Serikalini inayotokana na watumishi wa umma tulio nao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imetiwa moyo na malengo ya Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu ya kuwapatia mafunzo Maofisa Utumishi wa Wizara na Taasisi za Umma juu ya namna bora ya matayarisho ya Makisio ya Mishahara *(Nominal Roll),* kukusanya na kuweka kumbukumbu na taarifa za msingi za wafanyakazi wa Utumishi wa Umma na kuziingiza katika Mfumo wa Taarifa za Wafanyakazi *(Human Resource Database)* pamoja na kuja na mpango unaorahisisha kuwatambua wafanyakazi wanaotegemewa kustaafu. Kamati inalipongeza hili na kuitaka Ofisi hii kutumia mfumo huu wanaokusudia kuuanzisha kuwabaini watumishi hewa na wastaafu hewa ili kudhibiti upotevu wa fedha za walipa kodi zinazopotea kupitia malipo ya watu hao wasiokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, Kuhusu Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi, Kamati inapongeza hatua ya kukamilisha Miundo ya Utumishi *(Scheme of Service)* kwa kufanya uchambuzi wa kazi na kupanga madaraja kwa kada zote za watumishi wa Wizara na Taasisi zote za Umma. Kamati pia inapongeza malengo ya Idara hii kwa mwaka ujao wa fedha ya kutengeneza Mkataba wa Kutoa Huduma kwa Wananchi *(Service Charter)*, hatua ambayo itaiweka nchi yetu sambamba na nchi nyingi zilizoendelea zenye mkataba kama

huu ambao hutumika kama mwongozo wa utoaji huduma na hivyo kuinua kiwango cha utolewaji huduma kwa wananchi na hata wageni wanaofika nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hizi tatu tulizozitolea maoni hapa yaani Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu, Idara ya Mipango na Rasilimali Watu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi ndiyo roho za Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika kutekeleza mageuzi makubwa yanayotarajiwa kwenye Utumishi wa Umma, mageuzi ambayo yanatarajiwa yaongeze ufanisi na uzalishaji ndani ya Sekta ya Umma na pia kutoa mchango katika kushajiisha ukuaji wa Sekta binafsi hapa Zanzibar. Kwa msingi huo, Kamati inasisitiza kwa Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuhakikisha kuwa kasma zilizotengewa zinaingizwa kwa ukamilifu na kwa wakati ili lengo la Mheshimiwa Rais katika sekta hii liweze kutimia.

Mhe. Mwenyekiti, Utawala Bora katika zama hizi ni dhana muhimu na isiyoweza kuepukika. Kamati inaitaka Idara hii kuchukua hatua zaidi ya zile inazochukua sasa kwa kukamilisha muundo wake utakaoipelekea kuwa na vyombo vyake au maofisa wake katika Wizara na Taasisi zote za Umma kuangalia *(monitor)* utekelezaji wa misingi ya utawala bora katika utendaji wa shughuli za siku hadi siku. Kamati inaitaka Idara kufuatilia siyo tu Taarifa ya Haki za Binadamu inayotolewa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora bali pia zile zinazotolewa kila mwaka na taasisi binafsi kama Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar *(ZLSC).* Kamati inaitaka Idara kuchukua hatua za kuwasilisha yale yanayoripotiwa katika Taarifa hizi katika Wizara na Taasisi za Umma zinazohusika ili hatua za marekebisho ya hali ya haki za binadamu ziweze kuchukuliwa na kuzidi kuipandisha chati Zanzibar katika uwanja huo. Tutambue kwamba tukifikia viwango bora vya kuheshimu haki za binadamu na misingi ya utawala bora, basi tunajijengea sifa zaidi za kuingia katika kundi la nchi zinazostahiki kusaidiwa katika miradi yake ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imepewa jukumu muhimu la kukusanya, kuzihifadhi na kuzitunza nyaraka na kumbukumbu za taifa. Idara hii kwa miaka mingi sasa imekuwa ikipewa sifa kwa kuwa bora na kuwa na nyaraka za kale zaidi kuliko nchi nyingi za ukanda huu wa Afrika na Bahari ya Hindi. Hata hivyo, Kamati hairidhiki na hali iliyopo hivi sasa katika eneo iliopo la Kilimani ambapo kuna nyumba binafsi za raia ndani ya uzio wa jengo la Idara hiyo. Kamati ilitoa ushauri kwa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuona uwezekano wa kuzinunua nyumba hizo binafsi ili kutoa fursa ya kupanua jengo la Idara ya Nyaraka. Tunazo tetesi kwamba Ofisi inapanga kujenga jengo jipya la Wizara lenye ghorofa nane (8) ambalo linategemewa pia kujumuisha Idara ya Nyaraka na

Kumbukumbu za Taifa. Mradi huu hauonekani kuwemo katika miradi ya Serikali moja kwa moja. Kamati inapendekeza kwa Serikali kuupa mradi huu umuhimu wake ili Wizara na Idara zake ziweze kuwa na sehemu bora za kufanyia kazi kulingana na mahitaji ya sasa ya Wizara na Idara zake.

Mhe. Mwenyekiti, Kuhusu Ofisi Kuu Pemba, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Ofisi hii Pemba na Idara inazoziratibu na kujionea hali halisi ya mazingira magumu ya utendaji kazi kwa watumishi wake na hata Ofisa Mdhamini. Kamati inashauri Ofisi kuchukua hatua za makusudi kuona Ofisi yake iliyopo Pemba inapata mahitaji yake ya msingi kuweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake ili isiendelee kujiona kama mtoto wa kambo.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha Utawala wa Umma ni taasisi nyengine muhimu ya Serikali inayosimamiwa na Ofisi hii. Kwa jumla, Kamati imesikitishwa na mazingira magumu ya jengo ambayo Chuo hiki kinafanya kazi zake ingawa inatiwa moyo na hatua iliyofikiwa katika kujenga jengo lake jipya huko Tunguu. Pamoja na kufahamu mazingira magumu ya Chuo hicho, Kamati haikufurahishwa na kitendo cha Chuo kushindwa kuwasilisha mbele yake kama ilivyotakiwa kumbukumbu sahihi za mapato yake yanayotokana na ada za masomo zinazotozwa na jinsi yanavyotumika. Badala yake, Kamati imepewa makisio ya mapato na matumizi ya Chuo kwa mwaka ujao wa fedha. Hali hii haipaswi kuachwa ikiendelea na Ofisi inapaswa kulifuatilia suala hili na kujua hali halisi ya mapato na matumizi ya Chuo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imeridhishwa sana na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuweza kukamilisha na kuwasilisha Ripoti ya mwaka 2008-2009 ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kamati inaomba kutumia fursa hii kumpongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya ambayo imepelekea mageuzi makubwa ya utendaji kazi katika Ofisi anayoiongoza. Kamati inatoa wito kwa Serikali kuitumia Ofisi ya *CAG* kama kigezo chema *(role model)* ya vipi ofisi zetu na utendaji wao wa kazi unapaswa kuwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunatarajia sifa hizi hazitokuwa kama hadithi ya mgema kwamba akisifiwa tembo kulitia maji, bali tunaamini itaongeza ufanisi zaidi wa ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha uwezo wa wakaguzi wake, Ofisi imetoa mafunzo ya msingi ya *"Risk based audit*" ambayo lengo lake ni kuwajengea uwezo wafanyakazi kuweza kuhakiki maeneo ya upotevu wa mapato ya serikali na kutambua maeneo hatarishi ya matumizi ya fedha yanayofanywa kinyume na utaratibu ambao serikali imejipangia. Kamati pia inafahamu kwamba

mafunzo ya Ukaguzi wa Thamani *(Value for Money Auditing)* Ukaguzi wa Kompyuta *(Computerised Auditing)* na Ukaguzi wa Mazingira *(Environmental Auditing)* yametolewa. Ni matumaini ya Kamati kwamba ujuzi walioupata wakaguzi wa Ofisi hii kutokana na mafunzo haya utatumika kuinua kiwango cha ukaguzi hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaitaka Serikali kuthamini kazi zinazofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuendelea kuitafutia fedha za kukamilisha mradi wa marekebisho makubwa ya jengo la ziada la Ofisi walilolinunua ili kazi yao muhimu kwa Taifa iweze kufanyika katika mazingira mazuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya Idara na Taasisi ilizo nazo hadi sasa, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kuanzisha taasisi nyengine tatu mpya kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa lengo la kusimamia Utumishi wa Umma katika kuwahudumia wananchi na kuimarisha Utawala Bora linafikiwa kwa haraka. Taasisi hizo ni Taasisi ya Maadili ya Viongozi na Kuzuia Rushwa, Kamisheni ya Utumishi, na Idara itakayosimamia mawasiliano ya kielektroniki *(e–Government).*

Kamati inatoa wito kwa Ofisi hii kuharakiza kuanzishwa kwa Taasisi hizo kwani mahitaji ya wananchi kwa sasa ni makubwa na kuna haja uanzishwaji wake ufanywe haraka iwezekanavyo ili malengo ya mageuzi ya Utumishi wa Umma na usimamizi wa misingi ya Utawala Bora yaweze kutimia.

Sambamba na kuanzishwa kwa Taasisi ya Maadili ya Viongozi na Kuzuia Rushwa, Kamati inasisitiza Ofisi hii kukamilisha matayarisho ya Mswada wa Kuanzisha Taasisi hii ya Maadili ya Viongozi na Kuzuia Rushwa na kuiwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi mapema iwezekanavyo ndani ya mwaka huu wa 2011 kama ilivyokuwa imeahidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maoni hayo, na kwa niaba ya Kamati, niwaombe sasa wajumbe wenzetu wa Baraza lako tukufu, wakubali na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2011/2012, ambapo mapato yanakadiriwa kuwa Tshs. 5,000,000/= na matumizi ni TShs. 4,855,246,000/=. Katika matumizi Tshs. 1,997,003,000/= ni kwa kazi za kawaida za Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora (fungu 44) na Tshs. 1,283,928,000/= ni za matumizi ya kawaida ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (fungu 11) na Tsh. 1,574,315,000/= ni kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati katika kufuatilia mafungu ya matumizi imegundua kwamba fungu nam. 11 la kazi za maendeleo kwa Ofisi ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Tshs. 196,350,000/=) liliopo uk. 648 – 649 la kitabu cha Makadirio ya Mapato na Matumizi halikuwa limeombwa wala kukubaliwa na hivyo limeingizwa kimakosa katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi. Kamati inaliomba Baraza lako tukufu kulizingatia hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tunaunga mkono hoja hiyo na vile vile kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe nasema pia naunga mkono hoja na kuwaomba Wajumbe wenzangu wamuunge mkono Mheshimiwa Waziri ili Wizara itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana (*Makofi*)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikiwa mchangiaji wa mwanzo baada ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Naomba kabla ya kusema lolote kwanza kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani niunge mkono hoja hii mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, si kawaida yangu kuunga mkono mwanzo lakini nina kila sababu ya kuunga mkono. Naunga mkono kwa hoja na kwa sababu za msingi ambazo kitabu hiki kimetosheleza. Naunga mkono kwanza kitabu hiki kimeonesha sura halisi ya Umoja wa Kitaifa ambao viongozi wetu watatu wakuu wa nchi hii wamewekwa kwenye gamba la kitabu hiki.

Pili naunga mkono kwa sababu kitabu hiki kimeandikwa kwa ufupi lakini kwa ufasaha. Baada ya hapo nimpe pole Mhe. Waziri wakati wa kusoma hotuba yake alikuwa na mtihani wa kuzimwa na umeme. Hii maana yake ni changamoto ya uwajibikaji na ndio sehemu ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani suala lile linamuonesha Mhe. Waziri kwamba uwajibikaji katika mambo ya uma ni muhimu na limempa funzo kweli kweli kwamba akitoka hapa asimamie uwajibikaji wa Serikali hii ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze kwenye jambo muhimu sana ambalo Wazanzibari walikuwa wanalisubiri nalo ni maslahi ya wafanyakazi. Mimi binafsi kama Mwakilishi wa Jimbo la kiwani naunga mkono hatua ya serikali ya kuamua kupandisha mshahara kwa kima cha chini kwa asilimia 25.

Napongeza pia malimbikizo ya nyongeza ambazo tangu mwaka 2007 wafanyakazi wetu walikuwa wakidai sasa zimeamuliwa kupatikana kuanzia mwezi Oktoba. Nadhani hii ndio sehemu hasa ya utawala bora. Wafanyakazi

wetu walikuwa wamevunjika moyo sana kwamba nyongeza ile ya asilimia ndogo iliyoongezwa hadi hii leo kuwa wafanyakazi walikuwa hawajaipata. Maamuzi ya serikali chini ya Mhe. Haji Omar Kheri nadhani ni ya busara na ni ya kupongezwa sana kwa Wazanzibari.

Naunga mkono tena baada ya serikali kuona kwamba kuna haja ya kuangalia viwango vya elimu na muda wa utumishi wa wafanyakazi wetu. Tumekuwa hatuwafanyii haki wafanyakazi wetu kwamba wana elimu kubwa lakini maslahi yao ni madogo. Hatua hii ya serikali nadhani naipongeza. Wafanyakazi wenye viwango vya elimu na waliochukua muda mrefu wa utumishi lazima wapewe maslahi kulingana na uwezo wao.

Suala langu ni kwamba Baraza litaridhika vipi kwamba mfanyakazi mwenye digirii aliyefanya miaka 20 ya kazi kweli ameongezewa stahiki yake kwa mujibu sheria. Namuomba Mhe.Waziri hapa alielimishe. Mimi kama mwakilishi nitajuaje kama wafanyakazi wangu wenye viwango vya elimu stahili na wenye muda wa stahili kweli nyongeza yao imewafikia ili kuondosha migongano baadaye ya kufanya kazi. Mhe. Waziri naomba hilo aniweke wazi ili kwa niaba yangu na wafanyakazi wa Zanzibar hii wasije wakalalamika.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze serikali kwamba wameona kuna haja ya kudhibiti maposho mbali mbali. Ni jambo lisilo na kificho kwamba baadhi ya watumishi walikuwa wanapata maposho kiholela bila ya kuzingatiwa taratibu za kisheria. Kwa mfumo huu wa serikali nachukua nafasi hii pia kupongeza uwamuzi huu kwamba sasa maposho yataongezwa kwa kila mwenye sifa ya kuongezwa kwa utaratibu na nidhamu. Jambo hili pia limeonesha ukomavu wa wizara hii na serikali kwa jumla chini ya Mhe. Haji Omar Kheir kwamba sasa nyongeza za maposho yatazingatia sifa, vigezo na kwa wakati husika. Hili pia tumeambiwa kwamba utatolewa muongozo. Naomba nijue nani atatoa muongozo na utatolewa lini wafanyakazi wetu wafaidike.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu wafanyakazi kwamba wizara hii sasa imeamua kusimamia maslahi ya wafanyakazi sio mishahara lakini pamoja na kuwapatia mafunzo mbali mbali. Tumeona hapa kwenye hotuba hii kwamba Chuo cha Utumishi wa Umma kimefundisha wafanyakazi 208, wanawake ni 143 na 65 wanaume. Napongeza hatua hii na namuomba Mhe. Waziri aendelee kuwasomesha wafanyakazi wake. Hii ndio sehemu ya haki yao na ndio sehemu ya uwajibikaji wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nimelitoa dosari, namuomba Mhe. Waziri aniweke sawa. Kuna mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu nje ya nchi. Kuna mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi, wafanyakazi 53 lakini hakuna mchanganuo wa jinsia kwamba wanawake wangapi na wanaume wangapi.

Pia ni vizuri zaidi ili kuondosha shaka kwa wafanyakazi wetu tungepata majina tukamjua nani kapelekwa nje na nani hajapelekwa. Kuna wasi wasi kwamba kuna baadhi ya watu fursa hii wanaitumia vibaya, wanawapeleka watu wa karibu nje kusoma ovyo ovyo. Ni vyema Mhe. Waziri najua kwa sababu ya ugeni wa Wizara hii lakini nikuombe tu mara ya pili ni vyema ukatuandikia jina, jinsia yake na Idara aliyotoka ili kuweza kupima kwamba nani kapelekwa nje na jinsia gani imezingatiwa.

Pia kuna mafunzo ya muda mrefu ambayo kuna wafanyakazi wengi sana pia hilo halikuzingatiwa kuangaliwa jinsia yake ni wangapi wanaume na wangapi wanawake na majina yao. Tukajua kupima kwamba wafanyakazi wetu kweli wizara yako imezingatia kwa mujibu wa idara na uwezo wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri mwakani tukijaaliwa na hata leo pengine anifahamishe kwa vigezo hivyo ili wafanyakazi wengi wasijewakavunjika moyo kwamba kila siku amapelekwa fulani. Huu ndio uwajibikaji na huu ndio utawala bora.

Hotuba hii sio kubwa sana kwa sababu imeandikika na nidhahiri kwamba kuna mashirikiano ya Waziri na watendaji wake. Niseme tu kwenye kiambatanisho kule mwisho ninavyojua mimi kwamba Tume ya Maadili ya Utumishi wa Umma ni maadili ya Viongozi haijaundwa bado. Lakini kule mwisho nimeona ukurasa wa 53 kuna Tume ya Rushwa na Maadili ya Viongozi, kuna fedha zimetumika milioni nne, laki sita arubaini elfu mia nane na sabini na tisa. Naomba kujua tu tume hatujaunda bado, sheria hatujaunda lakini kuna fedha tayari imeanza kutumika mishahara au maposho. Mhe. Waziri labda uniweke sawa juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumuomba Mhe. Waziri kwamba jambo hili ni muhimu lazima sheria iletwe Barazani. Tuachane kabisa na majibu ya juzi ya Mhe. Waziri mmoja aliposema kwamba jambo hili linaleta fitna. Fitna huondoshwa kwa sheria. Ikiwa sheria huileti hapa ndio fitna inajengwa hapo. Lakini ukiweka sheria fitna itaondoka kila mtu atakula majani kwa mujibu wa urefu wa kamba yake.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana Mhe. Waziri kwamba Sheria ya Utumishi ya Maadili ya Viongozi ilete, kila mtu atangaze mali yake, mwenye ngalawa aseme, mwenye meli aseme hadharani wananchi wa Zanzibar wajuwe. Ili dhana ya kwamba kuna upotevu wa fedha za umma uondoke. Nakuomba usiogope fitna jenga historia mapema kwa sababu kazi ni kipimo cha utu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Afisi ambayo naipenda sana mie nayo ni Afisi ya CAG nimshukuru yule mama mwaka juzi alinipeleka Malesia. Na naamini mwaka huu haumaliziki atanipeleka pengine Uingereza.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu huyu mama ana uwezo. Uwezo huu umekuja sio to kwa sababu nyengine ila ni mashirikiano aliyokuwanayo na watendaji wake wote. Kadiri nilivyokuwa PAC miaka miwili na nusu iliyopita na ninavyomuuliza Mhe. Omar hapa kwa sababu sasa hivi yupo PAC bado mashirikiano yanaendelea kujengwa na wanafanyakazi kwa mashirikiano na uelewano.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimuombe kwamba aendelee kushauriana nao na waongeze bidii, waongeze mashirikiano kwa sababu wanawatetea Wazanzibari wote. Lakini nimejengwa wasi wasi kwamba kadiri unavyojituma na kutoa ripoti safi ya ubadhilifu wa fedha za umma uvunjaji wa sheria hakuna hatua inayochukuliwa kwenye serikali. Wasi wasi ni kwamba wataalamu hawa wa ofisi hii wanaweza wakabweteka na kuona kwamba madamu hakuna hatua yoyote basi tuacha jahazi itote. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nakuomba sana usimamie sheria hizi na wewe ndio kioo cha utawala Bora cha nchi hii.

Lakini pia afisi hii nimejengwa wasi wasi kwamba kwenye kitabu chako Mhe. Waziri ameomba fedha kwa ofisi hii bilioni moja milioni mia mbili thamanini na tatu laki tisa ishini na nane elfu (TShs. 1,283,928,000). Lakini kwenye kitabu kikubwa cha bajeti kuna bilioni moja milioni mia mbili thamanini na nne (TShs 1,282,000)ambayo ni zaidi ya milioni, zimezidi kidogo. Nilikuwa naomba nijue ipi sahihi na ipi imekosewa au pengine ndio kama vile Mhe. Jussa alivyozungumza kwenye maelezo yake ya ripoti ya Kamati.

Kwa ujumla Ofisi hii naiyunga mkono na naomba waongezewe fedha zipatikana kwa asilimia mia. Ili ule ukaguzi wa thamani wa kimazingira basi uwende na wakati. Vyengine ukaguzi wa kuangalia risiti umepitwa na wakati. Lazima tuwawezeshe ofisi hii wafanye kazi kitaalamu ili kugundua yale maovu au ule ubadhilifu ili wawe wanajenga kwenye utaalamu wao.

Mhe. Mwenyekiti nimesema kwenye hotuba hii sioni cha kukosoa na nimeridhika sana kuunga mkono mia kwa mia. Ingawa Mhe. Waziri amenivunja moyo kwamba Watumbatu hawana sifa ya kuoa mke mmoja, Watumbatu huanzia wawili mpaka wanne. Namuomba aoengeze ili ajenge ile heshima ya Kitumbatu. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti na mimi naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nikapata pumzi ya kuchangia.

Pili naomba nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuanzisha mahsusi wizara yenye jukumu la kusimamia masuala ya utawala bora. Sambamba na kumchagua Mhe. Haji Omar Kheir kuwa ndiye Waziri mwenye dhamana ya kuiendesha wizara hii ambayo mimi nasema ni moja kati ya wizara nyeti katika nchi. Wizara hii ndio serikali kwa sababu serikali ni watumishi wa umma na watumishi wa umma wote wapo chini ya muongozo wa wizara hii. Nampongeza Mhe. Rais, namtakia kheri na aweze kutekeleza vyema majukumu yake ya kuiendesha wizara hii.

Kabla sijaanza na miye, si kawaida yangu lakini naomba leo kwa mara ya kwanza nitangulie kuunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, utawala bora ni dhana pana sana yenye kuchukua eneo kubwa sana katika masuala haya ya uendeshaji wa serikali. Ni wizara mtambuka kwamba matendo na matokeo yote ya utendaji kazi Mawizara. Lengo ni kuleta ufanisi wa kumtumikia mwananchi. Lengo la serikali ni kuleta huduma, kuleta utendaji ambao mwisho ya siku mwananchi wa kawaida ndio anayenufaika. Kunufaika kwa mwananchi maana yake huo ndio utawala bora.

Wizara hii ni Wizara Mtambuka ambayo ina jukumu na ina wajibu wa kuhakikisha wizara zote katika serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatekeleza majukumu yake kama ilivyoagizwa na sheria mbali mbali zilizoundiwa. Nianze katika kada ya utumishi wa umma una changamoto kubwa sana. Tulikotoka haidhuru sivyo tulivyo, tumepiga hatua kwa kiasi kikubwa.

Serikali yetu inakabiliwa na tatizo kubwa sana la wafanyakazi hewa, tunakumbuka miaka ya karibuni tulikuwa na tatizo kubwa sana la wafanyakazi hewa. Mimi naamini mwenyekiti kwamba hadi sasa tatizo la kuwa na wafanyakazi hewa bado linaisumbua serikali. Sidhani kwamba inafanya kazi ya kutosha kufika hatua ya kuondosha wafanyakazi hewa. Bado mimi naamini wafanyakazi hewa wapo na ni budi hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe ili kuondokana na tatizo hili. Wafanyakazi hewa wameikosesha serikali fedha nyingi sana.

Changamoto ya pili tuliyonayo ni viwango duni vya maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na wanzangu kwa kuishukuru sana serikali kwa hatua yake ya kuongeza kiwango cha chini cha mshahara. Kwa kipindi kirefu tumekuwa tukisisitiza sana kwa serikali na tukisisitiza sana kwa wafanyakazi ili wahakikishe kwamba wanatekeleza wajibu wao. Wafanyakazi hutulalamikia kwamba ni kweli tunataka tutekeleze wajibu wetu lakini hali hairuhusu. Hali ya mishahara ni kweli hairuhusu. Mshahara anaopewa mfanyakazi haufiki hata wiki moja tayari hana kitu au ile siku ambayo anapokea mshahara ndio siku ile ambayo anapojilimbikizia deni jengine.

Inakuwa tayari keshalikopea na akimaliza kulipa inabidi anaendesha mwezi mzima hana chochote.

Nasema kwamba ni kwango kidogo lakini kwa muungwana kuongezwa chochote ni wajibu wake kushukuru. Tunashukuru kwa hatua hii ya serikali na tunaiyomba serikali isisite kufanya mapitio ya kuongeza mshahara kila mwaka. Isiwe leo imeshaongeza kiwango cha asilimia 25 kwa kiwango cha chini ikawa tena miaka hii mitano yote tunakwenda na kiwango hicho. Naiyomba sana serikali kwa mwaka huu ikiwa inaongeza hiyo tukijaaliwa na mwakani ifikirie tena. Naamini kwamba kwa jukumu hili alilopewa Mhe. Haji Omar Kheri kazi hiyo itakuwa ni rahisi sana kwake yeye.

Changamoto la tatu ni tatizo la kuwajibika kwa wafanyakazi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kama nilivyozungumza juzi sasa hivi unakuwa ni utamaduni. Ukiachia hii hoja ya maslahi duni ya wafanyakazi lakini kumejengeka utamaduni kwa wafanyakazi kutotomiza wajibu wao. Mimi nadhani wakati umefika kwa idara hii inayoshughulikia masuala ya wafanyakazi iyandae utaratibu maalum. Kila mfanyakazi kila mtumishi atekeleze wajibu wake. Inawezekana kabisa Mhe. Waziri akaandaa utaratibu wa kuweza kufahamu kwamba kila mtu katika siku kafanya kazi gani.

Mhe. Waziri hilo lizingatie sana. Ikiwezekana Waziri ajiulize leo umefanya kazi gani, Katibu Mkuu leo umefanya kazi gani, mtumishi wa kawaida karani leo umefanya kazi gani. Tutakapofanya hivyo tutapata kwa wiki mtumishi kafanya kazi gani kwa mwezi na ndio ule uhalali wa malipoyake utakapojiri. Leo Mhe. Mwenyekiti, inawezekana mtumishi mwezi mzima anakwenda kazini wakati anaotaka na anaondoka kazini wakati anaotaka, utakapomuuliza mtumishi mwezi huu umefanya kazi gani ili ustahiki kulipwa huo mshahara unaopewa kama mchango wako kwa taifa. Nina hakika utakuta baadhi ya wafanyakazi hawakufanya kazi yoyote kwa muda wa mwezi mzima.

Namuomba sana Mhe. Waziri kupitia idara zake hizi ajaribu kuandaa utaratibu wowote utakaowawezesha kila mfanyakazi kuweza kutoa ripoti zake kwa siku, kwa wiki na hatimaye kwa mwezi. Utakapofanya hivyo ndio itakuwa taifa tumelitendea haki. Kinyume na hivyo tutaendelea kuwalipa baadhi ya watu waliokuwa hawawajibiki. Kitu ambacho ni hasara kubwa sana kwa taifa.

Mhe. Mwenyekiti, wote walioendelea na wote watakaoendelea katika ulimwengu kipimo chao kikubwa ni kazi. Ukisikia wajapani, wameendelea watu wanatuhadithia wengine hatujawahipo kufika. Lakini Mjapani huona tabu ile saa 1:00 kwenye kutafuta pahala akala. Mara nyingi huwa tunaambiwa Japani wanakula kwenye magari, kwa vile jinsi ambavyo hataki apoteze hata dakika 10 kuipoteza bure bure bila ya kufanya kazi.

Kwa hivyo wote walioendelea siri kubwa ni kufanyakazi kwa bidii hakuna siri nyengine. Ikiwa Zanzibar na sisi tunataka tuendelee na tufike katika hatua hiyo. Ni lazima sasa tufanye mageuzi makubwa katika tabia yetu na kazi. Ni lazima tubadilike ndivyo ambavyo maendeleo ya haraka yatakuja katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine ni wingi wa wafanyakazi. Mheshimiwa ifike pahala tukubali. Imani yangu inanambia kwamba wafanyakazi tulionao ni wengi kuliko mahitaji tunayoyahitaji. Siku moja nilikwenda katika sehemu fulani ya kuuzia miche jimbo la Mhe. Abdalla Juma, idada ya wafanyakazi waliokuwepo pale ni wengi kuliko hata hiyo miche iliyokuwepo pale.

Hili ni tatizo na tukubali kwamba ajira tulizotoa kwa namna fulani tu. Tukubali kwamba kuna pahali tulikosea. Binaadamu akishajua kama kakosea kujirudi ndio wajibu. Idadi ya wafanyakazi tulionao sasa hivi katika serikali ni wengi sana. Pamoja na kwamba tunaunda ajira lakini ziwe ni zenye tija. Haiwezekani kwamba wafanyakazi waliokuwepo wanaotakiwa hasa ni wafanyakazi 20 sehemu ikawa na wafanyakazi 100, hilo ni tatizo. Fedha nyingi zinapotea na ndio siku zote tunazungumza kwamba matumizi ya serikali huzidi kila mwaka. Kwa nini matumizi ya serikali yazidi kila mwaka. Maana yake ni hii kwamba idadi kubwa ya wafanyakazi ambao hawahitajiki.

Zipo sehemu maalum, ukija kama haya Mabaraza ya Manispaa, ukija kwenye vikosi, hizo ni sehemu tunazoambizana mimi nina mtoto wa mjomba wangu na nenda kaombe Mungu, ndio kwahala kwa kuomba Mungu huko. Nina kijana wangu anataka kazi. Sasa wewe bwana huna sifa. Ah! lakini mlete tu na yeye aombe Mungu. Hana sifa yoyote lakini ndio utaratibu tunaotumia kuomba Mungu. Huo ndio utaratibu.

Changamoto nyengine tuliyonayo ambayo Mhe. Waziri atapaswa kuifanya, haidhuru tuwe na programu ya kufanya *estimate* watendaji wetu. Lakini ni lazima tufike pahala tujiangalie idadi ya halisi ya kiwango cha wafanyakazi wanaohitajika katika utumishi wa umma.

Tatizo jengine linalotukabili katika hili ni suala zima la namna ya kuwaendeleza wafanyakazi. Nashukuru Mhe. Waziri kalizungumzia vizuri, wafanyakazi wetu Mhe. Mwenyekiti, wanahitajika kuendelezwa kila baada ya kipindi. Ndio ile inayoitwa human resource development, haiwezekani leo mtumishi kakaa miaka miwili, mitano, kumi hajendapo kozi hata ya wiki moja. Haiwezekani, lazima serikali iwe na utaratibu maalum ya kuwapa mafunzo watendaji kila baada ya kipindi fulani.

Sambamba na hilo kuna suala zima la kuwadhibiti wale ambao tayari wameshapata taaluma. Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo kwa serikali kwani Zanzibar ina vijana wengi sana waliosoma na ni mategemeo katika nchi kadhaa ulimwenguni. Bado hatujawa na mipango sahihi na mipango madhubuti yakuweza kudhibiti hizi rasilimali zetu tulizonazo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tunapofika mahala mtu ameshapata elimu yake kikubwa anachokijua ule uzalendo siku zote mimi huzungumza uzalendo na njaa hauji, hata ukimuona mtu mzalendo huyo na ana njaa huyo ni peponi moja kwa moja. Mhe. Mwenyekiti, kitu kama hicho katika ulimwengu wa sasa hivi ni nadra kukipata kwani kila mtu hutaka maslahi bora.

Kwa hivyo, mimi ninachoishauri serikali katika hili ni kuwa serikali ifanye juhudi maalum ya kudhibiti vijana wetu hawa waliokuwa wana taaluma maalum. Hivyo isiwe siku zote tunazalisha watumishi wakuzitumikia nchi nyengine tunapoteza fedha nyingi, lakini vijana hawarudi nchini kuja kufanya kazi. Mhe. Mwenyekiti, lazima serikali jambo hili iliangalie kwa makini sana ili tufike pahala basi *resource* zetu tulizonazo hizi zirudi nchini kwa lengo la kuitumikia nchi na kujenga uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto nyengine tulizonazo ni tatizo hili la kuthibitisha kazini na malipo ya viinua mgongo. Mimi naomba niipongeze serikali tukubali kwamba serikali katika miaka ya karibuni imejitahidi sana na suala zima la viinua mgongo. Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa tulizonazo sasa hivi mtu leo akistaafu kwa kweli haifiki miezi mitatu tayari ameshamaliziwa mambo yake yote. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tumshukuru sana Mhe. Rais Karume aliyeondoka ni imani kwamba na Mhe. Dk. Shein ataendeleza kazi hii kwamba hata uislamu na dini nyengine zinasema kwamba mtu akimaliza kazi umlipe ujira wake kabla ya jasho halijakauka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mtu anapoacha kazi ama anapostaafu ni vyema mtu kupata malipo yake kabla ya jasho kukauka. Kwa hivyo, tunaiomba serikali iendelee na hilo na ikiwezekana malipo haya yarahisishwe iwe ni mapema zaidi kuliko muda unavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu tatizo la kuthibitishwa kazini sijui liko katika hatua gani maana yake Mwenyekiti niliwahi kupitia Baraza la Mji kama mfanyakazi, lakini pale palikuwa pana matatizo mtu alikuwa akifanya kazi zaidi ya miaka 40 siku ya kustaafu hapo huja kishindo kweli kweli. Mhe. Mwenyekiti, maana yake tayari mtu ameshastaafu anahitaji malipo yake anaambiwa wewe hujathibitishwa kazini, sijui hali sasa hivi ikoje, lakini kama hali iko mbaya naomba juhudi zichukuliwe ili matatizo kama haya yasijirudie tena.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na utumishi tulionao katika taasisi hizi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini katika Zanzibar ni wabia wakubwa wa Muungano, Muungano wetu huu Zanzibar ni sehemu ya Muungano na kuna taasisi za Muungano ambazo Wazanzibari wao ni sehemu ya wafanyakazi hao. Mhe. Mwenyekiti, taarifa tulizonazo ni kwamba hali hairidhishi kwani Wazanzibari wamekuwa ni wachache sana katika taasisi za Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, hebu Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie hali ikoje sasa au ana mkakati gani wa kuhakikisha kwamba nafasi katika taasisi za Muungano Zanzibar tunakuwa na *portion* yetu maalum kwa sababu hili limekuwa ni tatizo kubwa sana. Lakini sambamba na hilo jana ilizungumzwa hapa nafasi za Zanzibar katika taasisi za Kibalozi nalo vile vile kama Zanzibar kwa kweli tunahitaji kujua haki yetu kwa sababu kati ya sehemu ambazo tunaweza tukapata ajira kwa wingi ni katika taasisi kama hizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja katika majumuisho atuweke sawa katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niingie katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mimi naomba niungane na Wajumbe wa Kamati walivyotoa pongezi kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati wa PAC kwa karibu sana tunafanya kazi na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali na mimi napenda kukiri kwamba kwa kweli Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anafanya kazi kubwa sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitoe wito kwa taasisi za Serikali ziende kwenye ofisi kama ikiwa kuna sehemu ya kujifunza *management* kama ikiwa kuna sehemu ya kujifunza uongozi basi ni kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwa sababu hii ndivyo nilivyoamini ule usemi uliokuwa unazoeleka miongoni kwamba kweli “mwanamke ukimuwezesha anaweza”. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli utakapotembea tulikwenda siku moja katika Ofisi ya Mdhibiti na Katibu wangu wa Baraza ilibidi nimwambie Katibu wa Baraza soma kidogo hapa, maana yake tulishindwa kuzuia hisia zetu haidhuri Baraza ndio chombo chetu lakini tulimwambia Katibu soma hapa kwa mama huyu. Kwa hivyo, naomba niungane kwa kutoa pongezi hizo na tunasema hivyo ili kama alivyosema Mhe. Jussa asijegeuka mgema tembo akalitia maji. Kwa hivyo, sisi tunamuomba aendelee, aongeze bidii, aongeze juhudi na taasisi nyengine za serikali naamini kwamba sasa zitatiririka kwenda kuangalia utendaji katika taasisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni moja kati ya nyenzo kubwa sana yakuleta utawala bora katika nchi. Kama utashuhudi Mhe. Mwenyekiti, kwamba tutakuwepo zaidi ya mwezi mmoja katika kikao hiki kwa ajili ya kupitisha bajeti, tupo tunapitisha bajeti ya

matumizi ya serikali kwa kipindi cha mwaka mzima unaokuja. Lakini baada ya kupitisha hatua hii ya kuidhinisha matumizi, maana yake lazima matumizi hayo yakaguliwe. Mhe. Mwenyekiti, huo ndio utawala bora Baraza tunaidhinisha matumizi kwa serikali, lakini katika *accountability* maana yake na serikali nayo lazima iangaliwe namna inavyotumia. Mhe. Mwenyekiti, hii mana yake ni kutokutumia vibaya fursa hii tunayoipa serikali kwa ajili ya kutumia fedha za walipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo ofisi hii kwa kweli ina changamoto kubwa sana pamoja na juhudi yote aliyoichukua Mhe. Waziri kwa sababu naamini kwamba waziri amechukua juhudi kubwa ya kuongeza bajeti katika ofisi. Lakini bado bajeti haijakidhi haja, tunakushukuru kwanza Mhe. Waziri lakini lazima tukubali kwamba bado bajeti ya ofisi hii haijakidhi haja kwa sababu ofisi hizi zinakuwa na mtandao kidunia. Kunakuwa na *afrosae, introsae* hizi ni jumuiya za ofisi za ma-*audit* wote huungana pamoja na kujadiliana na kuangalia vipi mambo yanavyokwenda. Kwa sababu ofisi hizi hazifanyi kazi kama visiwa ni mitandao katika dunia.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema hapa kwamba sasa hivi dunia ya ukaguzi inakabiliwa na changamoto kubwa sana ya kuingia katika VSM. Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi chote tulichokuwa tunakwenda nacho hata ripoti ya mwaka 2009-2010 kama ilivyoeleza ile ripoti inaelezea ukaguzi wa matumizi. Mhe. Mwenyekiti, ni ukaguzi wa matumizi tu haijaingia ripoti ile kugusia ukaguzi unaohusiana na thamani halisi ya fedha. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ukaguzi huo umeshapitwa na wakati, leo unamwambia mtu atumie lakini ukenda pale akuoneshe risiti si zinauzwa tu humo mitaani zimejaa. Lakini je, fedha aliyoitumia ni kweli ameitumia na kama katumia kweli thamani alichokitumia kweli kinalingana na alivyotumia.

Mhe. Mwenyekiti, dunia sasa inaelekea huko na tayari wenzetu hata Bara wameshaingia katika eneo hilo muhimu, fedha nyingi za serikali zinakwenda katika manunuzi, fedha nyingi tunazozipitisha katika Baraza hili sasa zinakwenda katika manunuzi. Mhe. Mwenyekiti, katika manunuzi kunakuwa na ufisadi mkubwa hivyo sasa ni lazima Mdhibiti awezeshwe ili aweze kufanya kazi kwa sababu bila ya kuwezeshwa Mdhibiti hawezi akafanya kazi hiyo. Mimi nasema siku zote kwamba kama kweli tunataka utawala bora ni kuiwezesha Ofisi ya CAG. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya CAG tutakapoiwezesha nina hakika atatufanyia kazi ambayo tunaihitaji yakufichua mafisadi katika nchi hii bado mafisadi wamo na lazima tuwafichue sasa kwa ajili ya kuleta maslahi kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya VSM kama ilivyosema Kamati na hotuba ya Mhe. Waziri kwamba sasa hivi mambo yote yanakwenda kwa njia ya kompyuta

ukitaka risiti ya aina yoyote unakwenda kwenye kompyuta unaitoa risiti kama ilivyo. Kwa hivyo, bado tu hujamkamata mtu katika hapo, lazima sasa ofisi ya CAG ielekee huko lakini aina nyengine ya *auditing* lazima ifanywe ni ile *auditing* ya kimazingira kwa sababu hata sisi Wajumbe wa Baraza hili hatujajua kama mazingira sasa hivi yanaathari mbaya sana kwa uchumi wa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, neno mazingira lina athari mbaya sana kwa uchumi wa nchi na ndio wakubwa wetu katika dunia sasa hivi wameshaingia huko, sisi ndio kwanza tunashangaa tukisikia ukaguzi wa kimazingira ndio kwanza tunashangaa. Lakini tunajua namna gani mazingira yatakavyoharibika, maradhi yakaenea ni namna gani uchumi wa nchi unavyoweza kuathirika, namna gani ardhi yetu itakavyoweza kwena na maji na kusombwa na vitu vyengine. Kwa hivyo, hilo ni eneo ambalo lazima mdhibiti sasa wakati umeshafika ni lazima aelekezwe huko ili aweze kuliwezesha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala jengine ni suala la ukaguzi. Suala la ukaguzi sio suala la Muungano kwa sababu halimo katika orodha ya mambo ya Muungano na katika mambo hayo kuna mwahala ambapo Zanzibar na sisi tuna interest kwa uchumi wetu katika masuala ya mapato, na kwa kuwa Mdhibiti wa Bara hakupewa mamlaka na Katiba ya Muungano wala hakupewa idhini na Katiba ya Zanzibar kwamba ni moja kati ya taasisi nne zile zilizoruhusiwa kuja kufanya kazi yake hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ukiisoma Katiba ya Zanzibar kifungu 124 utaikuta hiyo kwamba kuna taasisi ambazo sio za Muungano lakini zinaruhusiwa na Katiba ya Zanzibar zifanye kazi zake Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, bahati mbaya sana Ofisi ya Mdhibiti Bara haijapewa ruhusa hiyo, hili suala sasa tunalifanya nini wakati sasa hivi Mdhibiti wetu hana ile fursa ya kukagua mambo kama hayo. Kama vile masuala ya mapato yanayotokana na utalii ambayo yanaingia kwenye *migration* mkaguzi hana uwezo huo. Leo fedha zinazoingia *migration* nani anayekagua hapa Mhe. Waziri atakapokuja hebu atupe somo kuhusu hili.

Mhe. Mwenyekiti, leo asubuhi tuliangalia hapa kwamba watalii wanapokuja kutokana nje hulipa *visa* katika Ofisi za Kibalozi, tunaomba tuelezwe namna gani mdhibiti wetu hupata fursa ya kwenda kuzifanyia *auditing* fedha zile kule. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri atakapokuja hapa atatueleza suala hilo la ukaguzi na masuala ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimtanabahishe Mhe. Waziri kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama nilivyosema haiendi peke yake lazima ajiunge katika jumuiya hizi. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba

tuna vigezo vyote Zanzibar tuna Katiba, Zanzibar tuna Serikali, Zanzibar tuna Bunge, Zanzibar tuna kila kitu ambacho kwa kweli kinatwambia kwamba sisi tayari ni nchi. Leo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali sio Mwanachama wa Afrosae wala sio mwanachama wa Introsae. Mhe. Mwenyekiti, kwenda katika vikao kama hivi ni ihsani tu ya Mdhibiti wa Bara kumchukua ama anaweza anaweza akamchukua ama asimchukue.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda katika mkutano mmoja na wakatwambia kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Afrika ya Kusini wana Mabunge yao madogo madogo wachilia mbali lile Bunge la Taifa, lakini wale wote ni wanachama katika Jumuiya hizi za Kiafrika. Kwa hivyo, kwa nini sisi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali asiwe ni mwanachama. Mhe. Mwenyekiti, ninachomuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ni namna gani atamuwezesha Mdhibiti wetu ili na yeye ajiunge na sisi Zanzibar tuendelee kunufaika na fursa ambazo zinapatikana katika Jumuiya hizi nilizozitaja.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba niseme kuwa kila mara huwa tuna ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo baadae PAC nayo huwa inatoa ripoti. Kwa hivyo, ripoti zile ni kipimo sasa tunachotaka kujua sisi Mhe. Waziri hebu twambie baada ya ripoti zile kutolewa na Mdhibiti pamoja na PAC serikali ina-*react* vipi na ripoti zile. Kwa sababu lengo sio kutoa ripoti tu, lengo tunataka tuone serikali inavyochukua hatua juu ya ripoti zile. Nani atakayekuja kutupa matokeo ya ripoti zile, ni wizara gani ambayo itachukua majukumu kutwambia jamani ripoti ya mwaka jana ya Kamati ya PAC ambayo inatokana na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, serikali ripoti ilieleza hivi na serikali inachukua majukumu haya na haya. Mhe. Mwenyekiti, tunataka tuambiwe nani ambaye atawajibika na kutoa ripoti mwisho wa mwaka unaofuatia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo basi naomba niunge mkono hoja, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Makadirio na Matumizi ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake iliyoonesha mwelekeo na imani ya serikali kwa wananchi wake. Hongera sana Mhe. Waziri kwa hotuba yako hii.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki kimekusanya mambo mengi sana karibu kimemaliza mambo yote watoto wa Mjini wanasema mboga zote zimo humu.

Kwa hivyo, mimi nafikiria michango yetu ndio maana utakuta Waheshimiwa Wajumbe michango yao inakuwa midogo sana, maana hukioni uongezee wapi ameshamaliza kila kitu Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, hapa ni kumpigia makofi tukaondoka na tumuidhinishie ili tumalize hadithi yetu lakini labda sehemu nyengine kidogo kidogo mna nyama nyama tuziongezee.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niende kwenye utawala bora, ni kwamba tunapita humo humo kwani ndio njia wenyewe ilivyo lazima tupite humo hamna pengine. Mhe. Mwenyekiti, neno utawala bora wenzangu waliopita Mhe. Hija alilizungumza sana hapa, lakini mimi zaidi nataka niende kwenye uwajibikaji kwa watumishi. Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo sugu sana kwa watumishi nilikuwa namuomba Mhe. Waziri aeke mikakati madhubuti ili watumishi wetu waweze kuwajibika pasi na kulazimishwa. Mhe. Mwenyekiti, kwani mtu hajichuni mwenyewe utaratibu wa kuingia kazini anajua ni saa moja na nusu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimekwenda kuna ofisi fulani siitaji basi saa mbili na dakika ishirini mtu wa masjala hajafika, basi nilikaa pale mpaka dakika ishirini na tatu ndio kaingia, ndio nikaacha barua mbaya. Kwa hivyo, ikiwa masjala saa mbili na dakika ishirini haijafunguliwa kazi zitaanza saa ngapi maana hata barua itakuwa hazipokelewi. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri kwenye hili akazisimamia zile sheria ambazo tumezipitisha hapa vizuri ili watu waweze kuwajibika.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi wanakwenda kwenye maofisi hasa ya serikali ndio kwenye tatizo, haya ya binafsi hayana tatizo sana maana wanayasimamia wenyewe. Lakini ukija kwenye serikali ndio kwenye tatizo huduma zinatolewa kwa mtu anavyopenda yeye, na mtu yule ukimwambia ndio huduma huipati kabisa na sehemu ya kulalamika huna. Mhe. Mwenyekiti, ingawa katika maelezo yake humu niliposoma hiki kitabu nimeona kuna pahala anasema unatakiwa kupeleka malalamiko.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba bado suala la uwajibikaji ni zito kidogo, mimi ningetoa ushauri tungeacha kufanya kazi kwa mazoea. Kwa hivyo, hili kama utaisimamia vizuri mimi nina hakika utawala bora utapatikana vizuri, maana mtu ambaye amepewa dhamana sehemu ikiwa yeye mwenyewe aliyepewa hiyo dhamana anaingia pale saa tatu na nusu, hawa anaowasimamia wataingia saa ngapi. Kwa hivyo, hawezi kujua kwamba wamekuja saa mbili au saa mbili na nusu akifika yeye saa tatu na nusu kwa sababu wanamjua bosi anakuja saa tatu nusu basi wao wataingia saa tatu na robo ili akija yeye anawakuta wameshafika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ofisi mimi nishakwenda siku moja saa moja na nusu basi hata ile milango haijafunguliwa. Mimi nikauliza leo hapa hapafanywi kazi wakasema ndio tumefika hivi. Kwa hivyo, tuone namna gani wasivyoweza kuwajibika Mhe. Waziri sijui utakuja kutueleza nini hapa ni mkakati gani ambao umeuweka wa kuhakikisha kwamba watu wanawajibika katika sehemu zao za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala zima la kutoa elimu ya uraia kwa wananchi nalo pia mimi nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri utakapokuja hapa utueleze kidogo mikakati yako juu ya namna utakavyoliendesha zoezi hili kwani nalo ni muhimu kwa wananchi wetu, ili waweze kupata elimu ya uraia wakajua zile haki zao za msingi. Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukakuta unadaiwa mambo pengine sio haki yake, lakini kwa sababu hajui basi akawa anayadai, na yale asiyoyoyadai akayaacha. Kwa hivyo, ningekuomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa hebu utupe ile mikakati hasa uliyoiweka kuhakikisha kwamba zoezi hili linafikia malengo.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la elimu ya uraia nilisogea pale kwenye kifungu cha 45 nimeona kwenye suala la kupeleka malalamiko katika sehemu hizi wanazokwenda kupewa huduma ili kuweza kuupata ule utawala bora. Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri ameweka mahala kwamba wananchi watoe malalamiko yao. Mimi ningekuomba Mhe. Waziri uje utupe maelezo kidogo maana mimi sikufahamu vizuri, yale malalamiko yanatolewa wapi isijekuwa tunaweka malalamiko mahala akisha yule ambaye tunamlalamikia ndio mfunguaji mwenyewe akatizama linalomkera yeye akaondosha, lisilomkera ndio akalipeleka.

Mhe. Mwenyekiti, pia nisogee kidogo kwenye Idara ya Makumbusho na Nyaraka. Mimi nahisi idara kama imesahauliwa kidogo maana yake kama Makumbusho ninayoyaona mimi naona yamechoka kidogo. Vile vile niliwahi kutembelea sehemu za Unguja Ukuu nikakuta jengo nikaambiwa ni la Makumbusho kwamba lilikusudiwa kuwekwa Makumbusho ya kitaifa. Kwa hivyo, lile jengo naona limeachwa kabisa kama halina mwenyewe sijui utaratibu wake ukoje juu ya jambo lile kwa sababu pale palitengenezwa pesa za serikali zimetumika pale. Zile pesa zilotumika pale ni pesa za wananchi ni nyingi kwa kiasi kwa sababu lilimaliza, limeanza kuwekwa milango, madirisha lakini hatujui limemalizikia vipi naona limeachwa tu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja hapa hebu kidogo tusaidie katika hili ili tuweze kuona ofisi yako imejipanga vipi katika kuliendeleza jengo lile au umeachana nalo tunaomba tuweze kupata ufafanuzi katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiendelea sasa nije kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli kama alivyotangulia kusema

Mwenyekiti wa Kamati ya PAC pale huyu mama anastahili hongera sana kabisa. Mhe. Mwenyekiti, mama huyu ni kioo cha watumishi wengine wakaangalie pale jitihada zake na namna gani utawala bora unavyofanya kazi pale. Mhe. Mwenyekiti, mama huyu anapita mle kwenye ule utaratibu unaotakiwa, Mhe. Waziri pale umepata kifaa nakuomba ukitunze na ukiendeleze. Mhe. Mwenyekiti, mimi nisizame kwa sababu Mwenyekiti wa PAC ameshamaliza yote juu ya ofisi ile. Kwa hivyo, amenifilisi nisirejee yale yale ambayo yeye ameshayazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala la mishahara hii nyongeza aliyoizungumza Mhe. Waziri hapa. Mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa nyongeza hii ya mishahara ya kima cha chini. Hongera sana, lakini mimi nina malalamiko kidogo kule kuanza kutumika kwake kunaanza mwezi wa Oktoba imekuwa kama hawa wafanyakazi wamenusishwa tu. Mhe. Mwenyekiti, kama kulikuwa hakujakaa vizuri mimi ningeshauri kwa nini isianze ukaitangaza kwa muda unaofuata, lakini ukitangaza leo halafu watu wasubiri mpaka Oktoba naona ni muda mrefu sana kwa kustahamili kusubiri hiyo nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wanaweza kukata tamaa kwani miezi mitatu ni mingi sana, hakuna uwezekano wa kuisogeza nyongeza hii ikaanza katika mwezi wa Julai maana sababu zilizoandikwa mle ni ufinyu wa bajeti. Kwa hivyo, mimi nashangaa ufinyu wa bajeti ndio kwanza bajeti yenyewe tunaianza mwezi huu wa Julai. Huku nyuma ungetuletea kwenye mwezi wa tano ungetwambia vyengine tungejua hii bajeti sio yako umeikuta tu unaiendeleza. Lakini hii mpya ambayo tunaianza mwezi wa Julai kwa nini isianzie Julai hii nyongeza. Mimi nafikiria Mhe. Waziri hebu kaeni vizuri ili utakapokuja hapa utusaidie kidogo kwa nini wasipatiwe uwezekano wakaanza kwenye mwezi wa Julai ambapo ndio matumizi ya hiyo bajeti yanaanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi nafikiria nisiende zaidi niunge mkono hoja mia kwa mia mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Mkwajuni hatuna tatizo na hili, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kidogo hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuweka hapa tukiwa haia na wazima. Pili, nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii leo ya kusimama hapa kwa kuchangia. Tatu, napenda kumpa pongezi zangu nyingi sana Waziri wetu wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haji Omar Kheir.

Kwa kweli nichukue fursa hii pia kumpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa yeye ni mfanyakazi bora na ni mfanyakazi mzuri ameamua kutuundia wizara hii ili kuhakikisha kwamba kazi zinafanywa vizuri, maslahi ya wafanyakazi yatakuwa mazuri na tutajipanga vizuri katika kazi ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Lakini juu ya hayo, Mhe. Rais amemteuwa Mhe. Waziri ili kuhakikisha kwamba hii wizara inakwenda vizuri kwa sababu anafahamu uwezo wake na ninamuombea dua Mwenyezi Mungu amujaalie waziri huyu aweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza katika ukurasa wa 20 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Nimefurahi sana idara hii kuwa leo imewekwa katika wizara ambayo itakuwa msimamizi mkuu wa nyaraka zetu. Kwa sababu kwa kipindi kirefu sana nyaraka zetu zimekuwa zinaharibiwa. Si hivyo tu, pia kuna upotevu mkubwa sana wa nyaraka za Zanzibar.

Zanzibar ina historia kubwa na Zanzibar ina historia ndefu. Sasa lakini nyaraka nyingi za Zanzibar zimepotea na hatujui tuzitafutie wapi, nyaraka zenye historia ndizo zilizotupa umaarufu hapa Zanzibar.

Mimi nilipata bahati nikatembelea Ujerumani, nilipofika kule kwa bahati nzuri nikaenda sehemu ambako wanahifadhi nyaraka. Katika ofisi ile tulikuta nyaraka za Zanzibar, nyaraka ambazo zina miaka mia moja, lakini kwa bahati mbaya nyaraka hizo Zanzibar hazipo, zilikuwa ni nyaraka ambazo zina historia ya Zanzibar namna walivyoanza biashara na nchi za nje. Tulikuja kutambua kwamba Zanzibar katika Afrika Mashariki ilikuwa ni nchi ya mwanzo ambayo ilianza biashara na nchi za Ulaya na Asia. Nina wasi wasi mkubwa mpaka hii leo sijui hata kama nyaraka hizo ziliweza kuletwa Zanzibar kwa sababu tuliomba na kwa bahati nzuri alikuwepo afisa ambaye anashughulika na nyaraka katika idara hiyo na kuambiwa kwamba pengine zitaweza kuletwa Zanzibar.

Mwenzangu aliyepita amezungumzia suala la makumbusho. Mhe. Mwenyekiti, Makumbusho zetu sehemu ambazo tumeweka utamaduni wetu zimekufa kabisa, zimekufa kwa sababu sisi wenyewe hatujijali. Kwa sababu tungekuwa tunajali historia yetu mimi naamini kabisa kwamba majengo yale tungeyatunza na leo hii watoto wetu wangeweza kutambua historia ya Zanzibar vizuri sana, lakini pia tungekuwa na uwezo wa kuwavutia watalii wengi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda katika ukurasa wa 28 ukurasa ambao unazungumzia masuala ya UKIMWI katika ajira ambapo nafikiria kuwa wizara hii itafanya jambo la busara kuhakikisha kwamba mafunzo maalum yatatolewa

kwa wafanyakazi ili kupunguza maambukizo mapya ya Ukimwi. Ukimwi bado ni janga na wizara ina kila sabbabu kuhakikisha kwamba maambukizi yanapunguzwa. Sasa basi, elimu inayotolewa katika mawizara haya au fedha ambazo zinaingia katika sehemu hizi mara nyingi sana zinakuwa fedha zile kwa kweli hazifanyi lile ambalo limetarajiwa kufanywa.

Mara nyingi sana miradi ile pesa zinapofika huwa haitekelezwi au pesa pengine zinahamishwa zinapelekwa katika kifungu kingine. Ningemuomba Mhe. Waziri ahakikishe elimu hii inatolewa vizuri inamfikia kila mfanyakazi wa serikalini.

Katika kifungu hicho hicho Mhe. Mwenyekiti, tumezungumzia suala la uajiri na jinsia. Mhe. Mwenyekiti, ,wakati niko katika kamati mimi nilikuwa mkorofi sana wa kuuliza, wanawake wako wangapi katika ofisi hii? Baadhi ya ofisi nikagundua kwamba hakuna jinsia kwamba ofisi wanaume wako 50 pengine wanawake wako 10, hapana usawa. Wapo wanawake ambao wanaweza kufanya kazi zile zile ambazo wanazifanya wanaume, lakini kwa bahati mbaya hawapewi nafasi kwa sababu labda ni mwanamke au sababu nyengine ambazo huwa mara nyingi tunazishuku sisi wanawake wenyewe, kwamba labda inabidi tuwaridhishe wale ambao wanataka kutuajiri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nazungumzia umri, nataka aje aniambie hapa Mhe. Waziri kwa nini wanawake tunastaafishwa mapema? Ikiwa tunazungumzia usawa kwa nini wanaume wanapewa muda mrefu wa kufanya kazi wanawake wanaambiwa wafanye kazi mpaka kufikia umri wa miaka 55. Kuna sababu gani? Tupewe sababu labda pengine maumbile yetu au vipi, twambieni tujue, lakini wanawake wanaweza. Wako wanawake wanaacha kazi kwa kustaafishwa kwenye maofisi ya serikali wanatafuta kazi za *private* wanafanya wengi sana, wanawake wengi ambao wameanzisha *NGOs* haba Zanzibar ni wanawake ambao walikuwa wana uwezo mzuri sana wa kuendelea kufanya kazi serikalini, wameacha kwa sababu ya umri wao tu, leo wanatumika katika *NGOs*.

Sasa mimi nafikiri Mhe. Waziri hili tuliangalie tena, kama tunakwenda katika dunia ambayo inasema watu wote ni sawa basi na hili tulifanye sawa, yule ambaye anataka kustaafu mapema na astaafishwe, lakini yule ambaye ana uwezo wa kuendelea basi umri uwe sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia maslahi ya wafanyakazi. Kwa kipindi kirefu sana wafanyakazi wamekuwa maslahi yao ni madogo. Nashukuru sana kwamba sasa serikali imeona kuna umuhimu mkubwa sana kwa wafanyakazi sasa hivi maslahi yao yaongezwe, lakini la msingi lilikuwa ni posho. Wafanyakazi katika wizara nyengine utakuta wanapata posho lakini ukija mawizara mengine

hawana posho, kwa sababu gani? Kulikuwa na wizara maalum hizo kila siku wao wanapata posho lakini kuna wizara nyengine posho hawalijui. Posho la likizo kuna watu hapa tangu wameanza kazi pengine miaka mitano au sita hajui nini maana ya posho la likizo. Mhe. Waziri waangalie wafanyakazi, tunawaambia watu wafanye kazi lakini na maslahi yao tuyaweke vizuri ili na wao wafanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia Utawala Bora. Kama wenzangu walivyosema una dhana pana sana, sasa basi, kila mtu awajibike sio mfanyakazi tu, pamoja na viongozi wawajibike kwenye utawala bora tuwe wawazi. Utawala bora hauendi bila ya kuwa wazi, unaingia ofisini nyengine unakuta taarifa muhimu wafanyakazi wengine hawazijui anazijua bosi tu, hakuna sababu hebu toeni mafunzo ya *Comunication Skills* watu waelewane ndani ya maofisi.

Taarifa nyingi lazima unaambiwa wende kwa fulani au fulani, hata yule pengine afisa anayehusika anakuwa hana taarifa atakwambia nenda kwa katibu au kwa mkurugenzi kwa nini? Wakati pengine yeye ni moja katika jukumu lake lakini taarifa hana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nafikiri katika kipindi hiki viongozi wetu wengi wa serikalini wamekuwa wakipata semina mbali mbali kuhakikisha kuwa wanakuwa viongozi bora, sasa watekeleze. Kinachotakikana sasa ni utekelezaji tu, lakini mafunzo wameshayapata.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kwamba nimeona kutakuwa kunafanywa *capacity assessment*. Ni kweli kama wenzangu waliotangulia kusema kwamba kuna baadhiya wafanyakazi katika maofisi kwa kweli hawafai, hawafai kabisa. Inawezekana ana *degree* au nini lakini pale akifika ofisini anakuwa hafai, aidha hafanyi kazi kama inavyotakiwa au uwezo wake wa kufanyakazi ni mdogo.

Mimi nimefanya kazi serikalini ninajua, ukitoka skuli mwanzo ukifika pale kuna tatizo kwamba wale walioko juu mara nyingi huwa wanaogopa na hata mafunzo ya kazi pale ofisini mfanyakazi ambaye kaja mpya anakuwa hayapati, anaambiwa si anajidai kasoma na afanye basi. Sasa mimi nafikiria kuwe na utaratibu mzuri sana wa kwamba kila mfanyakazi afanyiwe *assessment* ili ajulikane uwezo wake. Hiyo ni bora ifanywe kila mwaka na inawezekana na sio iwe kwa katibu tu au mkurugenzi, lakini iwe kwa kila mfanyakazi hata yule mfagiaji. Kwa sababu kila mmoja amepewa jukumu la kuwajibika kwa hivyo, ajue anawajibika vipi na kwa nani.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuzungumzia suala la elimu kwa wafanyakazi. Kwa kweli nitarudia yale yale kuwa wafanyakazi wengi katika maidara mbali mbali wengine wametupwa kabisa hawapati mafunzo, kama alivyosema mwenzangu kwamba inatakiwa kila mwaka mfanyakazi katika

serikali au taasisi yoyote apewe mafunzo, ajengwe uwezo na mfanyakazi yule mkimuacha nyuma kazi haiwezi kufanyika kwa sababu umemshamnyima uwezo wa kufanya kazi yake. Kwa hivyo, ni vizuri kwamba kila mfanyakazi serikalini awe na haki sawa na mwengine kupata elimu. Nasema hivyo kwa sababu kuna wengine wanapata fursa na wengine hawapati na sijui kinakuwa ni kitu gani hasa kinachosababisha kuwa fulani apate na fulani asipate. Sasa tunazungumzia utawala bora lakini pia tuzungumzie haki sawa.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wetu serikalini wengi wana kilio cha kutaka kwenda kusoma lakini hawapati fursa ya kwenda kutokana na malipo kuwa hapati katika taasisi zao. Mfanyakazi ana nia ya kwenda kusoma lakini anaambiwa kwamba sasa hivi huwezi kusoma kwa sababu hamna fedha za kusomeshea, tena wengine mara nyingi huwa wanaomba angalau walipiwe zile *tuition fee*. Sasa nafikiri kama kweli tumekusudia Wazanzibari wafanyekazi tuwape fursa ya kwenda kusoma Vyuo Vikuu wale ambao wanataka kusoma, tuna Vyuo Vikuu vingi sana Zanzibar sasa hivi vya kuwasomesha wafanyakazi wetu tutumie fursa hiyo, serikali ijikite.

Mhe. Mwenyekiti, elimu ni ufunguo wa maendeleo bila ya elimu kwa kweli hatutofika mbali. Elimu sio lazima mtu aisome skuli kuanzia darasa la kwanza au langapi, elimu hata mtu mzima anaweza kusoma, tumepata viongozi wengi sana katika serikali hii yetu ambao wamesoma wakiwa watu wazima na wameelimika wametambua, leo wengine ni viongozi wetu. Sasa basi, kuna umuhimu sana wa kuwapa elimu wafanyakazi wetu, lakini vile vile utoaji wa vyeo.

Mhe. Waziri licha ya kuwa kuwe na uwiyano wa kupata vyeo wanawake na wanaume kwa sababu kuna umuhimu wake, pia wanawake nao wapewe vyeo wanaweza. Mwanamke anafanya kazi miaka 20 lakini atakuja mwanamme kwa muda wa miaka mitano atapanda cheo yeye mwanamke hapandi maisha.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe baada ya kwisha kumsikiliza Mwenyekiti wetu Mhe. Mgeni Hassan Juma tumebakiwa na wachangiaji wanne *back benchers* pamoja na Naibu Waziri mmoja, hawa *Inshaallah* tutamaliza kesho tukijaaliwa halatu tutaendelea na taratibu nyengine.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 1/07/2011 saa 3:00 asubuhi)